Damu nyeusi,

DAMU NYEUSI

Ken Walibora

Dhamira Ya Mtunzi

Dhamira ya mwandishi ilikuwa ni kuelezea namna ubaguzi wa rangi ulivyosakini katika nchi ya Marekamo. Kwa mfano, Mwafrika ambaye heunda huko kwa malengo ya kujijengea msingi wa maisha ya baadaye hukumbana ana kwa ana na dhiki za kubaguliwa kutokana na weusi wao na mataifa ya Afrika walikotoka. Ingawa katika nchi hiyo kuna watu weusi ambao ni Waamerika, huwa hawana imani na watu weusi waliofika huko. Kadhalika, imebainishwa kuwa ubaguzi kwa misingi ya rangi ya ngozi hauna msingi wowote, kwani binadamu ni binadamu.

Maudhui

1. **Ubaguzi wa Rangi**

   Katika hadithi hii, imebainishwa kuwa Mwafrika hubaguliwa kwa misingi ya kule alikotoka na pia kutokana na rangi zao. Kwa hivyo, hubaguliwa katika hali mbalimbali. Kwa mfano, baadhi ya watu weupe wana mwelekeo hasi kuhusu Afrika. Fikirini anaulizwa, “Ni upi mji mkuu wa Afrika?” (Uk.23), “Je, mwaishi kwenye miti kama tumbiri?” (Uk.23) mwingine anadai “Nasikia wasichana wenu wote mnawakeketa na kuwashona ili kuzuia ukware?” (Uk.23). Mambo hayo yanamfanya Fikirini kutambua kuwa Mwafrika ni mtu asiyependwa, asiyependeka na wengine? (Uk.23).
   Kadhalika, watu weupe huchukulia kuwa Bara la Afrika limejaa uchawi na ushirikina (Uk.27). Isitoshe, hakuna anayejali maslahi au mahitaji ya mtu mweusi. Kwa mfano, dereva Mzungu wa basi alimwacha Fikirini katika kituo cha basi ingawa dereva alitarajiwa kumhudumia msafiri.
   Swali tunaloweza kujiuliza hapa ni: Je, kama Fikirini angekuwa mtu mweupe angehudumiwa? Jibu ni ndio!
   Zaidi ya hayo, mtu mweusi anakejeliwa. “Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua?” (Uk.23). Sheria ya nchi ya Marekani inawabagua watu kwa misingi ya rangi zao. Kwa mfano, Fikirini ametozwa “marambili” faini na polisi Mzungu kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekezea magari zikiwa zimewaka rangi nyekundu.” (Uk.23).
   Tatizo hapa hi kwamba wapita njia Wazungu waliachiwa kuvuka barabara na wala hawakuadhibiwa.
   Huko chuoni, mambo hayakuwa mazuri pia kwa sababu, “Wahadhiri wantoa alama kwa kupendelea watu weupe na kuwakandamiza weusi” (Uk.24)

siku moja, Fikirini alipokuwa akitembea na kufurahisha macho madukani, alituhumiwa mwizi au mdokozi. Kwa hivyo, mtu mweusi amekuwa haaminiki miongoni mwa weupe.

Kadhalika, Fikirini anapatikana na hatia wakati alipokuwa amesahau kufunga zipu ya suruali yake.

Wakati huo alijiambia kuwa kama angekuwa kwao Afrika, angefanyiwa hisani kwa kuambiwa, "Aisee funga duka" (Uk.24). Uhalisi wa mambo unamjia Fikirini kuwa magereza ya ughaibuni ni "jela imeundiwa mtu mweusi" (Uk.24). Dhiki hizo hazitkutokana na watu weupe tu bali pia na Wazungu weusi.

Weusi hao hawataki kuwaona wenye rangi nyeusi kutoka Afrika. Kwa mfano, Fikirini alipokutana na "pandikizi la jimama limekula likashiba" (Uk.25), alidhani kuwa amekutana na Mwafrika mwenzake kumbe hilo silo.

Kutokana na mazungumzo yao, Fikirini anabaini kuwa huyo mwanamke kwa jina Fiona alikuwa jambazi aliyeshirikiana na Bob, jambazi mwenzake. Katika nyumba hiyom Fikirini anapata vistisho vya kulipuliwa kwa bastola. Fikirini anatambua uzuri wa kwao alikotoka. Tahadhari zilikuwa zikitolewa na viongozi kama vile Baba wa Taifa la Kenya rais Daniel arap Moi, "msifikiri kwamba mzungu anatupenda sisi watu weusi" (Uk.22). nasah hizo zilikura zikipuuziliwa na baadhi ya watu huku wakitamani kuenda ughaibuni.

Tunaarifiwa kwamba majela kajengewa waafrika au watu weusi kutokana na dhaha kwamba wao ndio wavunja sheria.

Ni bayana kuwa jaji mweusi aliyemtoza Fikirini dola mia mbili aifanya hivyo akizingatia kuwa alikuwa akimhukumu mweusi mwenzake.

2. Elimu ya Ughaibuni

Baadhi ya vijana kutoka mataifa ya Afrika kama vile Kenya, wamekuwa wakitamani kupata elimu ya juu kutoka Ughaibuni. Matumaoni yao ni kwamba elimu hiyo ingewafanya kujijengea ngome imara ya maisha na wangeweza kuutumia ujuzi wao katika kuuinua uchumi wa mataifa walikotoka. Kwa hivyo, mtu anapopata nafasi ya kuendeleza masomo huko ughaibuni huichukulia kuwa ni jambo la fahari. Imebainishwa katika hadithi hii kuwa wanafunzi weusi wanapoenda kusoma huko ughaibuni hubaguliwa kirangi na kielimu. Mwandishi kwa mfano anasema;

(i) Wahadhiri wanatoa alama kwa kupendelea watu weupe na kuwakandamiza weusi. (Uk.24)

(ii) Mwanafunzi wa uzamifu katika somo la kiingereza huchukuliwa kuwa hana ufahamu kiingereza. (Uk.24)

(iii) Mhadhiri Mzungu na wanafunzi darasani (Uk.23) hawasiti kuuliza wanafunzi Waafrika maswali ya kudhalilisha na kudunisha

(iv) Mwanafunzi mweusi hujuta kuenda kusomea ughaibuni. Kwa mfano, Fikirini anasema kuwa: "Anaomba tu muda wake wa masomo umalizike, ahitimu arudi kwao." (Uk.23)

Kadhalika, mtunzi amehimiza kwamba mwanafunzi anapopata fursa ya kujiendeleza kimasomo anapaswa kuzingatia yale yaliyompeleka huko. Kwa mfano, kuziba masikio kuhusu sitihozai anazofanyiwa, kuwa mwadilifu na anapomaliza masomo arudi nyumbani ili kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

3. Upweke

Suala la upweke limesawiriwa kupitia kwa mhusika Fikirini. Kabla ya Fikirini kuendea Ughaibuni, alifikiria kuwa watu wa huko watakuwa wakarimu kama vili ilivyo kwao. Anapofika huko Marekani, anagundua kuwa:

(i) Mazingira hayo si kama yale aliyoyazoea; kuna baridi shadidi na theluji kali (Uk.22)
(ii)Lazima avae mavazi na viatu vizito. (Uk.22)
(iii) Hawaa za starehe si lolote si chochote na kila wakati mtu mweusi hushukiwa mwizi, jambazi na mdokozi.
(iv) Hakuna urafiki wa dhati.

Kadhalika, wanadhiri na wanafunzi wenzake wanamuuliza Fikirini maswali ya kmdunisha. Vilevile, rangi yake nyeusi inamtia doa na kila anapopita hujihisi hana raha. Msaada haupatikani popote ila kwake yeye na maisha anayokabiliana nayo. Upweke huo unamfanya Fikirini kutaka, “muda wake wa masomo umalizike” (Uk. 23) haraka ili arudi nyumbani. Mtazamo wa mwandishi ni kwamba, “hakuna mahali kama nyumbani, “Nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni.” (Uk.23)

Maudhui mengine yanayoweza kuzingatiwa ni kama vile:

4. Ukosefu wa Utu

Mwanafunzi azingatie:

(i) Fikirini alivyoachwa katika kituo cha basin a dereva Mzungu. (Uk.22)
(ii) Wanafunzi weusi kubaguliwa chuoni hasa na wahadhiri ingawa wanafunzi hao walikura hodari katika masomo. (Uk.24)
(iii) Fikirini kufanyiwa dhihaka za kumdharau. (Uk.23)
(iv) Fikirini kushinikizwa kufanya mapenzi na pandikizi la jimama. (Uk.25)
(v) Fikirini kupatikana na hatia ingawa wenziwe weupe wanasamehewa. (Uk.24)
(vi) Fikirini kulazimishwa kuvua nguo na kubaki uchi wa mnyama. (Uk.27)
(vii)Kuporwa mali na kutupwa nje kwa barafu na theluji akiwa uchi wa mnyama.
(viii) Fiona alimsingizia Fikirini kuwa alitaka kumbaka. Huku kulikuwa kumdhalilisha.
(ix) Fiona alikuwa anatishia kumkata Fikirini mrija wake alipoona kwamba Bob hataki kumpiga Fikirini risasi.
(x) Bob na Fiona walimrusha Fikirini nje kwenye theluji na barafu huku akiwa uchi wa mnyama.

5. **Chuki Dhidi ya Wageni**

Waafrika hawapokelewi kwa mikono miwili kule marekani ndiposa wanakejeliwa kudhililishwa na kuadhibiwa. Pia chuki hizi zinadhihirika wakati Bob anapomuuliza Fikirini, "Nini kinawatoeni Afrika kuja kutusumbua hapa Marekani?" Kisha "Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina wenu?" (Uk.27)

Bob anapomwita Fikirini tumbiri baada ya kusalamiwa, ni dhihirisho kuwa bob ana chuki dhidi ya wageni

Maswali ya dhihaka ambayo Fikirini alikuwa anaulizwa pia ni dhihirisho la chuki miongoni mwa wazungu dhidi ya weusi.

6. **Usaliti**

Mwanafunzi azingatie:

(i) Fikirini kuombwa kufanya mapenzi na Fiona ilhali Fiona ana mbinu za kumnasa wala hana mapenzi naye.
(ii) Fiona alimlaghai Fikirini kuwa angemsaidia lakini anageuka kumtesa na kumpora.
(iii) Fikirini kuwasabahi watu weusi akidhani kuwa ni waafrika.
(iv) Bob na Fiona wanamtesa Fikirini na ilhali wao pia wana asili ya Afrika.
(v) Mwanamke mzungu anamwita polisi aje kumshika Fikirini baada ya kumwona amewacha zipu wazi. Alifaa kumkosoa.
(vi) Wazungu wana mtazamo hasi kuwahusu weusi na ilhali wao hushirikiana katika mambo mengi kama vile biashara.

7. **Utengano**

Mwanafunzi azingatie:

(i) Utengano wa rangi.
(ii) Utengano wa fikira na mielekeo.
(iii) Utengano wa tamaduni.
(iv) Utengano wa kielimu na kinafsia.

8. **Kasumba**

Wazungu wana dhana potofu kuwa weusi hawajui kiingereza.

Fikirini anadunishwa kiasi cha kuitwa tumbiri na bob punde alipomsalimu akimwita ndugu. Bob anamwona Fikirini kama kitu duni kinachoweza kumithiliswa na mnyama.

Usawiri wa Ujenzi wa Wahusika

Hadithi hii haina wahusika wengi waliojidhihirisha wazi. Mhusika mkuu ni Fikirini. Fiona na Bob ni wahusika wadogo.

1. **Fikirini**

Ni mhusika mkuu katika hadithi hii. Ameenda Marekani ili kujipatia elimu ya juu ya uzamifu.

a) *Ni mvumilivu* na mwenye matumaini. Kwa mfano, anapoachwa na basi anaamua kuendelea na safari yake ya kuenda chuoni. Ingawa anafanyiuwa stihizai na wahadhiri na wanachuo wenzake, yeye anaandama masomo yaliyompeleka huko. Amekuwa akijiliwaza kuwa atakapomaliza masomo atarejea kwao.
b) *Ana msimamo thabiti/ Mwadilifu* hasa katika masuala ya kimapenzi. Kwa mfano, Fiona anapomshurutisha wakati Fiona huyo anapomwambia kuwa, By the way, do you want a good time?" (Uk. 26). Fikirini alikataa kujihusisha na maswala ya mapenzi.
c) *Ana utu*. Aliwachukulia weusi wenzake kuwa ndugu na dada. Kwa mfano, Fikirini "....alipomuona mweusi mwenzake, alikumbuka dada zake kule nyumbani Afrika Mashariki" (UK.25). Jambo lililomkirihisha zaidi Fikirini ni ubaguzi ukiosakini katika jamii za weupe. Alitaka autokemeze.
d) *Mwenye papara.* Hufanya maamuzi ya haraka bila ya kufikiria. Kwa mfano, jimama jeusi la Marekani lilipomwendea kwa hadaa, Fikirini anaamua kwa haraka kuandamana naye hadi katika makazi yake.
e) *Ni mwoga.* Anapotishwa kwa mtutu wa bastola, tunaambiwa Fikirini aliumimina "mkojo kwenye sakafu ya ukumbi" (Uk.29) Kadhalika, "Fikirini alimuona yule dasa akikielekeza kisu kweny kinena chake, akachutama na kumwomba amwonee imani" (Uk.29)
f) *Ni mmakinifu.* Anaelewa kuwa kule alikoenda alifuata masomo ambayo yangesaidia katika kuimarisha uchumi wa nchi yake. Kwa hivyo, hakutaka kubabaishwa na hawaa za ughaibuni.
g) *Msomi* – kutokana na hadithi tunaona kuwa ameshasoma hadi akapata shahada ya kwanza na sasa amesafiri ughaibuni ili aweze kupata shahada ya uzamifu katika kiingereza.
h) *Mzalendo* – Yeye anaipenda nchi yake jinsi ilivya na ndiposa anasema kuwa angependa kurudi kwa ili akafaidi kutokana na umaskini wa kwao. Anavipenda vyakula na vileo vya kwao.

Umuhimi wa Mhusika Fikirini

(i) Mwandishi ametumia kuonyesha dhiki wanazopitia watu weusi wanaokwenda ughaibuni.
(ii) Ni kielelezo cha wageni ambao licha ya kujipata katika mazingira tofauti, hawabadiliki. Angali na utu wake hata baada ya kuhishi miongoni mwa watu wasio na utu.
(iii)Mwandishi amemtumia kuonya. Waafrika wanaokimbilia nchi za kigeni wakitarajia kupata utulivu.

2. Fiona

Ni mwanamke jambazi ambaye ni Mwamerika mweusi.yeye ni dadake bob. Ingawa ngozi yake ni nyeusi, hawapendi Waafrika.

a) *Ni asherati*. Si mwanamke ambaye ni mwadilifu, kwa sabadu huwavuta vijana wa kiume kufanya mapenzi naye. Kwa mfano, anamwambia Fikirini, "*Do you want a good time*?" (Uk.26.Hapa aliashiria kuwa alitaka washiriki ngono.
b) *Ni msaliti.* Anaishi maisha ya ujambazi na kuwasaliti watu walio katika shida kwa kujifanya atawasaidia. Hali hiyo imedhihirishwa wakati alipokutana na Fikirini na kumrai ili aende naye kwake kwa malengo ya kumpora. Alipogundua kuwa Fikirini hakubaliani na fikra zake, anamsingizia ubakaji.
c) *Ni mtu chachari.* Ni mtu ambaye hana huruma kwa sababu alimtaka Bob amuue Fikirini. Kwa mfano, anamsisitizia Bob, "*I say shoot him Bob*!" (Uk.29). Aidha, alikuwa na kisu cha kumtishia Fikirini.
d) *Ni mporaji na tapeli*. Anamtapeli Fikirini kuwa atamsaidia kufika chuoni na hatimaye kumtia katika shida za umateka.
e) *Ni katili* – Anatishia kuukata mrija wa fikirini anapoona Bob akisita kumlipua kwa bastola. Anamchochea bob ampige Fikirini risasi eti kwa sababu hana pesa.
f) *Mnafiki*- Yeye hujifanya msamaria mwema anapowaona watu wakiwa matatani kisha huwageuka baadaye na kuwapora.

Umuhimu wa Mhusika Fiona

(i) Ametumiwa kuonyesha jinsi Waamerika huwadhulumu weusi wenzao kutoka Afrika.
(ii)Mwandishi amemtumia kuonya wasomaji dhidi ya kuwaamini watu ambao hawawajui vizuri. Wachuje mambo badala ya kuyaparamia.
(iii) Ametumiwa kama kielelezo cha unafiki na ukosefu wa utu.

3. Bob

Ni mwamerikani mweusi ambaye Fiona anadai ni kakake.

a) *Ni jambazi*. Anaishi maisha ya ujambazi. Tofauti na dada yake, Bob hutekeleza ujambazi kwa tahadhari ili asije akajikuta hatiani. Kwa mfano, anaamriwa amlipue Fikirini lakini hatekelezi amri hiyo. Aidha, anamsihi dada yake asimuue Fikirini kwa kisu. Hii ndiyo sababu alipaza sauti, kumkataza Fiona kumdhuru Fikirini. "La, Fiona!" ... we utazua zani hapa, mwache aende" (Uk.29)
b) *Mwenye chuki kwa Waafrika weusi*. Ana mwelekeo sawa na wa dada yake kwa vile hawapendi Waafrika weusi. Hapendi huhusishwa na Waafrika weusi. Kwa mfano, hataki kuitwa ndugu. Kwa mfano, anamfokea Fikirini kuwa: "Fala kabisa wewe, twawezaje sisi kuwa ndugu wa tumbiri kama nyie?" (Uk.27)
c) *Ni dhalimu*. Anamlazimisha Fikirini kuvua nguo na kumtisha kumpiga risasi.Baadaye anaamua kumrusha Fikirini nje huku yuko uchi.

Umuhimu wa Bob

Kama ilivyo na Fiona, Bob ametumiwa kudhihirisha jinsi Wamerekani weusi wana chuki dhidi ya Waafrika.

Wahusika wengine ambao wametajwa kwenye hadithi ni kama vile:

(i) Daniel arap Moi. Yeye ni mzalendo na mwenye tahadhari kutokana na maonyo yake aliyotoa dhidi ya wazungu. Yeye pia ni mwenye busara.

(ii) Dereva wa basi. Yeye ni mwenye ubaguzi kutokana na tendo lake la kumwacha Fikirini.

(iii) Mama Mzungu. Yeye ni mchochezi, mfitini, mwenye chuki na ubaguzi kutokana na tendo lake la kuwaita polisi baada ya kumwona Fikirini hajafunga zipu.

(iv) Mhadhiri Mzungu. Yeye ni mbaguzi, katili na mwenye mapendeleo kutokana na tabia yake ya kuwatuza wanafunzi alama kwa misingi ya rangi yao.

(v) Wanafunzi wa chuo kikuu. Wao ni dhalimu, wwenye chuki dhidi ya waafrika na wapyaro kutokana na maswali wanayomwuliza Fikirini.

Hawa pia ni wahusika wadogo lakini wamesaidia kuendeleza maudhui katika hadithi.

Mbinu Za Lugha

1. Methali

Methali zilizotumiwa katika uwasilishaji wa hadithi hii ni kama:

a) Methali ya “nyumbani ni nyumbani ingawa pangoni. (Uk.23)” imewasilisha kumbukumbu za Fikirini kuhusu kwao. Hili linatokea hasa inapobainika kuwa ughaibuni kuna dhiki chungu nzima dhidi ya Waafrika.

b) Methali ya “Baharia wa Pemba kufa maji mazoea (Uk.24)” imetumiwa ili Fikirini aweze kujifariji kwa hali ambayo ameizoea.

c) Methali ya “Simba akikosa nyama hula nyasi (Uk.24)” imetumiwa kushihirisha kuwa chakula ambacho hakijazoelewa kimeliwa kutokana na ukosefu wa uchaguzi mwingine.

d) Methali ya “Siku ya nyani kufa na ambapo miti yote huteleza (Uk.29)” imetumiwa kuwasilisha hali ya hatari iliyomkumba Fikirini mikononi mwa Fiona na Bob.

Jambo la msingi ni kwamba methali hizi zimechangia katika uwasilishaji wa ujumbe wa msanii kwa njia ya mkato, tena inayonitia.

2. Utohozi

Huu ni uswahilishaji wa maneno ya lugha nyingine. Maneno yaliyotumika kwa mwendelezo wa Kiswahili ni kama vile:

a) Soksi (Uk.22) (socks)

b) Blanketi (Uk.22) (blanket)

c) Glovu (Uk.22) (glove)

d) Zipu (Uk.25) (Zip)

e) Faini (Uk.25) (fine)
f) Dola (Uk.25) (dollar)
g) Jaji (Uk.25) (judge)
h) Pochi (Uk.30) (pouch)
i) Polisi- Police
j) Dereva- Driver

3. Kuchanganya Ndimi

Mwandishi amechanganya matumishi ya lugha ya Kiswahili na yale ya kiingereza na hata ya Kiafrika kama mifano ifuatayo inavyodhihirisha.

a) Waragi (Uk. 22) aina ya kileo kipatikanacho nchini Uganda).
b) Someone called to say you are exposing yourself? (Uk.24)
c) Do you speak English (Uk.24)
d) Mlenda (Uk.24). Aina ya mboga, maarufu kule magharibi mwa Kenya.
e) How are your doing? (Uk.25)
f) Am cool (Uk.25)
g) You guys are our brothers (Uk.26)
h) Do you want to have a good time? (UK.26)
i) Bob! Bob! Come here! (Uk.27)
j) Don't bring that kind of nonsense, you know what I mean? (Uk.27)
k) Come fast! This dude wants to rape me.
l) Drop that bag! (Uk.27)
m) I say, remove your cloths or else....
n) Out! (29)

Mifano hii inadhihirisha tamaduni tofauti zilizo mwadhiri Fikirini; utamaduni wa kwao Afrika mashariki ambao anaukosa. Kisha wahusika Wamarekani ambao huzungumza kiingereza.

Waamerika weusi wana lafudhi yao inayowatambulisha.

4. Semi

Mwandishi pia ametumia kauli maalum zinazotoa maana isiyo wazi, kwa mfano.

a) Moyo mweusi (Uk.22). Fikirini anamchulia dereva kuwa na moyo mweusi kwa vile nampuuza. Hapa panadhihirika kejeli.
b) Majuu (Uk.22). Nchi za kigeni hasa Ulaya na Marekani wanakokwenda Waafrika elimu ya juu na maisha ya kifahari.
c) Baba wa taifa (Uk.22). Kiongozi wa taifa.
d) Huwaambia kimasomaso (Uk.23). Fikirini huwabainisha kinagaubaga kuwa amechoshwa na sharau zao.
e) Funga duka (Uk.24). Huu ni msimu unaomtahadharisha mtu kurekebisha jambo linalomtia aibu kama vile kuonyesha sehemu nyeti.

f) Alipopigwa pingu mikononi (Uk.24)
g) Kutoswa ndani ya gari (Uk.24)
h) Alikuwa pandikizi la jimama limekula likashiba. (Uk.25)
i) Alisema kwa roho ya kisebusebu na kijoyo kipopo. (Uk.26)
j) Maji yamezidi unga. (Uk.26)
k) Nimkate mrija. (Uk.29)
l) Maji yamezidi unga
m) Akasalimu amri

5. Tashibihi

Kauli zinazoonyesha ulinganisho wa moja kwa moja ni kama vile:

a) Avae safu ya maguo na maguo ... na viatu vizito kama wanajeshi. (Uk.22)
b) Kupepesuka pepesu pepesu kama mlevi chakari (Uk.22)
c) Umehanikiza na kufunika kila kitu kama blanketi la unga uliofunika maji.
d) ...akitetemeka kama majani ya mgomba kwenye dhoruba (Uk.27)
e) Aliishi huku akilia machozi kama kitoto kidogo. (Uk.29)
f) Kukimbia kasi na tupu tupu kama mtu aliyepagawa pepo mabaya (Uk.29)
g) Zilikuwa zimeshika baridi la kuzizimua kama mwili wake ulivyozizimia (Uk.29)
h) Alijitosa nje tupu tupu kama alivyozaliwa. (Uk.29)

6. Maswali ya Balagha

a) Lo! Huyu ni mwenzangu, au sio? (Uk.25)
b) Nini kinawatoeni Afrika kuja huku kutusumbua hapa Marekani? (Uk. 27)
c) Mbona hambaki kwenu huko kwenye uchawi na ushirikina wenu? (Uk.27)
d) Unataka kumbaka dadangu kwa nini? (Uk.27)
e) Nani ndugu yako? (Uk.29)

Maswali hayo ya balagha yamesaidia kujenga usemezano wa nafsi na usemezano wa mlengwa au walengwa.

Tabaini- Theluji ilikuwa kote, si madirisha, si mlangoni, si paani, si ukuta…….

Tanakali za sauti-Mlevi chakari, kunyapia nyapunyapu, pepesuka pepesupepesu

Mtindo Katika Uwasilishaji wa Hadithi

1. Viona Nyuma/Mbinu rejeshi

Mwandishi ameyasawiri matukio yaliyotokea katika mandhari mengine, kwa mfano:

a) Alikumbuka siku zake za fahari alipofuatia *waragi* kwenye kitongoji duni cha kibuye jijini Kampala, gongo kwenye vichochoro vya Ubungo, Dar es Salaam, na chang'aa kenye fondogoo la Mathare, Nairobi. (Uk.22)
b) Kauli ya Baba wa talifa la Kenya, rais Daniel arap Moi "msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi." (Uk.22)
c) Kama angekuwa kwao Afrika, mtu angefanya hisani ya kumwambia "Aisee funga duka" badala ya kumwitia polisi. (Uk.24)
d) Fikirini alipomuona mweusi mwenzake, alikumbuka dada zake kule nyumbani Afrika Mashariki (Uk.25)

Mbinu hii imesaidia katika kujenga dibaji ya kuelewa muktadha wa uchimuzi wa hadithi hii.

2. Kejeli

Mbinu hii imetumiwa kubainisha zaidi dharau waliyo nayo. Wazungu weusi dhidi ya Waafrika, kejeli zilizotumiwa ni kama vile:

a) Je, kule kwenu watu wanavaa nguo au wanatembea rabana? (Uk.23)
b) Mtu anaugua ukimwi, malaria, polio na utapiamlo huko Afrika? (Uk.23)
c) Ulivaa nguo mara ya kwanza ulipotua kwenye uwanja wa ndege hapa Marekamo? (Uk.23)
d) Ni ipi mji mkuu wa Afrika? (Uk.23)
e) Huu weusi wenu unaozidi kiza unatokana na kuangukiwa na lami au kupigwa na mionzi ya jua? (Uk.23)
f) Nasikia wasichana wenu wote mnawakeketa na kuwashona ili kuzuia ukware (Uk.23)
g) Je mnaishi mitini kama tumbiri?

3. Taswira

Mbinu hii inahusu picha inayoundwa katika fikira za msomaji baada ya kuzingatia kauli au kisa chochote kinachowasilishwa katika hadithi hii.

a) Dereva mweupe mwenye moyo mweusi. (Uk.22)
b) Kote weupe wa theluji umehanikiza na kufunika kila kitu (Uk.22)
c) ...Mara ya kwanza alipojikuta darasani yeye peke yake mweusi, kisiwa cheusi kwenye bahari ya weupe (Uk.23)
d) Kwa desturi Fikirini huvaa tabasamu na kuonyesha bashasha na kutikisa kichwa kwa moyo mkunjufu (Uk.25)
e) Siku ya kufa, kifo cha aibu na nguo amevuliwa (UK29). Hapa ni pale ambapo Fikirini alikuwa anahangaishwa na Bob akiwa na Fiona.
f) Alijitosa nje, tupu tupu kama amevuliwa. (Uk.29)

g) Damu nyeusi (anwani ya hadithi)
h) Tafakari Fikirini akitiwa mbaroni na polisi kwa kutofunga zipu.
i) Tafakari mandhari ya chumba cha akina Fiona kiivyokuwa kichafu na vitu kutapakaa.

4. Taashira

a) Theluji

Theluji iliyopatikana ughaibuni ni ishara ya ukosefu wa utu ambao umesakini kote Marekani; si miongoni mwa watu weupe tu bali hata wamarekani weusi.

b) Weusi na weupe
Anaporejea dereva, dhana ya weusi wa moyo wake inarejelea ukosefu wa utu. Katika miktadha mingine, rangi nyeusi pamoha na damu nyeusi dhidi ya Waafrika, mizizi kule marekani, weupe ni ishara ya ubaguzi.

5. Majazi- Jina Fikirini limetokana na abia ya mhusika huyu ya kuwaza kila wakati. Yeye hujipata katika hali mbaya kila wakati inayomlazimu kuwaza sana.

6. Kinaya- ni kinaya kuwa Bob na Fiona wanadhaliisha Fikirini na ilhali wao ni weusi kama yeye.

Ni kinaya kuwa mama mzungu na polisi wanamsumbua Fikirini eti kwa kukosa kufunga zipu. Wanafaa wamwonyeshe ukarimu na utu kwani yeye ni mgeni.

NDOA YA SAMANI

Omar Babu (Abu marjan)

Dhamira ya mtunzi

Mtunzi alidhamiria kubainisha athari ya vikwazo ambavyo huwekewa vijana wanaopendana wakati wanapotaka kufunga ndoa. Aidha, alitaka kuonyesha kuwa vijana kutoka matabaka mbalimbali huweza kusalitika kimapenzi lakini wazazi huweza kuvunja mahusiano hayo kutokana na vikwazo ambavyo huviweka. Hat hivyo, maswala ya uchumba na ndoa hayapaswi kuwekewa vizingiti vya kiuchumi na kiatabaka.

Maudhui

Maudhui makuu ni kama vile maswala ya ndoa, kazi na uchochole.

1. Ndoa

Kulingana na jamii inayosawiriwa vijana walipaswa kuwafahamisha wazazi wao kuhusu uamuzi huo. Hata hivyo, msimulizi (mchumba mtarajiwa) na Amali hawana uamuzi kuhusu uchumba wao.

Wazazi hasa wa msichana ndio wenye uwezo wa kutoa uamuzi wa mwisho. Kulingana na mtunzi ni kwamba, wazazi hawapaswi kuwawekea vijana wao vikwazo vya kiuchumi, kwa sababu, jambo hilo huweza kuleta kutoelewana kwa wapendanao. Kwa mfano, msimulizi anapopeleka posa yake mamake Amali anasema, "Amani hataki kuolewa ... tena, sijui kama utaweza mahari" (Uk. 87).

Mawazo kama hayo hayazingatii mwafaka wa asasi za ndoa. Hii ndiyo sababy ya mjomba wake msimulizi kuhimiza kuwa, "ndoa hufungwa mbinguni" (Uk.87). Maelezo yanayotolewa katika hadithi hii ni kwamba, tabaka linalojiweza huwa halitaki kuzingatia misingi ya asasi za ndoa ila kwa kuweka mbele suala la fedha machoni pao. Huo si utu.

Ni baada ya kutambua uwezo wa kiuchumi wa msimulizi ndipo posa hiyo inakubaliwa. Hata hivyo, jambo la msingi kwa wazazi ni kuhakikisha kuwa vijana wao wanapendana na kutoa ushauri utakaowasaidia katika kuiamrisha ndoa yao. Kwa mfano, msimulizi ni kijana ambaye ana mwelekeo mzuri katika maisha. Kwa sababu, amekuwa akijitahidi katika kazi aifanyayo na pia kusaidia familial yao. Kwa hivyo alikuwa mwenye maono mazuri kuhusu maisha na bila shaka angeweza kujenga ngome imara katika masuala ya ndoa. Kutokana na vizingiti vya wazazi wa Amali, binti yao hapati mchumba. Naye msimulizi ametatitizika mno katika mfumo mzima wa ndoa.

2. Kazi/Ajira/Bidii

Kulingana na mtunzi, kazi ni muhimu. Kwa mfano msimulizi ambaye ni kijana amekuwa akijitumikisha katika kazi. Kwa hivyo, hakulaza damu. Ingawa alitokana na aila ya wachochole, yeye aliweza kuimarisha hali yake ya kimaisha kutokana na juhudi za kibinafsi kama invyoelezwa kuwa, "sikuwa mzembe. Nilifanya kila sampuli ya kazi za vibarua. Nilijenga kijumba cha msonge kilichokandikwa kwa udongo" (Uk. 86). Kwa sababu hiyo msimulizi aliweza kupata "mali ya kutosha" (Uk.86) kumlisha yeye mwenyewe na kuisaidia jamaa zake. Anakwenda Arabuni anapochapa kazi. Katika masuala ya kazi, ni vyemna kujitahidi kila wakati. Kadhalika, mtu anapofanya kazi anapaswa kujiwekea akiba ambayo itamsaidia katika maisha. Hii ndiyo sababu msimulizi alitundiza fedha na kuanzisha miradi pale kijijini kwao. Kutokana na juhudi hizo aliweza kununua matatu na kuwajengea wazazi wake "nyumba nzuri" (Uk.87). Kupitial kwa msimulizi mtunzi anafahamisha kuwa mtu ni kazi hat iwe ni ya nama gani. Katika muktadha huo, mtu huweza kuwa mlalahoi na baadaye kuwa mlalaheri. Shime ni kufanya kazi, la sivyo mtu huweza kupata dhiki na kudharauliwa katika jamii.

3. Dhiki za Uchochole/Umasikini

Uchochole una dhiki zake. Katika kijiji cha msimulizi kuna watu ambao hawakujiweza katika maisha, kama inavyoelezwa kuwa, "Kijiji kwetu tulikuwa masikino waliokuwa wakipigiwa mfano. Hakuna aliyekuwa na uwezo wa kumwauni mwenziwe" (Uk.86).

Watu ambao hawana hali nzuri ya kimaisha wamekuwa wakidharauliwa na wale wenye nacho. Hata wakati wa kuoa vijana hawakuruhusiwa kupata jiko katika familia zilizojiweza. Mawazo hayo husumbua akili za watu kama abainishavyo msimulizi anaposema ... mtule kama mimi haingekuwa rahisi kujishindia mke dhamana na huo ulitima wangu (Uk.86).

Kwa hivyo, watu hao huvunjiwa heshima kwamba, “nilipata tetesei mitaani kwamba mama Zena alikataa posa yangu kwa kuwa sikuwa na uwezo wa kujilisha mwenyewe seuzw binti yake” (Uk.87). mtunzi anapiga vita mielekeo hiyo ambayo haijajengwa kwenye misingi ya utu. Kwamba, mtu anayetokana na jamii ya kimasikini pia ni mtu na heshima zake.

Kilicho muhimu ni kutambua uwezo na utu wa mtu badala ya kujishughulisha katika maswala ya utabaka.

Suluhisho linalotolewa na mtunzi ni kwamba, mtu huweza kujinasua kutoka kwa hali ya umasikini wa kutupwa jana, sasa nilikuwa nikisowera katika utajiri.” Kadhalika, utajiri haupaswi kuwa kigezo cha kuwadharau watu wasiojiweza katika jamii. Kwa mfano, msimulizi alipokuwa mwenye hali nzuri ya kifedha aliwasaidia sana jamaa na rafikize katika kupata ajira. Huo hi uungwana uliolekezwa kwa utu.

4. Uhusiano Mwema Katika Jamii

Uhusiano mwema katika jamii hujengwa kwa kuzingatia utu na kujaliana. Kwa mfano, msimulizi alipokuwa anataka kupata jiko mjomba wake alihusishwa katika kupeleka posa kwa akina Amali.

Hata wakati ambapo msimulizi kwa kumwambia kuwa, “Usife moyo mwanangu (Uk.87). Katika kazi za vibarua alizizifanya, zilimsaidia kujenga uhusiano mzuri kwa “kusaidia jamaa (Uk.86) zake.” Kadhalika, alipopata bahati ya kuenda Arabuni na kufanikiwa kimaisha hakujawa kiburi bali aliwasaidia zaidi jamaa na rafikize kuanzisha miradi ambayo itatoa mwanya wa kuwapa ajira wale waliokuwa hawana kazi kijijini kwao.

Msimulizi alikuwa mtu wa kupigiwa mfano, katika masuala ya kujenga uhusiano mzuri katika jamii. Kwa mfano, kila alipopate likizo aliweza kuwatembelea wazazi wake huko kijinini kwa malengo ya kuwasaidia na kujuliana hali.

Hata wakati wa harakati za kujipatia jiko, aliamua kudumisha uhusiano huo kwa kuenda kwa wazasi wa Amali. Wazee hao walikuwa ni majirani zao.

Uhusiano huo unaosawiriwa ulikuwa ni tofauti na mielekeo ya wazazi wa Amali ambao walitaka uhusiano na wale waliojiweza tu.

Maudhui zaidi ambayo yanaweza kujadiliwa darasani ni kama:

5. **Suala la mapenzi**

   Msimulizi alimpenda sana amali na ndio sababu yake ya kurudi kwa akina Amali kwa mara ya pili hata baada ya kuponzwa kwa mara ya kwanza. Aliweza kumnunulia amali vitu vyote ambavyo alitaka kama vilemajora ya vitambaa na vitu vya dhahabu.
6. **Utabaka** . Msimulizi alikataliwa kwa mara ya kwanza kwa sababu alitoka katika familia maskini. Wakati huu wazazi wa amali walikuwa na pesa na ndiposa hawakutakamtoto wao kuolewana mtu maskini.
7. **Uchu au kiu ya mali**/ Tamaa

   Abu aliweza kukataliwa hapo awali kwa sababu alikuwa maskini. Hata hivyo, baada ya mamake Amali kuona Abu ashapata mali, alikula njama na msichana wake na wakaandaa orodha ya vitu vya thamani ambavyo Abu alikuwa anunue kabla ya posa yake kukubaliwa. Hii ni pamoja na: vitu vya dhahabu kama vile mikufu, pete, herini na samani. Pia jamaa za Amali walitaka vitu kama vile mkoba wa nguo, majora ya vitambaa na doti ya kanga.

   Mtu mmoja alidai apewe kitu kidogo ili aweze kumruhusu Abu kuingi ukumbini ambako arusi ingefanyika.
8. **Malezi.**

   Amali amepata malezi yasiyofaa kwa kufunzwa na mamake kudhamini mali badala ya utu. Abu naye kwa upande wake amefunzwa kudhamini watu wa jamaa, kufanya bidii maishani na kushirikiana na watu.
9. **Kisasi.**

Msimulizimaliamua kuvunja ndoa kati yake na Amali baada ya kukumbuka aliyotendewa na kugundua kuwa familia ya Amali ilikuwa na haja na mali yake na wala sio utu wake.

10. **Usaliti**

Msimulizi anaamua kuvunja arusi dakika ya mwisho, kinyume cha matarajio ya wengi waliofika kwenye sherehe. Wazazi wa Amali pia walikataa posa ya Abu kwa kisingizio cha umaskini wake.

Usawiri na ujenzi wa Wahusika

Mhusika mkuu ni msimulizi wa hadithi. Wahusika wadogo ni kama vile amali, mama Zena, na baba Amali, mzee Kadiri

Msimulizi au Abu

Jina ‘Abu’ aliloitwa na binadamu yake huenda liwe ni jina lake au alilitumia kwa maana ya ‘babu’. Ni mvulana ambaye alitokana na aila ya umasikini.

Sifa

a) Alikuwa ni *mwenye bidii* katika kazi anavyosema kuwa “hata hivyo sikuwa mzembe. Nilifanya kila sampuli ya kazi za vibarua” (Uk.86). alipokuwa barobaro, *alijitahidi* kuhakikisha kuwa amejisimamia katika maisha yake.
b) Ni mkarimu. Kutokana na ukarimu na utu wake aliweza kuwasaidia wazazi wa jamaa zake. Hata aliponafasika alipoenda Arabuni katu hakuwasahau watu waliohusiana naye pale kijijini.
c) Ni mtu ambaye ana *mwelekeo mzuri* katika maisha. Alikuwa akijitahidi katika shughuli zake za kikazi na alipoona kuwa anahitaji jiko aliamua kupeleka posa kwa wazazi wake Amali. Hii inaonyesha kuwa alikaliwa kutokana na umaskikini wao. Alipokuwa akifanya kazi za vibarua na hata kupata ajira huko Arabuni alikuwa akihifadhi akiba ili imsaidie katika maisha ya baadaye. Hii pia inaonyesha kuwa alikuwa mwenye *busara*. Kwa ambavyo alikuwa akijitahidi katika maisha, hakuona kikwazo cha kupeleka posa kwa wazazi wa Amali.
d) *Mwenye kuweka kumbukumbu*. Baada ya kukataliwa kwa posa yake hapo mwanzoni aliteseka mno kimawazo. Hili lilimfanya agure hadi uarabuni kutafuta ajira. Anakumbuka alivyo alivyokataliwa kwa kuwa maskini.
e) *Ana msimamo dhabiti*. Kutokana na msimamo wake dhabiti hakukata tama kuhusu mambo ya msingi kama vile kutofanya kazi. Alichukulia kuwa maji yakishamwagika hayazoleki na maisha sharti yakabiliwe. Alipata kichochea cha kuzidisha shime katika shughuli zake za kuimarisha kipato. Kutokana na msimamo wake hakutaka kumuoa Amali. Hii ni kutokana na msimamo hasi wa wazazi wa Amali ambao waliuona utu kwa jicho la fedha. Tatizo hapa ni kwamba, iwapo wazazi wa Amali ndio walikuwa kikwazo, je Amali si alikuwa akimpenda kwa dhati yake!

f) *Mwenye kulipiza kisasi*. Aidha, ni mtu ambaye hakuweza kusahau mabaya aliyotendewa hapo mwanzoni kwa hivyo, alikuwa na kisasi kilichomtawala. Hii ndiyo sababu ya kujitahidi zaidi huko Arubaini ili awe na nguvu za kutuliza kilio chake. Hakujali atharo ambayo aingewapata wazazi wa Amali. Kwake utu ndio muhimu zaidi kuliko fedha.

Umuhimu wa msimulizi

(i) Amewakilisha vijana maskini kuonyesha matatizo wanayokumbana nayo katika jamii inayoabudu mali.

(ii) Mwandishi ametumia kuwapa maskini moyo baada ya kufanya kazi kwa bidii, mtu hupata chake na jamii ikaanza ‘kumthamini’.

(iii) Kupitia kwake, mwandishi anapiga vita kuthamini mali kutoka mapenzi katika ndoa.

Amali

Alikuwa binti ya mama Zena na Mzee Kadiri

Sifa

a) *Ni mtiifu*. Ni msichana ambaye aliwatii wazazi wake. Hiyo ni kwa sababu hata kama alimpenda mchumba wake, alishikilia uamuzi wa wazazi wake.
b) *Mtulivu.* Alikuwa msichana aliyetulia na hakutaka kujiingiza katika vitendo ambavyo vingemvunjia utu wake. Kwa mfano, baadhi ya watu waliomfahamy walisema kuwa, "mwone mtoto amejihifadhi, katulia kwao wala si kiguu na njia (Uk.87). Ingawa alikuwa mrembo, haukutia kiburi kwani, "alikuwa haachi ushungi. Alikuwa pia akivaa mavazi sitare" (Uk.87). Kadhalika, alikuwa mwenye heshima, kwa sababu alipoamkuliwa na mchumba wake alijibu, "Waalaikum salaam" (Uk.88).
c) *Hakuwa mdadisi*. Hakuweza kumuuliza mchumba huyo iwapo alikuwa anampenda, lakini amezubaa na kuuliza "mbona" (Uk.89).

d) *Mwenye tamaa nyingi*. Hadhihirishi msimamo wake moja kwa moja. Isitoshe, alimpelekea mchumba wake orodha ndefu ya vitu ambavyo vilipaswa kununuliwa huko Arabuni. Kama angekuwa mtu ambaye alitaka kuimarisha zaidi uhusiano wao angemweleza mwenziwe kuhusu mipando hiyo. Katika muktadha huo, mtunzi hapendi mwelekeo uliochukkuliwa na Amali.

Umuhimu wa Amali

j) Kielelezo cha vijana wanaofuata ushairi wa wazazi wao hata wakati unapoelekea kupotoka. Amekaa sana bila kuolewa kwa sababu ya msimamo wa wazazi wake. Aidha anaachwa na Bwana Arusi siku ya arusi yao. Aidha Amali andhihirisha nafasi ya mwanamke katika jamii ambapo hanaa usemi hata katika maswala yanayomhusu yeye.

Mama Zena

Ni mama yake amali

Sifa

***Mwenye ubinafsi na tamaa*.** Alikuwa mwanamke ambaye alitaka fahari ulioelekwa ka ubinafsi. Yeye hutaka ayaelekeze maamuzi yote muhimu katika familia yao. Kwa mfano, Baba Zena alipoletewa posa ya binti yao alishauriana na mkewe, ambaye alitoa kauli za kukatisha tama kuwa, "Amali hataki kuolewa ... tena", sijui kama utaweza mahari" (Uk. 87). Mjombake pamoja na msimulizi walimuuliza Babake Amali, lakini mama Zena alijitia kimbelembele na kukabiliana na wageni hao. Kwa hivyo, si mtu wa kutumia busara katika kauli anazozitoa.

a) ***Alikuwa na uchu wa mali*** ya haraka kupitia kwa uchumba wa bintiye.

b) Pia alikuwa ni mwenye ***majivuno na majitwazo*****.** Posa hiyo ya bintiye ilikuwa siri lakini kutokana na majivuno yake aliweza kueneza umbea hata mtaani. Kwa mfano, msimulizi anasema kuwa, "Nilipata tetesi kwamba mama Zena alikataa posa yangu" (Uk.87). Swali hapa ni kwamba, kwa nini ni yeye ambaye "alikataa" na wala si wao waliokataa? Kwa hivyo, hakuwa mwenye busara kama alivyokuwa mumewe.

Umuhimu wa mama Zena

i)Ni kielelezo cha wazazi wanaotumia wana wao wa kike kama vitega uchumi na kuishia kuyapotosha maisha yao. Pia ametumiwa kama kielelezo cha uovu wa tama na athari ya malezi mabaya.

Mzee Kadiri

Ni mumewe mama Zena na babake Amali. Ni mwenye uwezo wa kadri pale kijijini pao.

Sifa

a) ***Ni mwenye busara na maarifa***. Kutokana na busara yake hakutaka kutoka maamuzi ya kibinafsi bali kwa kumshirikisha mkewe kwa kila jambo. Hata hivyo, mchango wake si mkubwa sana kwa vile mkomdo wa maamuzi huelekezwa na mkewe. Kwa mfano, alipoupokea ujumbe wa posa, ni mkewe anayejitokeza kukabiliana na wageni. Hakuingilia kati ili kutia ufafanuzi zaidi. Alikuwa mzee wa busara, lakini huzidiwa nguvu na mkewe ambaye alikuwa "mshika usukani" (Uk.88)
b) ***Mtulivu***. Aghalabu, hakutaka kujiingiza katika mabishano na mkewe. Kwa hivyo, alikuwa mnyamavy na yote yaliyoamuliwa kwake ni sawa.
c) ***Mwenye heshima na stara***. Ni mzee ambaye hataki aibu pale kwake. Kwa hivyo alitaka "bintiye kumwondokea nyumbani asiye kuaziriwa kwa kulelewa wajukuu nyumbani" (Uk.88). kwa ujumla ni mzee ambaye ni mwenye busara lakini huemewa na mkewe.

Umuhimu wa Mzee Kadiri

Ni kielelzo cha wazee ambao hawajishugulishi sana katika kufanya maamuzi kuhusu wana wao, jamnbo linalohadhiri mkomdo wa maisha ya wana hao.
Wahusika wengine wanaoweza kujadiliwa darasani ni kama vile:
i) Fahami
ii) Mjomba wake msimulizi
iii) Bwana aliyemkingama msimulizi

Mbinu za lugha

1. Tashibihi

a) Nilijiona kama kwamba nilikuwa peke yangu katika gari hilo (Uk.83).

b) Nilitaamali hali yangu nikajiona kama rais au kigogo Fulani ambaye alikuwa akisindikizwa
kwenda shughuli muhimu ya kitaifa. (Uk.83).

c) ...Kiwe kigumu kama almasi. (Uk.85).

d) Siku yenyewe naikumbuka kama kwamba ilikuwa jana. (Uk.86).

e) Uzuri wa Amali ulikuwa aula kama hizo pesa (Uk.86).

f) Nilikuwa kama mtu aliyeona unyasi baada ya kuumwa na nyoka. (Uk.87).

Tashibihi hizi zimesaidia katika kusisitiza zaidi ujumbe ambao umewasilishwa katika hadithi.

2. Methali

a) Atafutaye hachoki, akichoka keshapata (Uk.86(

b) Ndoa hufungwa mbinguni (Uk.87)

c) Mtu akiona unyasi baada ya kuumwa na nyoka ...(Uk.87)

Methali hizi zimetumiwa kujenga usaili na utafakari wa mawazo yanayowasilishwa.

3. Tashihisi

a) Nilisikia sauti Fulani ikinadi akilini ndani kwa ndani katika nafsi yangu (Uk.83).

b) Soga lilikuwa limeuma moto garini (Uk.83).

c) Akili yangu ilikuwa ikitalii na kuandama mkondo tofauti (Uk.83).

d) Sauti hiyo ilinizuia kushiriki kwenye mjadala wowote ... (UK.83).

e) Moyoni nilikuwa nikihangaishwa na kibarua kigumu kilichokuwa kikinisubiri (Uk.83).

f) Tulishuka magari yetu na tukakaribishwa na sauti za akina mama. (Uk.83).

g) Harufu ya manukato ilizidi kiasi cha kukera pua badala ya kunukia (Uk.85-86).

h) Sikumuoa mimi, bali ameolewa na mali yangu (Uk.89).

4. Misemo

a) Bahari ya luja (Uk.83).

b) Moyo wangu ulikuwa ukitweta (Uk.83).

c) Liwalo na liwe (Uk.83).

d) Akipiga kemi (Uk.83).

e) Sauti ya ninga (Uk.85).

f) Hapa huingii bila kuninyooshea mkono (Uk.85).

g) Kitu kidogo (Uk.85).

h) Nilipiga darubini (Uk.86).

i) Sina sinani (Uk.86).

j) Kupata jiko (Uk.86).
k) Nilipiga darubini (Uk.86).
l) Sikuvunjika moyo (Uk.87).
m) Sikuwaacha mkono (Uk.87)
n) Kiguu na njia (Uk.87).
o) Sikutaka kumvunja mama Zena (Uk.87).
p) Mshika usukani (Uk. 88).
q) Arusi ya ndovu kumla mwanawe (uk.88).

Misemo hiyo imetumiwa kama mbinu ya kusisitiza mawazo katika hadithi na kuipa lugha ya msimulizi utamu, kuifanya ivutie.

5. Chuku

a) Mkajiona kama rais au kigogo Fulani ambaye alikuwa akisindikizwa kwendea shughuli muhimu ya kitaifa (Uk.83)
b) Walinisubiri kwa hamu na ghamu ili kutetemesha ardhi kwa miteteo ya sauti zao zenye uchawi wa kike (Uk.85)
c) Mama kiongozi wa waimbaji alikuwa amenizingira kono lake la kushoto na kuendelea kuniburura (Uk.85).
d) Kijijini kwetu tulikuwa masikini wa kupigiwa mfano (Uk.86).
e) Nilifanya kila sampuli ya kazi za vibarua.

Chuki imetumika katika hadithi hii ili kudhihirisha uzito wa kitu au wazo Fulani linalowasilishwa.

Maswali ya Balagha/ Maswali butu

a) Hii ni siku yako eti! (Uk.83).
b) Yu wapi bwana arusi aje hapa tuhangaike naye! (Uk.85).
c) Mbona! (uk.89).
d) Mimi si yule waliyenikataa kabla sijenda Arabuni? (Uk.89).

Maswali ya balagha yametumiwa ili kuendeleza mawazo yanayowasilishwa kwa hivyo hadhira huweza kujitolea majibu kulingana na muktadha unaowasilishwa.

Mtindo katika uwasilishaji

1. **Mbinu Rejeshi**

Mbinu hii imetumiwa kueleza:

a) Maisha ya msimulizi au Abu kule kijijini kwao.

b) Kazi alizozifanya Abu kabla ya kupeleka posa kwa wazazi wake Amali.
c) Posa ilivyotakaliwa hapo mwanzo.

2. **Taswira**

a) Hadithi hii imesawiri mandhari ya nyumba aliyoingia msimulizi huko kwa akina Amali.
b) Safari ya kuenda kwenye sherehe ya arusi.
c) Umasikini wa kwao msimulizi.
d) Hali aliyokuwa nayo msimulizi tangu posa kukataliwa na wazazi wake Amali.
e) Sherehe za arusi.
f) Kukataa kumuoa Amali katika hatua ya mwisho.

Taswira zilizozingatiwa zinaifanya hadhira kuweza kuona na kuhisi yale yanayowasilishwa.

3. **Nyimbo**

Nyimbo zilizoimbiwa bwana arusi siku ya sherehe pale nyumbani kwao Amali. Nyimbo hizo zilikuwa mbili: za kumkaribisha na kumhongera.

4. **Utohozi**

a) Motokaa (Uk.83) motor car.
b) Sampuli (Uk.86) sample.
c) Sukari (Uk.86) sugar.
d) Pasipoti (Uk.87) passport)
e) Kampuni (Uk.87) company.
f) Suti (Uk.)suit.

GILASI YA MWISHO MAKABURINI

Said A. Mohamed

Dhamira ya Mtunzi

Mtunzi anadhihirisha namna ushirikina unayoathiri jamii. Imani hizo huwakosesha watu mwelekeo katika maisha. Kadhalika, hii ni karne ya ishirini na moja (Uk.34) ambapo watu hawana imani na ushirikina lakini bado baadhi ya watu hawajakubali mabadiliko hayo.

Kadhalika, mwandishi amedhihirisha jinsi watu a tabaka la juu, hasa vijana, wanavyoendeleza anasa na starehe katika hoteli za kifahari mijini.

Maudhui

Maudhui mbalimbali yanajitokeza katika hadithi hii. Baadhi ya maudhui hayo ni kama:

1. **Dhiki za Ushirikina Katika Jamii**

Ushirikina katika hadithi hii umewasilishwa kupitial kwa mhusika Msoi ambaye anaamini kuwa ndoto huashiria uhalisi Fulani katika maisha. Kwa mfano anasema kuwa: "Ndoto zilizomwambia kwamba pahala walipozoea kwenda yeye na marafiki zake kupitisha wikendi, si pahala pa wanadamu hai, ni pa wafu; na wafu wenyewe wakiwa mapumzikoni wamechoka kukerwa, na kwa hivyo, siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami" (Uk. 32.

Msoi anaamini kuwa ana uwezo wa kuota ndoto za kweli. Kila mara ana hofu ya kutaka kujihami na imani za ushirikin. Kwa mfano, Msoi anapofikiwa na matukio ya kawaida kama vile kujikwaa, kubanwa kidole pamoja na ngurumo za radi, huchukuliwa kuwa ni "kitu kinacholiza ndege mbaya" (Uk.33

. Baadhi ya watu kama Msoi wamekuwa wakiamini ufukukaji wa wafu; kwamba, mava, makaburini, mashetani, vizuu ndio wenye nguvu zaidi ya wale walio hai. Kulingana na mtunzi, mambo hayo ni ya kidhahania yasiyokuwa na uhalisi wowote katika maisha ya jamii.

Baadhi ya mambo ya kawaida hujengewa imani kama vile mapasuko wa radi kuchukuliwa kuwa ni "ishara mbaya" (Uk.34). Mawazo ya kishirikina huwa yamepitwa na wakati na baadhi ya watu hukemea jambo hilo kama wafanyavyo marafiki Msoi. Kadhalika, imewasilishwa kwamba baadhi ya ndoto huweza kutokea miongoni mwa watu. Kwa mfano, Msoi anatabiri kuwa katika Baa ya makaburini au Exotic Resort, kama anavyoipata, mabaya yatatokea. Jambo hili limechukuliwa kuwa ni uzushi lakini uhalisi huo ulishuhudiwa wakati ambapo, "kule mavani kundi la vizuu limejifufua kwa

mtindo wa Thriller wa Michael Jackson" (Uk.37). Vizuu hivyo vilizua ghasia pale hotelini.

2. **Anasa na Starehe za Mjini**

Baadhi ya watu na hasa vijana hupitisha wakati mwingi katika hawaa na starehe za kimji. Kwa mfano, katika Baa ya makaburini, vijaa hao hawaoni raha pasi na kufika huko. Kwa mfano, Msoi anapotoa rai kwamba hatahudhuria starehe hizo, Semkwa anamwendea nyumbani kwake na kumrai. Asha na Josefina tayari walikuwa huko.Wanashiriki katika sherehe na anasa tu. Haya ni maisha ambayo hayana mwelekeo iwapo wahusika hao wamekuwa wakilaza damu wakati wa kazi.

Katika hoteli hiyo iliyopakana na mavani, si makabwela wanaoenda huko bali ni, "pahala wanapozuru wangwana kama wao wenye vyao" (Uk.32).

Mtunzi anaeleza kuwa sehemu kama hizo za starehe za usiku, huenda si pahali pa usalama. Kwa sababu zogo huweza kuzuka na watu wakaumizana au kuumizwa. Kwa mfano, imeelezwa kuwa, "ukwenzi ukafauliwa na kwenzi, na kwenzi zikawa mjumuiko wa zogo na ghasia. Muziki ukasita," (Uk.37).

3. **Urafiki**

Katika hadithi hii, marafiki wamekuwa wakienda katika Baa ya makaburini kila jumamosi. Wanaoenda huko huwa ni watu wenye mahusiano na mielekeo inayofanana. Kwa mfano, Semkwa alipogundua kuwa mwenzake haonekani hotelini, anaamua kwenda kumtafuta kwake kama ilivyoelezwa kuwa: "Semkwa aliyechoka kumpigia simu na kumbembeleza rafiki yake ... aliona simu haitafaa kitu kwa ukaidi wa rafiki yake Msoi. Semkwa aliona bora aonane naye uso kwa macho" (Uk.33). Huu ni uhusiano wa kujuliana. Asha na Josephine walikuwa wakiwangojea rafiki zao kuwasili huko hotelini.

Kama marafiki walioshibana, wanatumbuizana na kuzungumza kama njia ya kuumarisha mahusiano yao.

Pia urafiki wao unadhihirika wakati Msoi na Asha wanapokunusuru na kujaribu kuwapigia simu Semkwa na Josefina. Hatimaye Semkwa anapigia simu msoi kumweleza walikuwa salama.

4. **Ujambazi**

Jambo hili hali. Hata hivyo, inatangazwa katika runinga kuwa, "Majambazi waliojifanya vizuu mavani kuibia Baa ya Makaburini kila kitu pamoja na wateja wao!" (Uk.39)

Hili limebainisha kuwa katika miji au majumba ya starehe kuna visanga au visa vya ujambazi ambavyo huweza kushuhudiwa.

Kulingana na mtunzi, visa vya ujambazi huwatia watu hofu na kusababisha fujo au ghasia kwa wapenda amani. Kwa mfano, ujambazi huo katika Baa ua makaburini ulisababisha mtafaruku; "meza anguka, viti vunjika. Gilasi anguka na sahani anguka. Ghafla bin vuu taa zikazima" (Uk.39).

Vile vile, Semkwa amelalamikia hali hiyo alimojikuta kuwa, “Tulibakia wachache pale, wakatukamata na kutuibia kila kitu, pesa, nguo, viatu hata na chupi” (Uk.39).

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

Katika uwasilishaji wa hadithi hii, wahusika mbalimbali wametumika kama vile: Msoi, Semkwa, Asha na Josefina.

1. **Msoi**

Huyu ni mhusika mkuu katika hadithi hii. Ni mtu ambaye **huamini zaidi itikadi za ushirikina.** Ndoto ambazo huziota huzichukulia kuashiria jambo ambalo huweza kutokea. Kwa hivyo, kila tendo linalomtukia lina fasiri. Kwa mfano, hataki kwenda kujumuika na wenzake katika hoteli ya makaburini kutokana na maono yake. Kwa uelekezi huo alipojikwaa, alipojibana kidole na radi ailipopasula alichukulia kuwa ni ishara mbaya. Jambo hilo halikuingia katika akili ya rafikiye, Semkwa.

a) **Msoi ni kigeugeu**. Hana msimamo dhabiti. Kwa mfano, imani yake ilimwelekeza kuwa huko hotelini kungetokea mabaya. Kwa hivyo, hakutaka kuenda kujumuika na wenzake. Baada ya kushawishiwa na Semkwa, anakubali kuandamana naye.

b) **Mwepesi wa hasira**. Anapofika huko hotelini na kufanyiwa stihizai au mzaha, hapendezwi na hilo bali anaonyesha wazi hali hiyo. Kwa mfano, anapoambiwa kuwa, “Anataka kutuvunjia raha zetu kwa ndoto zake za ajabu ajabu. Kwnai unatutabiria nini hasa Bwana ndoto?” (Uk.34). Msoi anatoa jibu la mkato kuwa, “mtaona”. “wote wanacheka isipokuwa Msoi.” (Uk.35)

c) Ni kijana ambaye **hupenda starehe na anasa** za kimji. Kwa mfano, yeye na wenzake kama vile Semkwa, Asha, na Josefina hawakosi kutokea katika Baa ya Makaburini. Kwa hivyo, hupoteza muda mwingi katika anasa hizo za vileo na mziki. Katika densi amekuwa akisifiwa katika midemko yake. Hii ndiyo sababu ya Asha kukasirishwa kwa vile alicheza. “kwa kumwondosha mwenzake njiani tu.” Alikuwa ameathiriwa na imani yake kuwa kuna maafa yatakayotokea mle, kiasi cha kushindwa kudemka.

d) Mwenye **kusadiki ushirikina**. Ana imani ya kutokea kwa mizuka na hili linamwathiri sana.

1. **Umuhimu wa Mhusika Msoi**

(i) Kupitia kwake mwandishi ameonyesha jinsi imani za kishirikina zinavyoweza kuyatawala maisha ya mtu hata kuathiri waayehusiana naye.

ii) Kutokana na mtazamo wake unaopinganga na wenzake, mwandishi amedhihirisha kuwa kila tukio linaweza kufasiriwa kwa namna tofauti kutegemea wahusika. Hilo lisiwe msingi wa kuwatenganisha marafiki.
iii) Ni kielezo cha usasa ulioathiriwa na imani za kikale za kishirikina.

2. **Semkwa**

Ni rafikiye Msoi.

a) ***Ni mpenda anasa***. Amekuwa akipenda sana starehe huko makaburini. Hii ndiyo sababu ya kumlaumu Msoi kuwa, "He! Saa mbili na nusu sasa hujajitayarisha tu!" (Uk.33)
b) ***Mwenye utangamano mwema*****.** Ni mtu ambaye hapendi kuwa kando na rafikiye, Msoi. Kwa mfano, mwenzake anaposema kuwa siku hiyo hajihisi kuenda katika starehe huko Baa ya makaburini, anamtafuta mwenzake hadi nyumbani kwake.
c) ***Ana uwezo wa kushawishi*****.** Kutokana na ulimi mzuri, Msoi anakubali kuandamana naye huko hotelini. Swali ni kwamba, kwa nini asingeenda mwenyewe akajivinjari na akina Asha na Josefina? Jibu ni kwamba, hakutaka kuwa mbali na Msoi.
d) ***Mpenda utani na mzaha*****.** Semkwa hupenda kushiriki mazungumzo na rafikize hasa kwa kuhusisha utani na mizaha. Katika Baa ya makaburini, Semkwa anazua mzaha na ucheshi kwa wenzake kuwa, "Na tunywe kwa urafiki wetu" (Uk.35). Asha naye akajibu kuwa, "Na tunywe kujikinga na vizuu na mashetani ya makaburini (Uk.35)
e) ***Yeye Amekengeuka***. Ingawa rafikiye anaamini ushirikiana, Semkwa hakubaliani na imani hizo. Anamwona Msoi kama mtu anayeishi katika enzi zilizopita, kwa kumwambia kuwa, "Katika maisha yetu ya kisasa ya sisi vijana, yanaendeshwa kisayansi yenye kubeba mantiki ya waziwazi" (Uk.35). ni mtu ambaye hapendi mambo ya kidhahania kama vile ushirikina.
f) ***Ni jasiri.*** Kule makaburini, mizuka ilipojitokeza watu wengi walitoroka kwa woga, lakini Semkwa hakuondoka. Ujasiri huo unamfanya kuporwa "pesa, nguo, viatu hata na chupi" (Uk.39). Huenda alitaka kushuhudia iwapo ni vizuu au ni majambazi kama ilivyoelezwa na Msoi.

Umuhimu wa mhusika Semkwa
i) Kielelezo cha vijana wa kisasa ambao wametawaliwa na anasa na starehe.
ii) Ni kielezo cha urafiki wa dhati. Hamhukumu rafikiye aliye na imani za kishirikina.
iii) Ana imani tofauti na za Msoi na mwandishi amewalinganisha ili kudhihirisha jinsi imani za kishirikina zinavyoweza kuathiri mhusika.

3. **Josefina**
a) Ni msichana ambaye ni***mnyamavu***na wala hapendi kushiriki maongezi sana.

b) Ni ***mwenye kuufumbata usasa/Amekengeuka***. Katika mawazo yake haamini nguvu na maono, anasema kuwa, “Msoi ni kama ziraili mpaka aitoe roho ya kiumbe” (Uk.35)

c) ***Anapenda starehe*****.** Kwa sababu ni miongoni mwa wale waliofika mapema huko Baa ya makaburini siku hiyo ya Jumamosi. Kadhalika, hakutaka sherehe za hapo hotelini zisinoge kwa utabiri wa Msoi.

4. **Asha**

Ni msichana na ana marafiki wenzake kama vile Msoi, Semkwa na Josefina.

a) ***Yeye hupenda starehe na anasa kama wenzake*****.** Kwa mfano, kila Jumamosi nyakati za jioni hakosi kupatikana katika maeneo ya Baa ya makaburini.

b) ***Ni mchangamfu/Mcheshi*** Anapenda kushiriki maongezi yenye mizoha na wenzake. Alipomwona Msoi amekaa kwenye makao ambayo si ya mazoea yake anamwambia, “Leo Msoi umebadilisha mkao?” (Uk.34).

c) ***Ni mwoga*****:** Hakuwa jasiri kwa vile yeye na Msoi pasi na kuwajali marafiki zao. Ghafla, vizuu au majambazi wanapotokea, anajawa woga kwa “ kupiga ukwenzi mkali” (Uk.37).

Umuhimu wa Josefina Na Asha

i) Kama ilivyo na wenzao Msoi na Semkwa, hawa ni vielelezo vya vijana wanaopenda anasa. Hii ni karne ya ishirini na moja na vijana wa kike pia wanashiriki ulevi na anasa nyinginezo.

ii) Mwandishi amewatumia kupinga zaidi imani za Msoi kupitia kwa maoni na mizaha yao inoyodhihaki msimamo wa msoi.

Mbinu za Lugha

1. **Tashibihi**

Mwandishi ametumia mbinu hii ya ulinganisho ili kusisitiza hali mbalimbali na kuvuta nathari ya wasomaji.

a) Kusimama kama kijiti (Uk.32). mwandishi anasisitiza jinsi Msoi huathiriwa na imani zake za kishirikina hadi malaika yake yakasimama kama ishara ya uoga.

b) Hisia hiyo kali ilikuwa imeamuka haraka kama hamuri lililojazwa hamira (Uk. 32). Mwandishi anaeleza jinsi hisia ya wasiwasi inavyomtokea Msoi.

c) Umebaki kulala kochini kama mgonjwa wa malaria (Uk.33). msekwa anatumia kauli hii kumshawishi Msoi waandamane katika starehe.

d) Utabakije juu ya kochi kama mgonjwa wa homa na leo ni Jumamosi/ (Uk.33)

e) Alijua ni kitu kama jabali lenye mshindo mkuu. (Uk.33)

f) Anatutisha sisi kama watoto wadogo, anatutisha kaka (Uk.35)

g) Bwana huyu ... kama zira ili, mpaka aitoe roho ya kiumbe (Uk.35). Hapa alikuwa anaashiria kuwa msimamo wa msoi ni dhabiti.

h) Na wewe, mpaka unigande mimi tu kama kupe?

i) Mtititiko wa jasho kama maji ya mlizamo wa mto (Uk.37)

j) Kung'ang'anaa kama masanamu (Uk.37 -38)

k) Nyuso nyeupe kama chokaa. (Uk 37)

2. **Tashihisi**

Vitu visivyo na uhai vimepewa uwezo wa kutenda kama vitu vyenye uhai ili kusisitiza hali na pia kumvutia msomaji.

a) Wafu wenyewe wakiwa mapumzikoni wamechoka kukerwa, na kwa hivyo siku yoyote ile wangefanya kitu kujihami (Uk.32). Kauli hii imehimiwa kulainisha hisia za kishirikina za Msoi.

b) Imani yako imekutawala (Uk.33). Imani imepewa uwezo wa kutawala, kauli inayosisitiza jinsi imani zake Msoi zinavyomwaathiri.

c) Hutaki kuiacha ijapokuwa unajua kwamba haina haki ya kuketi wala kusimama katika maisha yetu ya sasa (Uk.33). kauli hii ya Semkwa ina husisha imani ili kusisitiza kuwa imani za kishirikina hazifai.

d) Njiani, mbingu ghafla ilikasirika – ikafunga uso wake mweusi (Uk.34) mbingu kutandazwa na Mungu (Uk.34)

e) Mbingu ilifanya hivyo, mara moja tu. Tena bila ya kitiririsha hata tone moja la chozi (Uk.34).

f) Hata mwezi na nyota zimeshuka kidogo kuja kuimarisha furaha yetu leo (Uk.35).

g) Harufu za mafuta mazuri ghali na ya fahari, zilikuwa zimekazana kuzikalia juu harufu za vyakula (Uk.35).

h) Kinywaji kilipotua juu ya meza tu, jamaa walinyanyua gilasi zao (Uk.35).

i) Hali ya hewa ilikuwa nzuri, baada ya kutishwa kuharibiwa na ile radi ...(Uk.35)

j) Jimwili jeusi la usiku (Uk.35)

k) Hakucheza mpaka muziki ukamwingia damuni (Uk.37).

3. **Utohozi**

Maneno yaliyotoholewa kutoka kwa Kiingereza ni kama:

a) Wikendi (uk.32,33) (weekend)

b) Kochini (Uk.33) (coach)

c) Sofa (sofa-set)

d) Baa (Uk.33,36,37) (bar)
e) Switch (switch)
f) Kauntani (Uk.35) (counter)
g) Bendi (Uk.35) (band)
h) Muziki (Uk.36) (music)
i) Gilasi (Uk. 33,39) (glass)
j) Stimu (Uk.37) (steam)

4. **Taharuki**

Mtunzi amewasilisha na kuendeleza matukio kitaharuki. Mosi anwani yenyewe unazua taharuki kisha mpangilio wa vijisehemu katika hadithi umeongezea taharuki na kuongezea hamu ya msomaji.
Mifano ya taharuki inavyojitokexa katika hadithi hii ni pamoja na:

- Sehemu ya mwanzo ni dibaji kuhusu mhusika Msoi (Kur. 32 -33).
- Sehemu ya pili mhusika Semkwa, Asha na Josefina wameletwa katika hadithi (UK.33)
- Sehemu ya tatu inahusu safari ya Msoi pamoja na Semkwa kuenda Makaburini (Uk.34).
- Sehemu ya nne inahusu mazungumzo ya kiurafiki – Asha, Josefine, Msoi na Semkwa (Uk.36-37).

Mapangilio huo unawasilisha matukio ambayo humtia hamu msomaji kutoka kujijuvya zaidi kuhusu matukio yanayowasilishwa. Kadhalika, baadhi ya kauli zinazotumika huibua taharuki kwa hadhira. Kauli hizo zinachangia katika kujenga usaili kwa wasomaji: kwa mfano:

a) Kuhusu ndoto ambayo humpa Msoi “uwezo wa kutabiri mambo huku akijua kwamba ... yatabiriwayo huwa.” (Uk.32).
b) Semkwa aliona bora aonane naye (Msoi) uso kwa macho (Uk.33)
c) Umeona ukalie kiti kitakachokupa mandhari ya mava? (Uk.34)
d) Mazungumzo yanayohusu, “mwezi na nyota zimeshuka kidogo” (Uk.35).
e) Wewe sharti unigande mimi tu kama kuoe? (Uk.36)
f) Vizuu limejifufua kwa mtindo wa “Thriller” na Michael Jackson. (Uk.37).
g) Tulibaki wachache pale, wakatukamata na kutuibia kila kitu, pesa, nguo, viatu hata na chupi (Uk.39).

Kauli hizo zinasaidia katika kujenga hamu ya kutaka kuendelea kusoma zaidi ili kuelewa tokeo la kauli ya mwanzo. Matumizi ya taharuki kwa ufanisi yamechangia kuifanya hadithi hii kuvutia.

5. **Kejeli.**

Wandani wake msoi wamezoea kumkejeli kutokana na imani yake ya kishirikina wanayotofautiana nayo. Mf: Asha anasema, “na tunywe kujikinga na vizuu na mashetani ya makaburini”.
Josefina naye anasema, “Kwani unatutabiria nini hasa bwana ndoto?”
Josefina anaongezea kuwa “Anatutisha kaka, anatutisha sisi kama watoto wadogo”

6. **NdotoNjozi**

Ndoto zinazotumiwa katika hadithi zinawasilishwa kimasimulizi kwa hivyo zinakuwa kama chombo cha kuibulia ujumbe wa ushirikina unaowasilishwa. Kwa mfano, ndoto kuhusu yatakayojiri katika ukumbi wa starehe kule makaburini. Ndoto hiyo ilihusu vizuu, wafu au mashetani ya makaburini (Uk.35). Ndoto za Msoi zinajenga dira au msingi wa kuibulia na kuendeleza msuko wa visa katika hadithi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho.

7. **Taswira**

Taswira zinazoundwa katika hadithi hii imetokana na kauli msingi za kitamathali na maelezo yaliyotolewa. Kwa mfano:

Mifano:

a) Maelezo ya mwandishi pale Baa ya makaburini (Uk.32, 35).

b) Maelezo ya jinsi hali ya anga ilibadilika punde Msoi na Semkwa walipotoka kuelekea mahali pao pa starehe (Uk.34) matumizi ya tashihisi yanzidisha athari ya taswira inayojitokeza kwa wasomaji.

c) Maelezo jinsi ya wateja walivyojistarehesha kule kwenye baa(Uk.37)

d) Maelezo ya hali ya mtafaruko uliozuka baada ya wateja kuvamiwa na ‘vizuu’ (Uk.37-38)

Baadhi ya kauli na maelezo huifanya hadhira kuunda picha ya kimawazo ambapo huchangia katika kunga zilizotumiwa katika uwasilishaji wa ujumbe.

8. **Tashira/Ishara**

a) Kujikwaa kwa msoi,umweso wa radi, msoi kujibana kidole na bakuli ya maua kuvunjika alipojikwaa wanapoondoka nyumbani kwenda makaburini huenda kukaashiria balaa inayowasubiri. Vilevile tunaambiwa kuwa taa inawaka kwa huzuni.haya yote yalitabiri maovu fulaani.

9. **Kinaya**

Kulingana na ubashiri, vizuu ndivyo vilitarajiwa kuja pale makaburini lakini badala yake ni majambazi wanafika pale na kuwapora wateja.
Pia, ni ajabu sana watu kuondoka mjini na kwenda kujivinjari makaburini, baa ambayo wanaiita exotic. Inaaminika hapa ndipo kwenye utulivu lakini tunaona watu wakivamiwa.

Msoi pia hakutarajiwa kwenda huko makaburini na wenzake kwani alikuwa amekwisha bashiri balaa.

10. **Semi**

Moyo mzito-huzuni
Shingo upande- bila kupenda.
Uso kwa uso- kuonana/kukutana kwa karibu
Ng'oa nanga- kuondoka.
Kodoa macho- kuduwaa.
Kupitisha wikendi- kujistarehesha wakati a wikendi.

11. **Takiriri**

Ujumbe wa mtunzi umekolezwa zaidi kupitia kwa uradidi wa maelezo yanayotolewa kwa namna inayofanana au tofauti tofauti.
Uradidi huvuta hadhari ya msomaji, akachunguza kauli mahsusi kwa undani zaidi. Kwa mfano:

a) Neno ndoto limerudiwarudiwa katika hadithi
b) ...pahala pele pazuri panavutia. Pana ladha tamu ...'
c) Na tunywe kwa urafiti wetu; ...na tunywe kujikinga na vizuu na mashetani wa makaburini (Uk.36)
d) Raha, raha, rah auk. 37.

Maneno mbalimbali yamerudiwa ili kuukariri zaidi ujumbe unaowasilishwa. Uradidi wa kimuundo, kama utumikao katika 'wakala, wakanywa, wakamaliza.

TAZAMANA NA MAUTI

Said A. Mohamed

Dhamira ya Mtunzi

Dhamira ya mtunzi ni kuonya kuhusu tamaa ya kupata mali ambayo hawakutokea jasho. Kwa mfano, Lucy hakutaka kujitahidi katika masomo ingawa alikuwa na ndoto ya kuwa tajiri na kuishi maisha ya kifahari yenye anasa na starehe.Tamaa hiyo inamsababishia kifo.
Aidha mwandishi anataka kututahadharisha dhidi ya kuwa na tama ya mali kiasi cha kujisahau na kufuata mali kwa vyovyote vile.
Mwandishi pia anataka kuangazia dhana potovu iliyoko miongoni mwa vijana waafrika kuhusu maisha ya kifahari ya ughaibuni.

Maudhui

Maudhui makuu ni tama na ukengeushi.

1. Tamaa

- Katika hadithi hii mhusika Lucy amesawiriwa kama mtu aliyekuwa ametawaliwa na tamma ya maisha na anasa na starehe. Kutokana na mawazo hayo, Lucy amekuwa amejiundia na ndoto, “kwamba kiwiliwili chake kila siku huruka angani kuenda kutua na kuikagua Uingereza – hasa London” (Uk.91).
- Kadhalika, aliamini kuwa, akitaka kitu lazima akipate” (Uk.91). alipokuwa akiangazia wasomi katika nchi yake ya Firauni hakuona kuwa wameimarisha maisha yao zaidi ya kupata riziki. Lucy hakutaka riziki tu au maisha ya kawaida bali muluki (Uk.91).

- Lucy alitaka kujifanya mkimbizi, kupita na kutabasamu ili aweze kuwanasa Wazungu ambao wamefika nchini humo kustarehe ay kutalii.
- Kutokana na tama, Lucy alipoambiwa atapewa zawadi kutokana na msaada wake kwa mzee mzungu alitaka, “zawadi ya kuchukuliwa Uingereza au Ulaya yoyote” (Uk.94).
- Zaidi ya hayo, tamaa ya Lucy ilimsukuma katika kuishi na mzee mzungu ambaye hakuweza hat kutema mate. Mambo hayo hayakumsaidia “kumvua upweke” (Uk.95).
- Kadhalika, Lucy alikuwa na mawazo ya kutendea mfadhili wake unyama kama vile kumuua mzee huyo. Angeweza kutenda hilo kama “asingehofu sheria” (Uk.96).

- Lucy alipoahidiwa urithi wa mali ya mzee crusoe, alikuwa na mkururo wa mawazo ya jinsi “atalipindua jiji juu chini” (Uk.96) kutokana na utajiri atakaoupata.
- Kwa hivyo tamaa ya Lucy ndiyo inayomfanya kufikiria mali na kusahau mambo ya msingi katika maisha. Mawazo hayo ndiyo yaliyomsababishia kifo cha London. Kulingana na mtunzi, tamaa mbele mauti nyuma.
- Lucy aliweza hata kuanza kutafakari jinsi Crusoe angeaga dunia.Lucy alitafakari jinsi angefanya kazi kisirisiri ili aweze kujilimbikizia mali atakapokuwa kule uingereza. Iwapo angefanya hivyo, angekuwa akikiuka sheria.

2. Ukengeushi

Kukangeuka ni kubadili au kuukimbia uhalisia. Maudhui ya ukengeushi yamedhihirishwa kupitia kwa mhusika Lucy.

- Kwa mfano, hakuamini kuwa ndoto yake ya maisha mazuri yangeweza kupatikana katika nchi yake ya Firauni bali ingetimilika huko Ughaibuni – uingereza au Ulaya.
- Kutokana na athari za utamaduni, baadhi ya vijana kama vile Lucy, wamekuwa wakiangalia ustaarabu kwa jicho la kigeni. Kwa mfano, sinema ambazo zilikuwa zikisaidia kujenga mawazo hayo ni zile zilizohusu maisha ya wazungu ambao waliishi katika miji mikuu yenye majumba makubwa na starehe zisizokuwa na kifani. Kulingana na Lucy, wazungu waliishi maisha ya raha pasi na kufanya kazi.
- Katika muktadha huo, aliona kuwa akienda Ulaya, atapewa mshahara bila ya kufanya kazi (Uk.91). Hali hiyo ni kinyume na uhalisi wa mambo katika nchi yake. Kwa hivyok hakujitahidi katika masomo yake ambayo yangemjengea msingi wa “kupata riziki” (Uk.91).
- kulingana na mwandishi, kutoistahi nchi na kutozingatia utamaduni uliopo humfanya mtu kukosa mwelekeo wa maisha.
- Jambo linalosailiwa hapa ni kwamba, katika nchi ya Firauni hakuna lolote linalovutia mazuri katika maisha ya mwanajamii? Kuendeleza zaidi mambo ya kigeni ni kukengeuka na kuishia katika maanganizi.

Utepetevu

- Kwa mfano, lucy hakujali kujitahidi katika masomo. Kwa hivyo, anafeli katika mtihani wake wa kidato cha sita. Wenzake ambao walitia bidii katika masomo waliweza “kupata riziki zao” (Uk.91
- Lucy hakutaka kufanya kazi ambazo hazitamletea “muluki” (Uk.91). kwa hivyo, aliweza kujifedhehesha mitaani kujifanya kutabasamu” (Uk.92) na watu asiowafahamu. Lengo lake hasa lilikuwa ni kupata “tonge la ugali” (Uk.91) pasipo kufanya kazi.

- Ingawa Lucy alikuwa mwenye “sura ya kuvutia” (Uk.92), aliwaza jinsi mwili wake ungeweza kuwa “kiota cha ndege kwa mwanamume yeyote mwenye baridi” (Uk.92). huku ni kujidhalilisha pasipo sababu

3. **Hisani/Utu.** (Zingatia mzee Crusoe alivyomzawadia Lucy and Lucy alivyomsaidia Crusoe).

4. **Matatizo ya ujana**. (Zingatia namna Lucy alivyokuwa hataki kujitahidi masomoni huku akijiundia ndoto ya kuenda Ughaibuni).

5. **uozo/ Utovu wa maadili**

- Zingatia namna Lucy alivyoishi na mzee ambaye si wa rika lake.
- Crusoe kumchukua Lucy kama mke ilihali ni mzee.
- lucy kufikiria kwa vyovyote vile jinsi angepata nafasi ya kwenda ngambo. alifikiria hata namna angetumia njia za hila ili afaulu.
- lucy hakudhamini utu na anakiri kwamba kama hakuhofia sharia, basi angemwondoa crusoe ili afaidi urithi.
- lucy anajikosea heshima kiasi cha kutembea barabarani huku akitabasamu na wazungu ovyoovyo.

7.Unafiki-

- Lucy alikuwa akijidai kuwa anatenda wema ilhali alikuwa anajua anacholenga.
- Anawaza njia mbalimbali anazoweza kutumia kwa hila ili aweze kuenda London Mf Kutabasamu na wazungu, kujidai mgonjwa, .
- Vieivile, Lucy aliweza kujidai kuwa anamfanyia Crusoe hisani ili aweze kumshawishi Crusoe ili aweze kupata urithi.

8. Anasa

- Lucy alipenda sana maisha ya starehe kama vile kuishi London ambako alipaita peponi.
- **Lucy** alipenda sana kuhudhuria maonyesho ya sinema ambaazo ni za kimahaba.
- Crusoe pia alipenda kuhudhuria maonyesho ya aina hii. Aidha crusoe alimiliki magari kadha ya kifahari pamoja na wafanyakazi wengi.
- Jumba lake lilikuwa la kifahari pia pamoja na magari ambayo hakutumia.

Ujenzi na Usawiri wa Wahusika

Mhusika mkuu ni Lucy. Crusoe ni mhusika mdogo.

1. Lucy

Huyu ndiye mhusika mkuu katika hadithi hii. Ni msichan ambaye amesoma hadi kidato cha sita. Alikuwa hapendi kujitahidi katika masomo.

Sifa

a) ***Ni mzembe.*** Kutokana na uzembe wake anafeli katika mtihani. Hakutaka kutumia nguvu zake bali alitaka miujiza itendeke ili aweze kupata maisha hayo ya kifahari.

b) ***Ana tamaa.*** Alitaka maisha yake yawe ya kifahari na ya anasa.

Hii ndiyo sababu ya kujiundia ndoto ya kuenda Uingereza au Ulaya. Kwake pesa ndiyo nyenso ya kufanikisha maisha.

c) ***Ni katili.*** Kutokana na tamaa yake kubwa, alikuwa na mawazo ya kufanya chochote ilimradi ndoto yake imefikiwa. Hii ndiyo sababu ya kuwa na mawazo ya kuua. Kwa mfano, mwandishi anasema, "asingelihofu sheria angemlaza yeye mzee wa watu ili apate uhuru na utajiri wake" (Uk.96).

d) ***Ana utovu wa adabu:Hajiheshimu.*** Hakuona fedheha kujishalilisha mbele ya watu hasa kwa kujitia "kutabasamu" (Uk.92). kutokana na msukumo wa tamaa alikubali kuolewa na mzee Crusoe ambaye si wa rika lake.

e) ***Alikuwa mpenda starehe***. Kwa mfano, alikuwa akienda katika majumba ya sinema akiwa Firauni. Alipokuwa London, alipenda starehe na anasa za mji huo. Hii ndiyo sababu ya kusema kuwa, "atalipindua jiji juu chini na yeye atakuwa tayari kupinduliwa na jiji juuchini" (Uk.96). kutokana na tamaa kubwa ya starehe anakumbana na kifo.

f) ***Alikuwa na chembe ya utu***. Hilo limedhihirishwa wakati ambapo alimsaidia mzee Crusoe alipokuwa akipepesuka "aliruka kama mshale, akawahi kwa nukta ya dakika kabla ya kufika chini na kigonga kichwa chake sakafuni ..." (Uk.94)

5. ***Alikuwa mnafiki-*** Lucy alikuwa akijidai kuwa anatenda wema ilhali alikuwa anajua anacholenga Anawaza njia mbalimbali anazoweza kutumia kwa hila ili aweze kuenda London Mf Kutabasamu na wazung, kujidai mgonjwa, . Vilivile, Lucy aliweza kujidai kuwa anamfanyia Crusoe hisani ili aweze kumshawishi Crusoe ili aweze kupata urithi.

Umuhimu wa Mhusika Lucy

i) Ni kielelezo cha wahusika waliotawalia na uchu wa pesa na watafanya lolote lile mradi wapate pesa.

ii) Mwandishi anamtumia kubainisha ukweli wa methali ‘Tamaa mbele, mauti nyuma.
’

2. Crusoe

Alikuwa mzee wa kizungu kutoka Uingereza. Nchini Firauni alikuwa amekuja kwa ajili ya kutalii.

Sifa

a) Ni mzee ambaye ni ***mpenda starehe*** na anasa. Kwa mfano, alikuwa akienda kutazama sinema wakati Lucy alipokuwa akipanda ngazi kuelekea ukumbini.

b) ***Mwenye tahadhari***. Afya yake haikuwa nzuri lakini alikuwa mwenye hadhari kwani hakuwa akiacha “dawa mfukoni” (Uk.94).

c) Kadhalika. “alikuwa ***mwenye hisani***. Kwa sababu, baada ya kusaidiwa na Lucy, alimwambia kuwa, “naomba tukitoka sinema uningojee hapa nikupe zawadi kwa huruma zako” (Uk.94)

d) ***Mtovu wa maadili.*** Alipenda wasichana wadogo kama vile Lucy ambaye alimchukua kama mke. Kwa mfano, anamwambia Lucy kuwa, “sijapata kumuona mwanamke mwenye imani kama wewe” (Uk.96)

e) Ni mtu ambaye hupanga mambo yake ya baadaye kwa utaratibu. Kwa mfano, alitaka kumrithisha Lucy utajiri wake wote kwa wakili.

Umuhimu wa Crusoe

i)ni kielelezo cha watalii wapenda anasa wanaozuri nchi maskini na kuwachukua wasichana wadogo wa rika za mabinti zao.

ii) mwandishi amemtumia kutahadharisha kuwa sio vyote ving’aavyo huwa dhahabu. Hakuhisi uovu na dhamira potovu zake Lucy.

Mbinu za Lugha

1. Misemo

a) Mifuko yake iwe tupe (Uk.92).
b) Damu ya ujana imechemka (Uk.92).
c) Mbele yake ilimfuma mzee mmoja wa kizungu (Uk.94).
d) Jicho lake la ndani (Uk.94).
e) Kwa matao ya mapozi (Uk.94).
f) Wachomwe wachomwao (Uk.94).
g) Waseme wasemao (Uk.94).
h) Kwa nini ajitupe? (Uk.95).

i) Kumvua upweke (Uk.95).
j) Kulambishwa asali (Uk.96).
k) Ilimbidi awe macho (Uk.96).
l) Atalipindua jiji chini juu (Uk.96).

Misemo hiyo imetumiwa kukariri au kutilia nguvu ujumbe unaowasilishwa.

2. Tashibihi

a) ...ikimchagiza kama vile kiu ya mtu aliyekuwa akisafiri jangwani kwa miaka bila ya kuyagundua maji.
b) Wengi walitabasamu ...lakini wakishafanya hivyo humpita kama upepo wa kimbunga (Uk.92)
c) Joto la mwili wake lingeweza kuwa kama kiota cha ndege kwa mwanamume... (Uk.92).
d) Aliruke kama mshale (Uk.94).
e) Nguo na mavazi aliyonunuliwa juzijuzi tu ni kama aliyonunuliwa mwaka mzima. (Uk.95).

Katika muktadha wa hadithi kauli hizo zimetumiwa kwa malengo ya kufafanisha na kutulia nguvu hoja zinazowasilishwa.

3. Tashihisi

a) Anwani. ‘Tazamana na Mauti.”
b) Ile ndoto ... imevuka kujiopoa nje ya akili yake (Uk.91)
c) Picha zinazotembea kwa rangi tofauti ili kumwonyesha yeye utamu wa London (uk.91)
d) Huku akiacha tabasamu yake imemganda mzungu moyoni (Uk.92).
e) Jiko la chini na juu ghorofani linamwambia mwenzake asogee huku.
f) Wale watumishi ambao ndio wana uhai hawamsaidii katika kumvua upweke (Uk.95)
g) Msichana mbichi na tajiri anakuja ili jiji lijitajirishe kumpokea (Uk.96).
h) Gari la polisi liliingia ndani ya uwanja (Uk.96)

Kauli za tashihisi zimetumiwa ili kuhuisha ujumbe unaowasilishwa.

4. Maswali ya Balagha

a) Lakini tokea lini mtalii mifuko yake iwe tupu? (Uk.92)
b) Nani atakayekubali kwamba yeye ni mtalii, tena kutoka Uingereza (Uk.92).
c) Nani atakaye toka kuju Uingereza kumwoa yeye? (Uk.92).
d) ...Lakini, huyo mwanamume kutoka uingereza atakayekuja kumwoa yeye yuko wapi? (Uk.92)

e) Aaa, anajiuliza nini, na huku ameshasema kwamba yeye akitaka kitu mara nyingi huwa? (Uk.92)

f) Asaa... amsaidie tu, ya nini kujipa tamaa ya bure? (uk.94).

Maswali hiyo yametumiwa ili kumfanya msomaji ajitolee yeye mwenyewe majibu kulingana na muktadha wa ujumbe unaowasilishwa katika hadithi.

5. Kinaya

a) Joto la mwili wake linaweza kuwa kama kiota cha ndege kwa mwanamme yeyote mwenye baridi. Bado maneno au fikra hizo hazijamsaidia (Uk.92).

b) Kutokana na uzee, ubovu na ugonjwa wangu, najua nitakufa mimi mwanzo (Uk.96). hat hivyo, mzee huyo hakutangulia kufa bali ni Lucy ndiye aliyetangulia.

c) La, hapana ...akasema waziwazi kwamba yeye ni mwanamke mwenye bahati kabisa duniani. Mzee alikanusha kauli ya Lucy na kumwambia kwamba yeye mzee ndiye mwenye bahati kuliko wazee wenye umri wake wa kukutana na msichana mstahamilivu na mwenye huruma kama yeye (Uk.96). swali hapa ni, je ni nani mwenye bahati ni Lucy au Crusoe? Kadhalika, ni Lucy au Crusoe ambaye anatazama mauti?

6. Istiara

a) Umegeuka sungura aliyezikosa zabibu (Uk.91). Ulinganisho unaorejelea mtu ambaye anapokosa kitu, anakiharibia jina.

b) Kiu (Uk.91) kuwakilisha tamaa kubwa.

c) Hizi zote ni mafiga tu, haziishi kuporomoka (UK.91)

d) Kupenya kwenye chungio (Uk.91).

e) Kama si peponi huko ni wapi? (Uk.92).

f) Minyororo (Uk.91).

g) Jahanamu (Uk.92).

h) Kozi (Uk.95).

i) Kuolewa tu na mwanamume mzee, lakini ndiye mwaguzi wa ndoto yake. (UK.95).

j) Mapenzi ya kulambishwa asali moja kwa moja kutoka sega la asali (Uk.96).

Mbinu za Uwasilishaji

7. Mbinu Rejeshi

a) “Lucy ...juzi juzi tu amemaliza shule ya upili ya juu, yaani kidato cha sita lakini hakufaulu vizuri (Uk.91).

b) Lucy alipokuwa huko London na Crusoe wake anakumbuka kuwa, “kakwepa yote aliyoyasikia. Kalikwepa jina la ukimbizi” (Uk.95).

Matumizi ya mbinu rejeshi, yamesaidia katika kuelewa matukio ambayo yamesawiriwa na kuwasilishwa hapo baadaye katika hadithi hii.

8. Taharuki

a) Ndoto ambayo ilikuwa ikiotwa kwa miaka mingi na Lucy, “sasa imepevuka na kujiopoa nje ya akili yake (Uk.91).

b) Lucy alivyokuwa akisimama barabarani na kuwapa wazungu “tabasamu” (Uk.92). kwa nini Lucy alikuwa akitabasamu? Je, atafanikiwa kupata malengo yake?

c) “Naomba tukitoka sinema uningojee hapa hapa nikupe zawadi kwa huruma zako” (Uk.94). ni zawadi gani atakayopewa?

d) Kesho kutwa nataka twende kwa wakili nikuandikishe wewe utajiri wangu wote (Uk.95). utajiri huo utamfaa vipi Lucy?

e) ...lakini Lucy hakurudi (Uk.96)

Kauli hizo zilizotumiwa huweza kumfanya msomaji kutaka kuelezwa zaidi kuhusu hoja zinazowasilishwa katika hadithi. Zaidi ya mifano hiyo, mtunzi amejenga taharuki mwanzoni kwa kuitwa hadithi yake anwani ya “Tazamana na Mauti”. Kwa mfano, msomaji huweza kujiuliza ni nani anayetazamana na mauti? Ni Lucy au ni mzee Crusoe.

9. Taswira

a) Picha ya nchi ya Uingereza inawasilishwa kimaono kupitia kwa ndoto ya Lucy (uk. 94).

b) Maelezo yanayotolewa wakati Lucy anapomsaidia mzee Crusoe katika jingo la sinema (uk.94).

c) Mandhari ya utajiri wa mzee Crusoe unabainishwa wakati Lucy anapofika nyumbani kwake (Uk.95)

d) Shughuli ambazo Lucy alikuwa akimfanyia mzee Crusoe huko London (Uk.95).

Hii ni mbinu ambayo inakoleza mizungu ya uwasilishaji katika hadithi hii mbali na mbinu za lugha zilizotumiwa.

10. Utohozi

a) Muziki (Uk. 91) (music)

b) Madisko (Uk.91) (disco)

c) Sinema (Uk.92) (cinema)

d) Pauni (Uk.95) (pound)

e) Friji (Fridge)

f) Tiketi (Uk.94) (ticket)
g) Kozi (course)

Utohozi huo umetumiwa kuelezea namna utamaduni wa kigeni ulivyopenyeza katika maisha ya wenyeji.

11. Sadfa

Matukio yanayotokea kwa pamoja bila kupangwa wala kutarajiwa yamedhihirika.

a) Lucy kuwa karibu wakati Crusoe anavamiwa na ugonjwa. (Uk.92).

b) Sinema wanayoingia kuona inahusu mapenzi baina ya mwanamume mzungu na mwanamke mwafrika; ilhali anayotamani Lucy.

c) Lucy na Crusoe walikuwa wakitazama sinema ya mapenzi iliyokuwa ikihusu mapenzi baina ya mzungu na mwafrika na hatimaye walikuja kujipata katika hali hiyo.

12. Kinaya.

Ni kinaya kuwa Lucy alikufa kabla ya Crusoe ilhali Lucy alikuwa buheri wa afya na alitarajia Crusoe afe kwanza.

Lucy alikuwa na ari kubwa ya kuishi London alipochukulia kuwa peponi lakini tunamwona akikumbana na mauti yake huko.

Hapo awali , lucy alitamani aende London ambapo angekuwa analipwa pauni 40 lakini anapofika huko anapata kuwa ni pesa kidogo sana.

KIKAZA

Na Robert oduori

Mandhari ya Hadithi

Hadithi imejengwa katika muktadha ya jamii ambayo hushiriki kilimo na ufugaji. Jamii hii hutegemea mvua katika shughuli zao za zaraa au kilimo. Mvua isipokuwepo maisha ya wakulima huwa yanatatizika. Ingawa muktadha huo ni wa vijijini au mashambani, ujumbe ambao umewasilishwa umeangazia pia huru za kiafrika ambapo watawala huteuliwa ili hushika hatamu za kuiongoza jamii. Baadhi ya viongozi huwa wenye mwelekeo wa kibinafsi unaowafumba macho katika kubaini dhiki zinazowakumba wanajamii.

Maudhui

1. ULAGHAI

Hadithi hii imebainishwa namna utawala dhalimu unavyoidhikisha jamii ya Tekede. Baadhi ya viongozi kama vile Bwana Mtajika hutumia ulaghai wa maneno ili wachaguliwe kushika hatamu za uongozi lakini baadaye huvunja "masharti ya kikaza ' (Uk.45).

Wanajamii au watawaliwa wanalaumiwa kwa kukubali kuuficha ubaya wa viongozi wao kwa kuzingatia "hisani na huruma" (uk. 45). Hayo hufahamika. Kwa mfano, mkewe Bwana Mtajika alijichukulia kuwa yeye ndiye kiongozi. Jambo hilo limedhihirishwa kupitia kwa kauli ya Bi. Mtajika mwenyewe anaposema, " Hakuna kiongozi mwingine kunishinda mimi. " (uk.46). Matamshi hayo yaliwahuzunisha watu ambao walijiuliza, "Kwani sisi tulimchagua nani?" (uk.46)

Kadhalika ,viongozi kama hao hufanya mambo ya kisirisiri ili "ukweli" usitambuliwe. Kwa kushadidia zaidi wazo hilo anasema, " Nimetumiwa ujumbe wa siri kwamba niende nikashone kile kikaza." (uk.47).Uongozi mbaya katika jamii hasababisha dhiki ya umasikini katika jamii.

Kwa hakika inasemekana kuwa Bw. Mtajika angebadili uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo.

Hadithi pia imesimuliwa jinsi kobe alivyowahadaa ndege aliosafiri nao kwenda ugenini na akajipa jina la sisi sote ili aweze kufaidi. Hadithi hii ni mshabaha wa hali ya Bw. Mtajika alpopata uongozi.

2. Kuelekezana katika jamii /Uongozi

Uongozi katika eneo la Tekede ulikuwa unawahusisha wote;waume kwa wake. Bwana Mtajika baada ya kuchaguliwa na wanatekede anaasi kwa kufanya kinyume na matarajio yao.

Katika jamii ya Tekede, kuna wazee wa busara ambao wamekuwa wakitoa nasaha na uelekezaji wa jamii. Kwa mfano, Mzee Babu amekuwa akitegemewa mno na jamii kutokana na busara yake. Katika hali hiyo ya kuelekezana, Mzee Babu ametoa kauli kwamba, "mawingu mazito si ishara ya kuwa mvua itanyesha."(uk.41). Kwa hivyo, anaisihi jamii kupanua mawazo yao. Katika kuielekeza zaidi jamii, anatumia mshabaha wa hadithi ya kobe ili kubainisha funzo kutokana na kikaza. Hata hivyo, anafahamu kuwa hata washiriki pia huweza kutoa mchango katika busara inayowasilishwa.

Kwa mfano, Bwana Pima anatoa ufafanuzi wa kina kuhusu kikaza kwamba, " Bwana Mtajika alivunja masharti ya kikaza " (uk 45). Katika kuelekekezana huko ,jamii huweza kubadili matendo hasi. Kwa mfano, Bi. Cherehani alidhihirisha kuwa, "Kwa mara nyingine tena, Bwana Mtajika ametuaibisha. Hawezi kulinda kikaza ." (uk.47). Lengo lake halikuwa kumaibisha kiongozi wao bali kumfanya afahamu ubaya wa matendo yake.

Bi Cherehani pia anapewa nafasi ya kushiriki katika uongozi kwa kutwikwa jukumu la kukishona kikaza

Ukarimu na Ubinafsi

Suala la ukarimu linajitokeza kupitia kwa mhusika Mzee Babu. Kwa mfano, immelezwa kuwa, " kila aingiaye kwake Mzee Babu hatoki bila kunywa angalau kikombe cha maji. La sivyo, hatazungumza nawe, " (uk.42). Wanakijiji hawakukata Mzee Babu apate shida ya chakula. Kwa hivyo, "Baada ya mavuno, wanakijiji walizoea kutoa sehemu ya mavuno kwa mzee huyu"(uk.42). Hata hivyo,Mzee Babu hakutumia alichopewa vibaya bali akikihifadhi vizuri.

Wakati wa kiangazi au mavuno yanapokuwa haba, aliwapa tena wanakijiji ambao walikuwa na ukosefu wa chakula Mzee Babu alikuwa akipata wageni wengi kila kuchao. Kwa hivyo, "Kina mama waliowahi mapema kwa mzee walielekea moja kwa moja jikoni na kabla ya kikao kuanza, kulikuwa na chai, uji, mihogo… viazi.. na hata maji baridi katika mtungi" (uk.42).

Kinyume na moyo huo wa hisani,Bwana na Bi. Mtajika hawakuwa na watu " umasikini"(uk.47). Suala la ukarimu ni la msingi katika jamii ya Tekede ingawa baadhi walivunja mwafaka huo. Kwa mfano,Bwana Mtajika na mkewe walichukulia kwamba watu wanaoenda ikulu huwa wanataka chackula tu. Mawazo hayo yamedhiririshwa na Bi. Cherehani anaposema, "Leo kuna sherehe Ikuluni.Sote tuelekee kula tunakula na kuunywa." (uk. 47). Kutokana na dharau hilo, watu walikuwa na lao kwamba, Hata majumbani kwetu, sisi hula na kuunywa. Kama ni hivyo, nenda peke yako lakini usirudi." (uk.47).

BIDII/ KAZI.

- Shughuli muhimu katika kijiji cha Tekede ni kilimo na ufugaji. Katika jamii hiyo, watu huwa wanatayarisha mashamba yao mapema ili yawe tayari wakati wa majira ya mvua.

- Kutokana na jitihada zao, waliwez kupata mavuno si haba. Kwa mfano, " mahindi yaliwekwa ghalani. Mtama utatiwa maguniani…. Maharagwe vile vile yakawekwa humo" (uk.41). Kwa sababu hiyo, njaa ilikuwa ni jambo la sahau kama wasemavyo wanajamii kuwa, "Hata majumbani kwetu, sisi hula na kunywa (uk. 47). Kwa hivyo, katika kijiji hicho hakuna asiyefanya kazi.

- Hata katika ushonaji wa kikaza kila mmoja hushiriki. Kwa mfano, Bi. Cherehani anasema kuwa, "kila mnapompa jukumu la kushona kikaza, mimi hufanya kazi yangu kikamilifu….(uk.47). Katika jamii hiyo, ukupe au uzohali haukuwa na nafasi. Kila mtu alitegemea jasho lake.

Maudhui madogo ambayo yanaweza kuzingatiwa katika mijadala ya darasani ni kama vile:

3. **Ushirikiano katika jamiii**
   Wanatekede walikuwa watu wa kushirikiana. Hili linadhihirika kupitia:
   - Babu amekuwa katika mstari wa mbele kutoa ushauri kwa wanajamii.
   - Katika hadithi ya kobe, ndege walikuwa wameshirikiana kumchangia kobe manyoya ili aweze kupaa. Hii ni hali inayoshabihiana na jinsi wanatekede walivyoshirikiana kumchagua Bw. Mtajjika.
   - Pia ni bayana kuwa wanatekede kila wakati wamekuwa wakishirikiana kumshonea kiongozi wao kikaza.
   - Wakati mvua ilisusia kunyesha, wanatekede walikuja pamoja ili waweze kutafuta suluhu kwa matatizzo yao.

4. **UZALENDO**
   Wanatekede wamedhihirisha uzalendo kwa njia mbalimbali. Mf:
   - Wao huja pamoja wakati wa kumchagua kiongozii wao.
   - Bi. Cherehani anakubali kutwikwa mzigo wa kukishona kikaza cha kiongozi wao kule Tekede.
   - Bi.Cherehani aliamua kufichua siri ya Bw.Mtajika kwa kuwa alikuwa anawapenda wanatekede.

5. **Ukombozi /Mapinduzi**
   - Wanatekede wanaazimia kuleta mabadiliko kwa kumfurusha Bw. Mtajika kutoka uongozini.
   - Ingawa Bi. Cherehani amekuwa akishauriana na Bw. Mtajika kisirisiri, wakati huu ameamua kufichua siri yao.
   - Bi. Cherehani pia anaamua kushona kikaza kidogo kisichoweza kumtosha Bw. Mtajika kuashiria kuwa uongozi pia sharti ubadilike.
   - Hali ya anga pia imeanza kubadilika kutokana na tendo la Bw. Mtajika kuvunja sheria za kikaza.

6. **USALITI**
   - Kwa mfano, Bi. Cherehani alisema, "Kila mnaponipa jukumu la kushona kikaza, mimi hufanya kazi yangu kikamilifu lakini sithaminiwi." (uk.47).

- Vilevile, Bi. Cherehani anamsaliti Bw. Mtajika kwa kuelezea hadharani kuwa alikuwa ameitwa kisiri huko ikulu aende akakishone kikaza.
- Bw. Mtajika anajinufaisha anapoingia uongozini na ndiposi inasemekana kwamba ameanza kunenepa.
- Vilevile, tunamwona Bw. Mtajika akimwacha mkewe kuchukua hatamu za uongozi licha ya kuwa wanatekede walikuwa wamemchagua yeye na sio mkewe.
- Pia ni bayana kuwa baa la kiangazi na kutonyesha linaletwa na kauli kuwa Bw. Mtajika alikuwa amevunja masharti ya kikaza.

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

Hadithi hii ina wahusika kadhaa kama vile Mzee Babu, Bi.Cherehani, Bwana Pima, Bwana Machupa na Bwana na Bibi Mtajika.

1. Mzee Babu

Mzee Babu anapatikana mwanzoni mwa hadithi na anawashajiihsha kutegua kitendawili cha kukaza wahusika wengine kama vile wanakijiji ni wahusika wadogo.

Ni mzee wa makamo katika kijiji cha Tekede.

Ni mhusika mkuu katika hadithi hii.

a. **Ni mwenye kuheshimiwa**
.Katika kijiji hicho, alipendwa sana na kustahiwa na wanakijiji wengi hufika pale kwake kumjulia hali na kufanyiana dhihaka. Alijua jinsi ya kuingiliana na kila rika. Watu wazima pia hufika kwake ili kupata uelekezi wa maisha. Kutokana na heshima yake kijijini, huletewa vyakula na kusaidiwa na akina mama katika mapishi. Hii ndiyo sababu , " Asubuhi na mapema, kila njia ilielkea kwa mzee Babu " (uk 42).

b. **Alikuwa mwingi wa busara**
wanajamii wote waliistahi busara yake. Kwa hivyo, tatizo linapotokea jambo yeye ndiye anayeendewa ili kuelekeza katika kutoa suluhu au jibu. Alitumia mafumbo,vitendawili na hadithi. Hutua kijuujuu kauli bila kubainisha jibu. Washariki hubidi kushiriki kikamilifu ndipo jawabu lipatikane. Kwa mfano, yeye alifahamu kwa mafumbo sababu ya kutonyesha mvua, ndiposa anasema ," Lo! Haitanyesha." (uk.41.). Fumbo hilo linajenga msingi wa maelezo ya kikaza. Kwa hivyo, hatumii kauli zake ovyo ovyo bali hutarajia kujenga usaili na utafakari katika akili za watu. Hii inadhihirika kupita kwa dhana ya mawingu ,hadithi ya kobe na kikaza. Kila aliyesikia busara yake hutaka kurudi kwake.

c. **Mzee Babu ni mwenye tahathari.**
Kwa mfano, tunaambiwa kwamba maghala yake yamefurika kwa vyakula, "Naye hakuitumia akiba yake vibaya."(uk.42.).

d. **Ni mkarimu.**
Wakati wa kiangazi aliwasaidia wenzake kwa chakula. Pia alifahamu kuwa watu wengi huenda kwake asubuhina hakutaka wageni wake watoke kwake bila ya kutia kitu mdomoni. Kwa hivyo," ….kulikuwa na chai ,uji, mihogo…Viazi vya kiasili….. Kila mmoja alijifaa kwa namna yake." (uk 42).

e. **Ni mtambuzi**.
Alielewa asili ya dhiki katika jamii yake na ametoa mchango wa kutatulia tatizo hilo. Anatumia busara yake kueneza uzindushi miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano anajua fika athari za uchafuzi wa mazingira kama vile kunyesha kwa maji ambayo yana sumu.(uk.41).

Umuhimu wa Mzee Babu

a. Mwandishi anamtumia kama sauti ya kuwaonya na kuwaelekeza wanajamii.
b. Kupitia kwake thamani ya watu wenye busara katika jamii inabainika.
c. Ni kielelezo cha binadamu wasio na dosari kitabia na katika mielekeo yao.
d. Ametumiewa kujenga na kuyaendeleza maudhui ya utu.

2. Bwana Mtajika

Ni kiongozi mteule wa kijiji cha Tekede.

a. **Ni laghai.**
Kutokana na ulimi wake mtamu aliweza kuwafanya wanakijiji kumteua kuwa kiongozi wao. Kwa mfano, " alipoongea aliwavuta wengi" (uk.44). Alikuwa fundi katika mazungumzo lakini ndani yake alitumia ulaghai. Msimulizii anasema, " angeubadilisha uongo kuwa ukweli na ukweli kuwa uongo,"(uk.44) na kwamba kuchaguliwa kwake kuwa kiongozi kulikuwa kama ndoto.
Alimwita Bi. Cherehani kisiri ili aweze kukirekebisha kikaza kilichopasuka.
b. **Mwenye utepetevu**
Hakuwa makini katika wadhifa wake wa uongozi, kwa sababu alimruhusu mke wake kuwa mshauri wake kuhusu masuala ya uongozi. Kwa mfano, mkewe alipotamka hadharani,"Hakuna kiongozi mwingine kunishinda mimi, hakuonywa wala kurekebishwa.
c. **Mwenye maono na tafakuri**.
Alielekezwa na ndoto zake inasemekana kuwa, "Sifa yake kuu zaidi ilikuwa ni uweza wa kuota. Licha ya uwezo wake wa usemi, mambo kwake yalitendeka kindoto" (uk.44).
d. **Msaliti**.
Hafuati uhalisi wa mambo, "Alivunja masharti ya kikaza….." (uk.45)
e. **Ni muoga**.
Ni mtu ambaye huweza kutishika. Kwa sababu alipokuwa akidhihirishiwa ubaya na uongozi wake, " utulivu aliokuwa nao… ulianza kubadilika " (uk. 47). Zaidi ya hayo, alipoona kuwa wanatekede wakikaribia Ikulu, "Bwana Mtajika akaonekana kutokea mlango wa nyuma" (uk.48).
f. **Ni fisadi.**
Anatumia mali ya umma visivyo wakiwa na wenzake ndiposa…."wameongeza uzito wa miili."(uk.47).

Umuhimu wa Bwana Mtajika

1. Ni kielelezo cha uongozi dhalimu unaowakandamiza wale walioteua. Yeye na wenzake waafaidi ilhali umma unateseka.

2. Kielelezo cha viongozi ambao hawafuati uhalisia. Wanaishi katika ndoto na mambo yanakwenda kombo bila wao kufahamu.
3. Hatima ya uongozi wake ni onyo kwa viongozi laghai, hawawezi kudhulumu daima. Hufika siku ambayo wanaodhulumiwa hawawezi kuvumilia zaidi. Wanawafurusha na kuwaaibisha.

Bwana Pima

Ni mjumbe mmjowapi wa wajumbe waliomwendea Mzee Babu kwa ufafanuzi zaidi kuhusu kitendawili cha mawingu.

Ni miongoni mwa watu ambao wanaheshimiwa katika kijiji cha Tekede.

a. **Ana busara na ni mtambuzi wa mambo ambayo yanakiathiri kijiji chake**.
Kadhalika, hufahamu " namna ukweli unavyoweza kuumiza, kuchoma, kukandamiza na hata kunyonga." (uk.45). Kutokana na busara yake, yeye na Mzee Babu, "walizungumza wakasikizwa." (uk.46). Alifahamu kitendawili kukitegua hadi pale anaposhinikizwa na watu. Kwa mfano, Machupa alimtaka Bwana Pima kugonga ndipo badala ya kuwasimulia hadithi ndefu. Aghalabu, maelezo anayoyatoa huwa hayaeleweki kwa urahisi bali hadhira hutaka ujasiri wa ujumbe unaowasilishwa.
b. **Ana umakinifu**.
Huwaza kabla ya kutumia kauli Fulani. Hii ndiyo sababu ya kudhuhirishwa kuwa, " wangapi walio na ujasiri wa kunena ukweli, hasa unapohusu uongozi ? Bwana Pima atahesabiwa humo?
c. Ni **mwenye bidii**.
Yumo mstari wa mbele katika kushona kikaza. Hata hivyo, alifahamu kuwa kikaza ni cha ushirika.

Umuhimu wa Bwana Pima

a. Kielelezo cha watu wenye busara ambao ushaur jamii kwa kauli zao ambazo hawapati kuzitoa, wanazipima kwanza.
b. Kielelezo cha wanajamii ambao japo ni watu muhimu, hawajitanzazi.

1. Bi Cherehani

Ni mwanatekede, mwamke kwa jina halisi Bi. Chirenga (uk.47).

a. **Ni msanii**.
Ni mshona kikaza. Anashirikiana vilivyo na wanajamii wenzake kutekeleza shuguli hii muhimu.
b. **Ni mpole**.
Hana mazoea ya kujitokeza hadharani isipokuwa wakati hana budi kufanya vile (uk.47).
c. **Ni mwenye haya**
.Alijulikana kama mtu aliyejaa haya, asiye weza kuhutubia umma lakini aliwashangaza (uk.47).
d. **Ni mchochezi**
Kwa vile aliwachochea wenzake wachukue hatua kurekebisha mambo ambayo yalikuwa yameenda kombo kule kupasuliwa tena kwa kikasa na bwana Mtajika (uk.47).
e. **Ni mtambuzi**.
Anaelewa hali halisi inayoikumba jamii yake na chazo chake.

f. **Ni msiri**.
Habobokwi na maneno ovyo. Mwandishi anasema kuwa " Bi Cherehani ameshona mpaka leo na mdomo wake ameufunga" (uk 46) kuonyesha kuwa hakusema ovyo ovyo. Hakutoa siri kuwa wakati aliposishona kikaza, alikikaza kisibakishe nafasi yeyote.

g. **Mzalendo-**
Yeye amekuwa akishiriki katika kukishona kikaza. Vilevile, aliweza kueleza ukweli wa mambo jinsi alivyoitwa huko ikuluni kushona kikaza kilichopasuka.

h. **Ni msuluhishi.**
Kwa kukaza kikaza, anajua kuwa Bwana Mtajika atakirarua na hilo litafaa kumwondoa uongozini ili kusuluhisha matatizo yanayoikumba jamii hii, ambayo yamezuliwa na uongozi mbaya.

Umuhimu wa Bi Cherehani

1. Ni kielelezo cha viongozi ambao hawajitangazi, wanaotenda vitendo vikadhirika.
2. Mwandishi amemtumia kuonyesha dhima ya wanawake katika ujenzi wa jamii mpya. Wanaweza kushiriki viliivyo na kuwa viongozi wema.

Wahusika wengine ambao wanaweza kuzingatiwa ni kama vile:

B.Mtajika-Mkewe Bwana Mtajika,hana subira katika kauli zake.

Bwana Machupa –Ni mnafiki (ndumakuwili).

Mbinu za lugha

1. **Tashihisi**
Mbinu ya uhuishaji imetumiwa sana na mwandishi kufanya hadithi kuvutia kwa vile ujumbe unawasilishwa kwa njia ya mnato.
Mifano ya tashihisi.
   a. Mingurumo ya radi ilisikika kwa mbali ikija sauti nzito ya kutetemsha.(uk.41.)
   b. Uk. 45- Ukweli unaweza kuumiza, kuchoma, kunyonga…….
   c. Uk. 47 _ Usingizi ulimmeza bi mtajika.
   d. Uk 41- Wasiwasi ulitembea

2. **Ishara/Taashira**
   (a) Dhana ya kikaza imetumiwa kuashiria vitu mbalimbali
   (b) Mvua ni isahara ya ufanisi ambao ulipiga chenga wanatekede kwasababu ya uongozi mbaya wa Bwana Mtajika. Ufanisi na utovu wake pia una athari zake nzuri na pia mbaya kama inavyodhirishwa na wasiwasi wa wanajamii waliojawa na "hofu ya mvua kunyesha kwa wingi bila ya kiasi au kutonyesha kabisa" (Uk 41)

3. **Takriri**
Kuna kauli zilizorudiwarudiwa na mwandishi ili kusisitiza na kukita ujumbe akilini mwa msomaji. Neno 'kikaza' limerudiwa mara nyingi mno. Mfano:
   (a) Kikaza kikazidi
   (b) Mambo yana mambo yake (Uk 44), (Uk 48)

(c) Kikaza, kikaza ni cha ushirika (Uk 48)
(d) Mbuzi na kondoo kukimbia huku na huku. (Uk41)
(e) Siri ilikuwa siri (Uk 46)
(f) Ujumbe wa kisirisiri (Uk 47)

3. Jazanda

Jazanda imetumiwa kwa upana kwa kurejelea dhana ya kikaza.
Katika hali ya kawaida, kikaza ni kitu au zana ambayo hutumiwa kushikamanisha vitu viwili. Katika muktadha wa hadithi, kikaza ni:

(a) Chupi au suruali ya ndani inayosetiri uchi
(b) Jambo ambalo huleta ushirikiano na utangamano katika kudhibiti nguvu za watawala.
(c) Makubaliano au maafikiano (katiba) yanayobainisha na kudhibiti guvu za watawala.
(d) Wadhifa muhimu katika jamii kama vile uongozi n.k
(e) Uhusiano wa viongozi na watawaliwa
(f) Njia au mbinu za kuleta maendeleo katika jamii
(g) Kudhibiti hisia mbaya zinazokwaenda kunyume na uadhilifu sifa zingine anazostahili kuwa nazo kiongozi.

i. **Uzi na sindano** pia ni jazanda inayoashiria katiba au sheria inayowafungamanisha wanatekede. Aidha Bi Cherehani anaweza kuchukuliwa kuwa mlinda asasi ya sheria.
ii. **Tendo lolote baya linalinganishwa na wimbo** (Uk 45) kwa vile habari zake huenea na kuvuma.
iii. **'Utupu'** (Uk 45) kuwakilisha matendo yote yanayoleta aibu na kufanya jamii ikachekwa.
iv. '**Darubini' na 'dira'** (Uk 46) ni istiari ambazo zinaonyesha jinsi Machupa alivyojaribu kurtafari mambo yaliyoyasema wanakijiji ili amplelekee Bwana Mtajika uvumi.
v. **'Mawimbi'** (Uk 46) yametumia kurejelea ukosefu wa utulivu kwenye jamii.
vi. **'Kiti'** kimetumika kwa maana ya uongozi (Uk 47).
vii. **Mvua** inaweza kuashiria ufanisi.

4. Tashibihi

Mwandishi ametumia ulinganishi wa moja kwa moja, kwa mfano:

(a) Aliyaona kama ndoto (Uk 44)
(b) Machupa hutafuna na kupuliza kama panya (Uk 46)

5. Methali

(a) Nyani haoni kundule (Uk 44)
(b) Mapenzi ni kikohozi (Uk 45)
(c) Wamemla mbuzi mzima na mkia utawashinda? (Uk 46)
(d) Mdokezo wa methali katika 'kama ni nguruwe, walijua kuchagua' – ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona.

6. Utohozi

Kuna maneno kadha yalitolewa. Kwa mfano:

(a) Stooni (Uk 41) – (Store)
(b) Muziki (Uk 44) – (Music)
(c) Picha (Uk 45) – (Picture)
(d) Sunami- sunami.

7. **Tabaini-** Si salamu, si chochote
   Si njaa , si magonjwa wala chochote.
8. **Balagha-** Uk 45_ Mwaakumbuka miaka miwili iliyopita?
   Uk 44- nani asiyeona gamba la kobe lilivyo leo?
   Uk 44- Nyote mwafahamu hadithi ya kobe?
   Uk 45- w. pima atahesabiwa humo?
   Uk 47 Kwani sis tulimchagua nani?
9. **Misemo**
   (a) Walipiga picha nyuma (Uk 45): Walitafakari kuhusu mabo yaliyotendeka awali.
   (b) Walao jasho (Uk 45): Wanaojitegemea na kuzikimu hoja zao wenyewe.
   (c) Alitonesha kidonda (Uk 47) Aliwafanya kumbukuka udhalimu waliotendewa.

Mtindo katika Uwasilishaji

1. **Majazi**
   (a) Mzee Babu: Ni mzee wa busara na hekima
   (b) Bwana Pima: Alipima kauli kwa hadhari. Pia alishiriki katika kupima kikaza wakati wa ushonaji.
   (c) Bi. Cherehani: ndiye anayeshona kikaza kama cherehani ambacho ni kifaa cha kushonea.
   (d) Bwana Mtajika: Anayefahamika kwa kauli zake na hutambuliwa kama kiongozi wa Tekede. Kinaya kinadhihirika hapo kwa vile kauli na matendo yake hayakuelekea kuonyesha kustahiwa au ‘kutajika’ kwake.

2. **Ndoto/Njozi**
   Mifano ya ndoto zinazojitokeza ni kama zile za ndoto za Bwana Mtajika kuhusu:
   (a) Kuteuliwa kuwa kiongozi wa Tekede (Uk 44)
   (b) Mambo mazuri aliyoona kama ndoto (uk 44)
   (c) Bwana Mtajika hakuzingatia uhalisi wa mambo. Hakuelewa matatizo yaliyokumba jamii yake na mchango wake mkumbwa katika kuyazua. Ndoto zake zinaitumbukiza tedeke katika dhiki chungu nzima.
3. **Hadithi Ndani ya Hadithi**
   (a) Masimulizi na Kitendawili kinachohusu kikaza (Uk 42)
   (b) Hadithi ya kobe (Uk 44)

   Hadithi hizo zimechangia uwasilishaji wa ujumbe katika hadithi hii.

MAEKO

Mohamed Khelef Ghassany

Dhamira ya Mtunzi

Mtunzi alidhamiria kuelezea athari za ulevi katika ndoa. Mlevi huwa ni msumbufu katika jamii na huletea msukosuko ndoa. Mwandishi wa hadithi amebainisha kuwa Jamila alichangia kuendeleza tabia na mumewe kwa vile hakumkanya, alipokea kipigo kile bila kuteta. Anaamini mumewe anampenda. Baadhi ya watu ambao hujifanya ni marafiki. Kama vile Salim wanapogundua udhaifu huo huwanyemelea wanawake hao.

Ubaya wa ulevi umesawiriwa kupitia kwa mhusika, Hamduni ambaye amekuwa mwenye mazoea ya kulewa kupindukia, “matusi na kelele zaidi” (Uk.50). mwandishi anadhihirisha kuwa ulevi humfanya mtu kudharauliwa na kukosa kuwa na maelewano mema na wenzake. Mtu kama huyo hufanya maovu ambayo huyajutia anapolevuka. Hii ndiyo sababu Hamduni hajilaumu kuwa yeye ni “mja wa laana, mbwa miye, mi...mi...e” (uk.55).

Mwandishi alinuia kutegua kitendawili cha ndoa ambazo zimejaa dhuluma lakini wahusika hawazivunji.

Maudhui

Mwandishi amewasilisha maudhui kama vile ya ndoa, ujirani mwema na unafiki zilizojaa dhuluma.

1. **Ndoa**

katika hadithi hii mtunzi amesawiri matatizo ambayo huweza kuvunja ndoa za watu. Kwa mfano, ulevi ni chanzo cha matatizo mengi katika ndoa. Katika ndoa kama hizi, mwenzi ambaye hubaki nyumbani hujawa wasiwasi kuhusu usalama wa mwenziwe. Kwa mfano, Jamila amekuwa akilia na kujiuliza kuwa: "Hadi hii? Hadi lini Duni utaendelea kurudi nyumbani chakari ...mwisho wa haya utakuwa lini, Ya Rabi?" (Uk.51). baadhi ya watu huweza kuvunja ndoa zao kutokana na matatizo kama hayo. Ndoa zenye misukosuko huwafanya majirani kuwalaumu na baadhi ya kutoa ushauri wa kusitisha mahusiano hayo. Kwa mfano, Ramla alishauri "wee hu kiwete ...kwani kakununua?" (Uk.53). Naye shangazi na mlezi wake Jamila alishauri kuwa "madhali ndoa ni mkataba ufungao urafiki wa kitambo, basi na uvunjwe ikiwa huo urafiki uliotarajiwa haukupatikana" (Uk.53). Huo ni ushauri mwema, endapo ndoa imekuwa "jehanamu" (Uk.54). Hata hivyo kuna baadhi ya wanaume ambao zaidi ya huruma hujaribu kuwanyemelea wanawake wa watu wanapoona kuwa hakuna masikilizano mazuri. Haya yamedhihirishwa kupitia kwa Salim, rafikiye Hamduni anayemweleza Jamila, "Nakuhurumia na kupenda shemeji. Kwa nini huikimbii jahanamu hii" (Uk.54). Swali hapa ni kwamba, Salim kama rafikiye hamduni anawezaje kumpenda mke wa mwenziwe? Mwafaka ambao angeufanya na kumshauri na kumwonya rafikiye na kama haikuwezekana angemweleza Jamila kutafuta njia ya kumfanya Hamduni kuepukana na ulevi. Kwa hakika, Jamila hafanyi juhudi zozote kumshinikiza mumewe kubadili mienendo yake. Anapopigwa, hateti hata anapoumizwa vibaya.Ana imani kuwa mumewe anampenda.Swali ni, je, Duni alimpenda kwa dhati mkewe? Dhuluma na mapenzi zinaweza kuandamana?

2. **Ujirani Mwema**

Kulingana na mtunzi Hamduni alikuwa akiwaletea kero majirani wake kwa ulevi wake. Jambo hilo halikuwa zuri, kwa sababu, wengi wao huwa wamelala usiku lakini bughuda

Za Hamduni huwakosesha amani hiyo kutokana na kelele za kilevi. Hata hivyo, kutokana na ujirani wema, walimvumilia Hamduni.Kadhalika, majirani wema huwa hawafurahi wakimwona mwenzao akiandama mambo ya kufedhehesha. Hiyo ndiyo sababu, baadhi yao hufika kwake Hamduni ili kutuliza zogo kati yake na mkewe. Kwa mfano imeelezwa kuwa "Huko zilijangaza hata majirani wakawa wanazipata zitendwazo na zisemwazo. Pengine hii ndiyo sababu ya kuzuka hao

wenye huruma tele nyonyo. Kipigo kilipozidi, wakawa wanawahi kuja mbio mlangoni kuombea, na matusi yalipochagiza wakawa wa mwanzo kupiga ‘msalie mtume, mwanetu wee!’ (Uk.53). hata hivyo, tahadhari inayotolea ni kwamba, si majirani wote ambao huwatakia wenzao mema. Mfano ni ule wa kauli za Salim ambapo alimtaka Jamila kuvunja ndoa yao na amwandame yeye. Kwa ujumla ujirani mwema ni nguzo ya ushirikiano na masikilizano mema katika jamii.

3. **Unafiki**
   Hii ni hali ya kujifanya mwema ilhali hana wema. Salim, rafikiye Hamduni ni mnafiki. Baada ya kumshauri rafikiye abadilishe mienendo na akome kumtesa mkewe, Salim anamnyemelea mke wa rafikiye. Anajitia kumhurumia Jamila kwamba ameumizwa na Duni na kumtaka amtoroke ili amchukue yeye. Ni dhahiri kuwa marafiki wa sampuli hii ni hatari. Wanafaa kuepukwa. Hata hivyo, Duni alikuwa amezama katika ulevi, hangeng’amua kuwa Salim ni ndumakuwili.

   Tabia zake Duni pia zinadhihirisha unafiki. Baada ya kumpiga kinyama mkewe, asubuhi inayofuata anamtendea wema uliokithiri ili kujaribu kufuta maovu aliyotekeleza. Anajifanya kumpenda mkewe lakini ukweli hudhihirika baada ya muda mfupi anaporudia tabia zake za kukirihisha. Iwapo kwa hakika Duni alimpenda mkewe. Ajabu ni kuwa Jamila hautambui unafiki wa mumewe. Anaendelea kuishi katika ndoa iliyojaa dhuluma, akishikilia kuwa mumewe anampenda.

4. **Uvumilivu katika maisha ya Ndoa.**
   Imekuwa kawaida kwa jamila kupigwa kila siku baada yaa Hamduni kulewa chakari. Licha ya kero na aibu anayoiletea familia yake change, Jamila anavumilia haya maisha magumu ya ndoa.
5. **Ulevi na Athari zake katika jamii**.
   Hamduni humpiga mkewe kila anapolewa chakari.
   Jambo hili limemfanya jamila kuwa na simanzi kila wakati.
   Ulevi pia umemfanya Hamduni kuwa kerokwa majirani kiasi cha yeye kutishiwa kuchapwa nao.
   Kutokana na ulevi wake, marafiki kama vile Salim wamegeuka na kuanza kumtongoza mke wake Hamduni
6. **Majuto**
   Duni kwa kawaaida huwa anajuta tu punde baada ya ulevi kumtoka. Yeye hulia kwa uchungu na hata kujaribu kumwomba msamaha na kuonyesha kuwa anayajutia matendo yake.
   Jamila huwa anaonyesha majuto kwa kuuliza kama kweli maisha ya ndoa huwa ya namna ile. Maisha ya kupigwa kila wakati na kupata dhiki.

Usawiri na ujenzi wa wahusika

Wahusika wakuu ni Duni na mkewe Jamila. Kuna wahusika wadogo kama vile Salim, shangazi, Ramla na majirani.

1. **Hamduni au Duni**
   Ni mkaazi wa Sebleni na ana mke kwa jina la Jamila.

   Sifa

   a) ***Ni mlevi*.** Ulevi umemtawala na amekuwa akirudi kwake usiku wa manane. Wakati akiwa mlevi hupenda kuimba kwa sauti ya juu. Amekuwa akimdhikisha mkewe kwa tabia ya ulevi na kurudi nyumbani usiku usiku.
   b) ***Mwenye kureka***. Hana mlahaka mwema na majirani zake kwa sababu ya tabia zake za kukirihisha.
   c) ***Ni msanii na mwimbaji wa taarab*.** Ni mwenye kipawa cha kutongoa tungo za kimahaba. Huenda tungo hizo zilikuwa zikielekezwa hasa kwa mkewe ambaye kimoyomoyo alizifurahia. Kwa mfano, aliposikia nyimbo hizo yeye aliitikia kuwa:

      Si mengi yaniwekayo, ewe mpenzi.
      Laikini ni mapenziyo, wangu lazizi.
      Na maeko unekayo, sijiwezi (uk.51)
   d) ***Ni katili na mwenyedhulma***. Ni mume katili anapolewa. Kutokana na athari za ulevi, amekuwa akizua zogo nyumbani kwake. Kwa sababu imeelezwa kuwa, "Duni alikuwa mpigaji mkubwa asiye mfano. Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga." Aidha, jambo hili limebainishwa kwamba, "lile teke la mbavu alilorushiwa Jamila eti kwa sababu hakufanya haraka kuleta chakula, ambacho hata vile kulikuwa hakikuliwa" (uk.53 -54).
   e) ***Ni mpyoro***. Alikuwa mbishi na aliyependa matusi. Kwa mfano, majirani walipomwonya kuhusu ghasia alizokuwa akizua "kwa kila baada ya adabu moja aliyopewa alizidisha vituko viwili, ikiwa ni pamoja na matusi na kelele zaidi." (Uk.50).
   f) ***Ni mwenye nafsi mbili***. Ingawa, alitenda maudhi mengi, asubuhi yake alienda jikoni kutayarisha staftani na kutayarisha maji mojo ya kuoga. Isitoshe, "akazikunjakunja nguo chafu zote ndani ya nyumba, nyingi zikiwa ni za mkewe, na kuenda nazo uwani" (Uk.55). hata matendo haya yanadhihirisha nini kuhusu wasifu wa Duni? Hii inaonekana ama hajielewi au ni mwenye nafsi mbili; ya wema na ya uovu.
   g) ***Aliyekengeuka-***. Ni mume wa kisasa ambaye hakuona aibu kusaidia katika shughuli za nyumbani. Wakati akiwa mlevi hutenda matendo yasiyo ya utu

lakini nishai zinapomtoka huwa ni mwenye utu na huelewa kuwa amekuwa akimfanuia vibaya mkewe. Hiyo ndiyo sababu ya kuelezwa kuwa "Masikini, hata mlevi huyu kumbe alikuwa na hisia, alikuwa akilia kujililia mwenyewe na kumlilia mkewe! (Uk.55).

h) ***Ni mwoga na kigeugeu*****.** Anapong'amua kuwa anamtendea unyama mkewe, anabadilika kwa muda tu kisha anaanza kufanya tena maovu aliyozoea kutenda. Hii ni tabia ya kigeugeu.
i) ***Ni mpishi hodari***. Alifanya kazi kama mpishi hotelini na alimwandalia mkewe kisabeho
j) cha kukata na shoka.

Umuhimu wa Duni

i) Mwandishi amemtumia kuonyesha jinsi ulevi huzua migogoro katika ndoa na jamii kwa jumla.
ii) Ni kielelezo cha wahusika wenye nafsi mbili. Mara ni waovu kupindukia, mara
wamenadilika na kuwa na wema usioeleweka.
iii) Ametumiwa kuonyesha jinsi maridhiano yanavyoweza kufikiwa kupitia kuomba
msamaha.
iv) Anadhihirisha taasubi za kiume katika jamii kupitia kwa vitendo kama vile kumpiga mkewe.

Jamila

Jamila ni mkewe Hamduni. Alikuwa ameishi katika ndoa kwa miaka miwili.

Sifa

a) ***Ni mwenye mapenzi ya dhati***. Alimpenda mno mumewe. Hakutaka kitu chochote kuweza kuwa kikwazo katika maisha yake ya ndoa. Hii ndiyo sababu Salim alipomtaka kuivunja ndoa yao, yeye alisema kuwa "Ama Salim amezidi tena. Yaani anadhani mimi nimekosa mapenzi ya mume wangu". (Uk.54)
b) ***Ni mwenye subira na matumaini katika maisha ya ndoa***. Kwa hivyo alimstahi mumewe ambaye ni mlevi huku akiwa na mawazo kuwa "suala la kuachana na mumewe halikupata kumpitikia mawazoni mwake hata siku moja na abadani asingeliwafiki shauri hilo" (Uk.53).
c) **Amekuwa *mwaminifu*** kwa mumewe na kuepuka vishawishi kutoka kwa majirani kama vile Salim. Salim alimtaka amkimbie "shetani huyu"

(Uk.54) lakini anakataa katakata kuridhi kishawishi hicho. Aliona kuwa huo ni msalaba wake.

d) ***Ana msimamo dhabiti*.** Kutokana na msimamo wake usiotererereka, anaamua kumvumilia mume wake wa ndoa.
e) Ni mwanamke ambaye ana ***moyo wa kusamehe*** na kusahau yaliyopita. Kwa mfano, anamwambia Hamduni, "wewe ni mume wangu; Mpenzi wangu. Kama ni kukosea, wangapi wakoseao, Dii? Wangapi wenye makosa makubwa kushinda yako?" (Uk.56). ingawa hapo awali mumewe alikuwa mtu ambaye humzulia baa, yeye hakutaka kufokeana au kujibizana na mumewe. Kwa kutaka amani anasema kuwa, "Aaa, aaa, Dii, hebu punguza zogo. Jamila alimbembeleza. Watu wamelala wamelala ... haya basi sikusaidii, najua unaweza kila kitu" (Uk.54). Jamila alisema hivyo kwa upole ili kusiwe na mabishano kati yake na mumewe, anawahurumia wanawake wengine amabo wamo katika mkasa wa ndoa kama yake.

Umuhimu wa Jamila

i)Ametumiwa kama kielelezo cha jinsi wanawake wanavyoteswa katika ndoa.
ii) ni kielelezo cha jinsi msamaha unavyoweza kuleta maridhiano.
iii) Jamila anatumiwa kama kielelezo cha madhila katika ndoa kwa kuzingatia sifa za uvumilivu, kusamehe na kuridhiana.

Salim

Sifa

a) ***Kijana nadhifu au 'mtanashati'***. Hapa mwandishi anamsambambaisha na Duni ambaye ulevi wake unamkosesha unadhifu.
b) ***Mwenye ulaghai*** wa kimapenzi na ***msaliti.***
c) Rafikiye Duni wa 'wa chanda na pete'. Kauli hii ni kinaya kwa vile Salim humfuata Jamila na hivyo si rafiki wa dhati.
d) ***Mnafiki.*** Anajifanya rafikiye Duni ilhali anamtongoza mkewe.
e) ***Mchochezi***. Kwa vile anachochea Jamila aiache ndoa yake bila mafanikio.

Umuhimu wa Salim

i)mwandishi amemtumia kama kielelezo cha urafiki usio wa dhati unafiki.
ii) kupitia kwake, tabia ya uaminifu wa Jamila inadhihirika.

Wahusika wengine ambao wanaweza kuzingatiwa ni kama vile:

- Ramla.
  Yeye ni shogaye Jamila. Yeye ni mchochezi kwa kuwa alikuwa anampa jamila ushauri kuwa anafaa kutengana na mumewe. Yeye ni kiwakilishi

cha wanajamii wasiotoa ushauri ufaao. Kupitia kwake, tunapata kuona msimamo dhabiti wa Jamila.

Mbinu za lugha

Mwandishi ametumia mbinu kadhaa ili kukoleza utamu wa hadithi katika kuwasilisha ujumbe kwa mnato na namna inavyoathiri.

1. **Methali**
   a) Dua ya kuku haimpati mwewe (Uk.50). laana na maapizo ya majirani hayakufua dafu katika kumfanya Duni kubadili mienendo yake duni.
   b) Tabia haigangiki (Uk.50). tabia haiwezi kubadilishwa na mtu kwa vile Duni alipuuza ushauri na vitisho vya Wasebleni.
   c) Usilolijua ni usiku wa kiza (Uk.54). jamila anaona kuwa watu hawaelewi kuwa mumewe anampenda.
   Methali hizo zimechangia katika kuwasilisha na kuubainisha zaidi ujumbe wa msanii.

2. **Istiara**
   a) Firauni (Uk.51. hii ni istiari ambayo inaonyesha udhalimu wake Duni jinsi anavyomtesa mkewe.
   b) Kinda (uk.51). Jamila ni Kiumbe anayepaswa ktuzwa wala si kuteswa.
   c) Mkataba (Uk.53). Ndoa inalingaishwa na mkataba kwa vile ni makubaliano baina ya watu wawili.
   d) Jahanamu (Uk.54). ndoa ya Jamila na Duni inalinganishwa na jahanamu kwa vile imejaa mateso.
   e) Kalenda (Uk.57). Imetumika kurejelea maisha ya Jamila.

3. **Tashibihi**
   Mwandishi ametumia mbinu ya ulinganisho wa moja kwa moja,
   Kwa mfano:
   a) Kinda kama Jamila (Uk.51).
   b) Alimpiga mkewe kama ngoma ya kimanga (Uk.53).
   c) Kuadhibiwa kama mwana asiye na kwao (uk.53).
   d) Yakachirizika mithili ya maji ya mvua katika ukingo wa bati. (Uk.55)

4. **Maswali ya Balagha/Maswali Butu**
   Maswali haya yasiyohitaji majibu yametumiwa ili kumfanya msomaji kutafakari zaidi hali zinazorejelewa.
   a) Hadi lini?

b) Hadi lini Duni ataendelea kurudi nyumbani chakari na wimbo wake huu (Uk.51).
c) Mwisho wa haya utakuwa lini, ya Rabi? (Uk.51)
d) Kwa nini akukongeshe ungali mbichi hapo ulipo? (Uk.53).
e) Kwani kakununua? (Uk.53).
f) Ananipenda? (uk.54).
g) Unalia nini Dii, Duni wangu? (Uk.56)
h) Wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anayofanyiwa na mume wake? (Uk.56).

5. Tashihisi

Mwandishi ametumia sana tamathali hii ya uhuishi.

a) Mtaa wa sebleni ulikuwa umegubikwa na utulivu mkuu. (Uk.50)
b) Nyakati kama hizi, ambayo mtaa wa Sebleni uliburudishwa na mtiribu huyu wa usiku wa manane. (Uk.50)
c) Sauti ilipenya kila dirisha na kupanda katika kila roshani. (Uk.51).
d) Walipopata wasaa huruma zao zilivuka mipaka kuwa mkombozi. (Uk.53).
e) Teke lilimtupa Jamila kwenye kochi (Uk.54).
f) Uso wake unabeba simanzi tupu kila wakati hata akiwa usingizini (Uk.55).

6. Majazi

a) Hamduni au Duni. Ni mtu ambaye si kamilifu wa utu. Mwanzoni jina 'Duni' lilikuwa ufupisho wa 'Hamduni' lakini baadaye mhusika akawa anadhihirisha tabia duni.
b) Sebuleni. Sehemu ya kubarizi au kustarehe.
c) Jamila. Kutokana na 'jamala' ladhihirisha wema wake Jamila, wa sura na tabia pia.

7. Utohozi

a) Dii (Uk.54 na 56). Ni ufupisho wa neon waitanalo wapenzi 'dear'.
b) Bendeji (uk.54). (Bandage)
c) Breki (Uk.54). (break)
d) Kochi (Uk.54). (Coach)
e) Supu (Uk.55) . (Soup)
f) Kalenda (Uk.57). (Calender)
g)

Mtindo katika uwasilishaji

1. **Viona Nyuma/ Mbinu rejeshi / kisengere Nyuma**
   Hii ni mbinu ya kisimulizi ambapo mwandishi hurejesha msomaji kwa mambo yaliyotendeka na yanayohusiana na yaliyomo.
   a) Jamila anakumbuka ushauri wa majirani, rafikiye Ramla, shangaziye na hate unafiki wa Salim (Uk.51,53)
   b) Mateso ambayo huyapata mumewe anapolewa yamebainishwa kupitia mbinu rejeshi.
2. **Nyimbo**
   Nyimbo hizi zimechangia utata na kitendawili cha ndoa yao Duni na Jamila. Ni taarab za kimahaba.
   i) Nyimbo za Hamduni wakati wa kutoka ulevini (Uk.50,51, 57)
   ii) Kujiimbia kimoyomoyo kwa Jamila. (uk.51).

3. **Mpangilio wa Uwasilishaji**
   Uwasilishaji wa hadithi hii umegawanyika katika sehemu nne mahususi:
   i) *Sehemu ya kwanza*: (inazingatia dibaji ili kudhihirisha mazoea ya ulevi wa Hamduni).
   ii) *Sehemu ya pili*. (inazingatia bughudha za kilevi za Hamduni na nasaha zinazotolewa).
   iii)*Sehemu ya tatu*. (Inazingatia maisha ya ndoa ya Jamila na Hamduni na jinsi Duni anavyoupiga teke uduni wake ulevi unapomwishia. Anamtendea mkewe matendo mema yanayomfanya kuamini anampenda).
   iv)*Sehemu ya nne*. (Inazingatia hali ya kukatisha tamaa kwa vile ndoa hii inarudia hali yake ya mateso baada ya muda mfupi).

MWANA WA DARUBINI.

Mandhari ya Hadithi

Mandhari yanayosawiriwa ni yale ya kijijini na mjini. Kijijini watu wamekuwa wakiishi maisha ya shida, mjini paliishi watu amboa walijiweza kiuchumi. mazingira hayo ni yale ya baada ya ukoloni, yaani baada ya nchi hizo kupata uhuru. Kwa wale waliopata elime waliweza kuimarisha uchumi wao na wale wa vijijini, maisha yalikuwa magumu.

Dhamira ya Mtunzi

Mtunzi kueleza ukosefu wa utu miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, kananda alitokana na jamii ya kimasikini. Kwa hivyo, aliwafanyia kazi akina Bw. Na Bi. Mwatela huko mjini. Hata hivyo, Bwana Mwatela alianza kumrai Kananda katika masuala ya mapenzi ya siri na hatimaye

kumwingiza katiak mateso. Funzo linalopitiswa katika hadithi hii ni kwamba, si vyema kukosa utu.

Maudhui

Maudhui ni kama vile kazi, malezi ya watoto, ulevi na utu.

1. **Kazi**

    - Wazazi wa Kananda walipofahamiswa kuwa Kananda atapata kazi, walifurahi mno, “wazazi wa Kananda walifurahi ghaya kupatas bahati hiyo” (Uk. 99). Ingawa Kanada alipata kazi ya uyaya, kazi ni kazi.

    - Bwana Mwatela alikuwa akifanya kazi katika kampuni ya “Simba Breweries” (Uk. 99).

    - Mkewe Bwana Mwatela, Bi Maria alikuwa akipata mafunzo katika taaluma ya ualimu katika chuo kimoja kijini” (Uk 99).

    - Kadhalika, Mbao (ami yake Kananda,) alikuwa akifanya kazi jijini Nairobi (ukaa). Kwa hivyo, mtu anapofanya kazi anahitaji kuifanya kwa bidii na kuepukana na mambo ambayo huweza kusababisha umwagaji unga. Kwa mfano, Bwana Mwatela, alipozembea kazini hakusita kupigwa kalamu.

    - Bwana Mwatela alipoteza kazi yake kutokana na ulevi. Alipofutwa kazi alirejea kwao na kufikiria tena namna atakavyojiendeshea maisha. Alipoacha ulevi, aliweza kuifanya kazi yake vizuri, kama inanvyoelezwa kuwa alianzisha “kazi ya uvuvi na kuuza samaki” (Uk. 101).

Malezi ya watoto

- Malezi ya watoto ni jukumu ambalo wazazi hupaswa kulitekeleza. Kwa mfano, Bwana Mwatela na mkewe walimlea mtoto wao Sami kwa njia zote zinazostahili.

- Kwa sababu ya shuguli za kikazi na uanafunzi wa Maria, walimwajiri Kananda aweze kumshughulikia iwapo uwezo huo upo.

- Wazazi wa Kananda waliweza kumlea hadi pale alipokuwa mkubwa. Kwa ambavyo walikuwa masikini, walikubali aende Nairobi kufanya kazi kwa kuandamana na ami yake, Mbao.

- Kadhalika, Kananda alipompata mtoto, mapenzi yake hayakukatika kwake. Alipokuwa ameuzwa huko Kongo kama mtumwa, mawazo yake yalikuwa kwa mtoto wake, Mwakitawa. Kutomwona mtoto wake ambaye alipokonywa

kulimhangaisha mno. Furaha yake hikutimilika pasi na kuwa na mtoto wake. Alimtafuta kwa udi na uvumba hadi akampata.

- Bwana na Bi. Mwatela waliweza pia kumlea Mwakitawa hata ingawa walikuwa wazazi wa ulezi. Mtoto huyo alilelewa na wazazi hao wa kambo ingawa kosa lililofanyika ni kumficha asili ya uzawa wake.

- Kulingana na mtunzi ni kwamba motto ana haki ya kujuzwa uzawa wake. Hii ndiyo sababu Maria kumtaka mumewe amwambie, “Mwakitawa sasa hivi… ukweli kwamba alikuwa anaua mama yake mzazi” (Uk. 106). Kukosa kumweleza motto ukweli kuhusu uzawa wake ni kumkosea.

2. Umasikini/Ajira kwa watoto..

- Jamii inayosawiriwa katika hadithi hii ile ya wale wanaojiweza na wale ambao ni maskini au wasiojiweza kiuchumi.

- Watoto wa familia ambazo haziwezi wanaowatumikia walio na uwezo. Watoto hao hata kabla ya kuujua ulimwengu huuza nguvu zao kwa wale wanaojiweza. Mfano hapa ni ule wa Kananda ambaye anakubaliwa na wazazi wake kuenda kufanya kazi ya uyaya katika familia ya Bwana Mwatela huko Nairobi.

- Watoto hao hutumukishwa kazi mbalimbali na kutumiwa vibaya na baadhi ya waajiri. Kwa mfano, Bwana Mwatela alipotaka kufanya mapenzi na Kananda, alimweleza, “usipoachana na mambo haya nitaacha kazi. Hata hivyo, Kananda alelewa kitisho hiki hangekitekeleza”. Hela alizozipata ziliwaauni wazazi wake pakubwa” (Uk 99).

- Tatizo hapa ni kwamba, kama Kananda angekuwa na uwezo wa kiuchumi angejiondokea. Jamii ya kimaskini, hutatizika mno katika maisha yao. Kwa mfano, Kananda anauzwa huko Kongo kama mrumwa na kupokonywa motto wake aliyemzaa. Huu ni unyama ambao haustahili kutendwa.

3. Ulevi

- Bwana Mwatela alimpiga mkewe kichapo cha mbwa” (Uk. 99) huku akimwonya. Jambo kama hili huweza kusababisha ndoa kuvunjika.
- Kadhalika, Bwana Mwaleta hazingatii kalamu. Isitoshe, anataka kufanya mapenzi na mhudumu wao wa nyumbani. Haoni soni hata ingawa ameoa na wana watoto.
- Ulevi wa kupindukia huweza pia kumletea mtu aibu. Kwa mfano, imeelezwa kuwa, “ulevi wa Mwatela ulimtia doa Kananda. Kananda alifadhaika sana lakini akaona heri anyamaze” (Uk. 99) Aidha ulevi wake ulimfanya Bwana Mwatela kupoteza kazi nzuri alipofutwa.kutokana na mtunzi, ulevi ni pingamizi la mauendeleo na ukosefu wa kimaadili katika jamii.

4. **Utu**
    - Bwana Mbao aliweza kufahamu matatizo yaliyopo kwa kina Kananda. Kwa hivyo, aliposikia kuwa Bwana na Bi. Mwatela alihitaji mtu wa kazi ya uyaya, alikumbuka jinsi ya kuisaidia familia ya wazazi wa Kananda. Hii ndiyo sababu ya kufunga safari ya kuwaletea "ujumbe wa heri" (Uk. 99).
    - Kananda alipohitaji msaada wa kumtafuta motto wake, alisaidia psi ya kutarajia chochote.
    - Askofu Mzungu huko Kongo alimsaidia Kananda kwa kumtoa utumwani.
    - Katana pia alikuwa mtu mwema, wlifahamiana na Bwana Mwatela na kila alipopata nafasi alimtembelea huko Mombasa ili kumjulia hali. Katika hadithi immelezwa kuwa, "Katana alikusudia kuenda kumtembelea Mwatela" (Uk. 102). Huu ni usuhuba ulijengwa kwa msingi ya utu.
    - Kadhalika, mwanawe Mbao alipokea ujumbe kwamba babake mzazi anamhitaji kule kijijini alifika mara moja. Kutokana na ushauri wake, ni kwamba, rafikiye anaweza kumwazima darubini. Hii inaonyesha kuwa kijana huyo alikuwa na mlahaka mzuri na vijana wenziwe.

5. **Utabaka**

    Kananda ametoka familia maskini ambapo hata hawawezi kujiendeleza kimasomo na ndiposa anaondoka kwao na kuenda kuajiriwa kama kijakazi.

    Mwatela naye ni tajiri mkubwa mwanzoni na hata mwishoni mwa hadithi.Yeye alikwa mvuvi mkubwa ambaye alikuwa amewaajiri wafanyakazi kadhaa.

6. **Ndoa**

    Kuna maisha ya ndoa katika hadithi ambapo tunaiona ndoa kati ya mwatela na mkewe. Ndoa hii imejaa misukosuko kutokana na tabia ya mwatela ya ulevi na kuwavizia vijakazi kama vile Kananda.

    Pia tunaon kuwa Kananda anatoka katika familia ya kule kwao kijijini ambapo amewaacha wazazi wake.

7. **Maridhiano/ Majuto**

    Mwatela anaungama dhambi zake mwishoni mwa hadithi na kuamua kumfidia Kananda kwa madhila yote aliyompa. Anaamuua kumpa mali kama vile nyumba na kuahidi kumsomeshea mwana.

    Mwakitawa vilevile anaamua kumwomba mamake msamaha baada ya kugundua kuwa alikuwa amepotoshwa na mwatela. Kananda anamsamehe.

8. **Ukatili**
    - Mwatela anamua kumbaka kananda ambaye ni motto mdogo nakisha baada ya kugundua kuwa ana uja uzito anamtisha ili asije akamwambia mtu yeyote.

- Mwatela amampokonya Kananda motto na kasha kumuuza kama mtumwa katika taifa la kongo.
- Mwatela anamchochea kananda dhidi ya Mwakitawa, jambo linalosababisha Mwakitawa kumwumiza mamake kwa jiwe.
- Bw. Mwatela alimchapa mkewe kichapo cha mbwa walipokuwa wanazozana.

9. Ulaghai

- Mwatela anamlaghai kuwa atamwoabaada ya kugundua kuwa ana uja uzito. Hata hivyo anaenda kinyume cha maafikiano yao kwa kumpokonya mwana na kumuuza kama mtumwa huko Kongo
- Baada ya kumuuza kananda, mwatela anawalaghai wazazi wa kananda kuwa Kananda alikuwa ametoweka katika hali isiyoeleweka.
- Mwatela vilevile anamlaghai mwakitawa kuwa kuna watu ambao ni wakora wanaomtaafuta ili waweze kumteka nyara ili waweze kudai fidia.
- Mwatela alimhadaa Mwakitawa kuwa mamake alikuwa ameaga dunia.
- Baada ya mwatela kuambiwa kuwa kuna mwanamke ambaye huitazama nyumba yake kwa darubini, yeye anasema kuwa huenda akawa ni mtu anayeipenda nyumba yake. Hakutaka kwenda polisi ili siri yake isije ikajulikana.
- Mwatela vilivile alimdanganya katana kuwa mamake mwakitawa alikuwa amefariki.

10. Usaliti

- Mwatela anmsaliti mkewe baada ya kujihusisha kimapenzi na Kananda mkewe alipokuwa ameenda safarini.
- Hata baada ya kupewa Kananda ili amsaidie kama yaya, Mwatela anaamua kumbaka Kamanda. Anaisaliti imani ambayo wazazi wa Kananda walikuwa nayo kwake.
- Mwatela anamsaliti mwakitawa kwa kumchochea dhidi ya Kananda; jambo linalopelekea mwakitawa kumwumiza mamake kwa jiwe.
- Mwatela anamlaghai kuwa atamwoabaada ya kugundua kuwa ana uja uzito. Hata hivyo anaenda kinyume cha maafikiano yao kwa kumpokonya mwana na kumuuza kama mtumwa huko Kongo.
- Bi. Mwatela anamsaliti mumewe baada ya kumwambia mwakitawa ukweli kuwa yeye alikuwa sio mwana wao halali.
- Katana vilevile alimsaliti Mwatela kwa kumwelekeza Kananda hadi katika eneo la makaazi ya Mwatela.

Usawiri wa Ujenzi wa Wahusika

Kananda ndiye mhusika mkuu, kwenye hadithi. Wahusika wadogo ni Bwana na Bi. Mwatela, Katana na Mwakitahi.

Kananda

Alizaliwa miaka mine kabla nchi ya Kenya kupata uhuru. Hakupelekwa shule kutokana na umaskini wa familia au jamii yake kwamba, “uchochole wao haungewawezesha kumsomesha” (Uk. 99.

Sifa

(a) ***Alikuwa na mlahaka mzuri na wazazi wake***. Kwa sababu aliishi nao hadi pale alipohitajika kuenda kufanya kazi Nairobi.

(b) ***Katika muktadha wa masuala yasiyokuwa ya kiuadilifu, alikuwa na msimamo madhubuti.*** Kwa hivyo, anamwambia Bwana Mwaleta kuwa, “usipoachana na mambo hayo nitaacha kazi” (Uk. 99). Alipata mimba ya Bwana Mwatele kutokana na shinikizo la Bwana huyo.

(c) ***Kananda alikuwa msiri.*** Hakutoboa siri na wala hakutaka kuitia ndoa ya Bwana na Bi Mwatela. Alikuwa ni anaelewa kuwa.
Bwana Mwatela alikuwa akimndanganya kuhusu masuala ya ndoa. Kwa hivyo, hakutaka kuzubaishwa kwa hilo.

(d) ***Mwenye bidii kutokana na kazi yake nzuri, aliweza kusifiwa na mamake Sami.*** Hii ndiyo sababu ya kuambiwa kuwa, “usibabaike. Ukijifungua nitakusaidia kwa njia nyingi” (Uk 100).

(e) ***Kananda alifanya mipango yake kwa makini.*** Kwa mfano, jambo alilolitaka zaidi ni kumwona mwanawe, kwa hivyo, alitaka darubini ili aweze kumwona mwanawe lakini hilo alilifanya kwa hadhari ili asiweze kuonekana.

(f) ***Alikuwa msahemevu*** Kwa mfano, alipoona kuwa Bwana Mwatela ameomba msamaha wa dhati, analikubali ombi hilo na kufungua ukurasa mwingine wa maisha yake.

Umuhimu wa Mhusika Kananda

(i) Anawakilisha tabaka maskini linaloteswa na matajiri.
(ii) Ni kielelezo cha mzazi anayemlinda mwanawe.
(iii)Mwandishi amemtumia kuwakilisha ukweli wa methali “Baada ya dhiki, faraja”

Bwana Benjamin Mwatela

Anaishi mjini Nairobi na anafanya kazi katika Simba Breweries japo baadaye, anafutwa kazi na kurudi kwao Pwani.

Sifa

(a) ***Mlevi kupindukia***. Alikuwa ameoa na na walibarikiwa kupaa motto wa kiume alioyeitwa Sami. Kutokana na elevi alikuwa akitenda mambo yasiyo ya utu. Kwa mfano, alikuwa akizua ugomvi na mkewe huku akimtisha kuwa, "tusije tukajadili kuhusu ulevi wangu daima katika nyumaba hioi". (UK 99)

(b) ***Mwenye mapuuza.*** Kadhalika, hukupenda kutilia maanani mawaidha aliyopewa. Kwa mfano, anashauriwa aache maswala ya mapenzi na Kananda lakini hakutilia maanani.

(c) Ni mtu ambaye ni katili. Jambo hili linadhirishwa wakati anapompokonya Kananda motto na kumfanya kuenda kuuzwa katika utumwa huko Kongo. Anampa Mwakitawa kisu akitumie.

(d) ***Ni mdanganyifu***. Kwa mfano, anatumia ujumbe kwao Kananda kuwa, "mwanao alitoweka na hakuna aliyejua alikotorokewa" (Uk. 101). Uvumi huo pia umedhihirisha kupitia maelezo aliyompa Katana kwamba, mama yake Mwakitawa alifariki" (Uk. 103). Kutokana na elevi anafutwa kazi katika kampuni ya Simba Brewweries na kurejea "kwao huko Taita Hills" (Uk 101).

(e) ***Mwenye kutubu.*** Aliacha mambo ya ulevi na kuanzisha kampuni yake ya uvuvi na samaki. Wakati huo, Mwatela alikuwa ameacha nyendo zake za hapo awali. Kutokana na hali hiyo ya mabadiliko, amekuwa mashuhuri mjini Mombasa.

(f) ***Mwenye huruma***. Ingawa alikuwa mpiga tindi, alikuwa mwenye moyo wa huruma. Kwa nmfano, alimsaidia kumpeleka Kananda hospitali wakati wa kujifungua. Hilo pia limedhihirishwa kwa kumpeleka mkewe kwa matibabu ya dharura.

(g) ***Mwenye kujirudia.*** Alikuwa mtu wa kuomba msamaha wa dhati hasa alipongundua kuwa ujanja wake ulijulikana. Huyu ni mhusika ambaye hudhihirisah sura mbili za wasifu wake.

- ***Katili*** - Mwatela anamua kumbaka kananda ambaye ni motto mdogo nakisha baada ya kugundua kuwa ana uja uzito anamtisha ili asije akamwambia mtu yeyote.
- Mwatela amampokonya Kananda motto na kasha kumuuza kama mtumwa katika taifa la kongo.
- Mwatela anamchochea kananda dhidi ya Mwakitawa, jambo linalosababisha Mwakitawa kumwumiza mamake kwa jiwe.
- Bw. Mwatela alimchapa mkewe kichapo cha mbwa walipokuwa wanazozana.

Msaliti- Mwatela anmsaliti mkewe baada ya kujihusisha kimapenzi na Kananda mkewe alipokuwa ameenda safarini.

- Hata baada ya kupewa Kananda ili amsaidie kama yaya, Mwatela anaamua kumbaka Kamanda. Anaisaliti imani ambayo wazazi wa Kananda walikuwa nayo kwake.
- Mwatela anamsaliti mwakitawa kwa kumchochea dhidi ya Kananda; jambo linalopelekea mwakitawa kumwumiza mamake kwa jiwe.

- Mwatela anamlaghai kuwa atamwoabaada ya kugundua kuwa ana uja uzito. Hata hivyo anaenda kinyume cha maafikiano yao kwa kumpokonya mwana na kumuuza kama mtumwa huko Kongo.

Umuhimu wa Mhusika Bwana Mwatela

(i) Ametumiwa kuonyesha jinsi ulevi humuathiri sio tu mhusika bali watu wengine wanaohusiana naye.
(ii) Kielelezo cha watu makatili wanatendea watu maovu bila kusumbuliwa na nafsi zao.
(iii)Mwandishi amemtumia kuonyesha kuwa Mui anaweza kuwa Mwema.

Maria

Ni mkewe Bwana Mwatela. Alijaliwa kupata motto wa kivulana, Sami. Kwa bahati mbaya motto huyo alikufa kutokana ma moto.

Sifa

(a) Alikuwa mwenye bidii na alisomea taaluma ya elimu jijini, Nairobi.
(b) ***Mpenda amnai***. Hakupenda kuzozana na mumewe. Kwa mfano, anapoambiwa kuwa, "Tusije tukajadili kuhusu ulevi wangu daima katika nyumba hii" (Uk 99), haongezi zaidi.
(c) ***Alikuwa mwenye utu na huruma***. Alimhakikishia Kananda kuwa, "usibabaike. Ukijifungua nitakusaidia kwa njia nyingi". (Uk 100)
(d) *Mkweli*. Alipenda kusema kweli. Alimtaka mumewe amwambie Mwakitawa ukweli kuhusu uzawa wake. Alipokosa kufanya hivyo anachukua jukumu hilo la kumbainisha Mwakitawa"kila kitu" (Uk 107).
(e) ***Wakati mwingine alikuwa mwoga***. Kwa mfano, hakutaka kumweleza mumewe kuwa amemwambia Mwakitawa uzawa wake akihofu kuwa afya ya mumewe ingezorota.
(f) ***Mpenda utulivu***. Hakutaka kusumbuliwa kwa maswali mengi sio tu kutoka kwa mumewe hata kutoka kwa Mwakitawa.
(g) Hata hivyo, alikuwa msiri, hakumwambia Mwakitawa kuhusu uhalisi wa uzawa wake hadi pale anaona kuwa mumewe yu mahututi hospitalin

Umuhimu wa Maria

(i) Ametumika kuonyesha jinsi baadhi ya wake hunyamazishwa wasitoe maoni.
(ii) Ni kielelezo cha watu waadilifu katikla jamii. Amamlea Mwakitawa kwa utu hata kama si mwanawe.

Wahusika wengine wajenzi ambao wanaweza kuzingatiwa ni kama:

- Sami
- Mwakitawa
- Katana

- Mbao

Mbinu za Lugha

1. **Misemo**
   (a) Pangu pakavu (Uk 99)
   (b) Kuchapa mtindi 9Uk 99)
   (c) Kichapo cha mbwa (Uk 99)
   (d) Mlevi chakari (Uk 99)
   (e) Kumtia ndoa (Uk 99)
   (f) Hasira za mkizi (Uk 100)
   (g) Nitakutoa roho (Uk. 100)
   (h) Uligonga mwamba (Uk 100)
   (i) Alipanga njama (Uk 100)
   (j) Mungu hatupi mja wake (Uk 101)
   (k) Kumtia moyo (uk 101)
   (l) Kukuteka nyara (uk 102)
   (m) Aone cha mtema kuni (Uk 105).
   (n) Moyo wake ulichafuka (Uk 105)
   (o) Alinigusa (Uk 107)

2. **Tashihisi**
   (a) Kimya chake kikawa kinamchoma ndani kwa ndani (Uk 100)
   (b) Hakika ekimu inemrembesha zaidi (Uk 99)
   (c) Tabia hiyo ilimgonganisha na mkewe (uk 99)
   (d) Tumbo la gari (Uk 103)
3. **Jazanda**
   (a) Alianza kumchokoza (Uk 99).
   (b) Asali chungu ilizaa karaha (Uk 99)

4. **Chuku**
   Alilia usiku na mchana (Uk 99)

5. **Methali**
   (a) Maisha ni fumbo (Uk 108)
   (b) Mungu si Athumani (Uk 108)
6. **Maswali ya Balagha**
   (a) Uniulie nini na ndao yetu na wewe inamhusu pia yeye (Uk 100)
   (b) Kwa nini hufanani kamwe na wazazi wako (Uk 101).
   (c) Kwa nini nimwambie (Uk 106).
   (d) Nilikuwa namuua mama yangu (Uk 106)

(e) Mamangu yupi (Uk 106).
(f) Mungu weangu, nikimuopna mama huyo nitamwambia nini (Uk 107)
(g) Kananda, kumbe maisha ni fumbo (Uk 108).

Mtindo Katika Uwasilishaji

7. **Sadfa**
   (a) Kananda kupelekewa hospitali kijifungua na moto kutokea nyumbani kwa Bwana na Bi. Mwatela. Bi Mwatela na Kananda wako hospitali.
   (b) Bwana Mwatela na Kananda wamelazwa hospitali moja.
   (c) Mwakitawa kutoroka nyumbani kutokana na kuambniwa ukweli na Bi. Mwatela.
   (d) Kananda kupata kazi katika familia ya Bwana na Bi. Mwatela?
   (e) Kananda kupewa urithi na Bwana Mwatela.
8. **Mbinu ya Taharuki**
   (a) Askofu Mzungu kumwokoa Knanada (Uk 101).
   (b) Bwana na Bi Mwatela walichukua hatua kubwa ya kumzuia Mwakitawa kukutana na Kananda (Uk 102)
   (c) Mwatela kumnunulia Mwakitawa silaha (uk 102)
   (d) Kujeruhiwa kwa kananda na mwanawe (Uk 106)

9. **Taswira**
   (a) Kananda kubaini kuwa na "kijusi tumboni" (Uk 99)
   (b) Moto ulizuka katika makao ya Bwana na Bi Mwatela (Uk 100).
   (c) Mwatela alikuwa ametajirika san (Uk 101)
   (d) Kananda kulala masikini, akaamka tajiri (Uk 108)

10. **Viona Nyuma/Mbinu rejeshi**
    (a) Katana alikuwa rafiki mkubwa na Mwatela (Uk 102). Katana kukumbuka alivyoambiwa kuwa mamake Mwakitawa alifariki.
    (b) Siku moja Kananda alionekana tena na Yule rafikiye Mwakitawa (Uk 105). Wiki mbili zilipita na Mwakitawa hakurudi nyumbani.
    (c) Mwatela alifikiria kuhusu maovu aliyomtendea Kananda (Uk 107)
11. **Utohozi**
    (a) Kampuni (Uk 96) (company)
    (b) Hospitalini (Uk 100) (hospital)
    (c) Dereva (Uk 101) (driver)

MIZIZI NA MATAWI

Ali Abdulla Ali

Dhamira ya Mtunzi

Lengo kuu la hadithi hii ni kuelezea kuhusu athari za kuwatupa watoto punde wanapozaliwa. Mzazi anapomtupa mtoto huwa hamtendei haki. Mtoto huyo akibahatika huweza kupata mhisani kama vile Bimkubwa alivyompata Sudi na kumlea, kumpeleka shule na kuwa mtu wa muhimu katika jamii. Kadhalika, mtunzi ameeleza kuwa ni muhimu kuwajibika katika malezi ya watoto, kwani hawana hatia. Kwa sababu kama mtu hamtaki mtoto huyo kuna wale ambao hawakubarikiwa kupata watoto na wanapowapata hufurahia jambo hilo. Kwa hivyo, malezi ya watot si jukumu la mzazi tu bali pia kwa jamii nzima.

Maudhui

Maudhui makuu ni malezi ya watoto, utu na majuto.

1. **Malezi ya watoto**

malezi ya watoto ni jukumu la jamii. Kwa mfano, Sudi alizaliwa na Bi. Kudura na kisha akamtupa jalalani. Huenda mzazi huyo alikuwa hana namna ya kukidhi mahitaji yake, lakino kumtupa mtoto ni jambo la ukatili na ukosefu wa utu.
Wazo hili limedhihirishwa kupitia kwa maelezo ya Bi. Kudura kuwa, “Bimkubwa bibi yangu nikwambie nini mhisani wangu? Mimi niliwahi kuzaa tena mtoto mzuri wa kiume, lakini kwa kuwa nilimzaa nje ya ndoa na siku hizo ujana unanenda nilithubutu kufanya jambo la ajaby sana katika maisha na hapo ndipo nimuombapo Mungu anisamehe” (Uk.115).
Kutokana na utu wa Bimkubwa, Sudi analelewa vizuri hata na kuelimishwa. Ingawa mtoto huyo alikuwa wa kuelelewa tu alipata mapenzi ya mama kupitia kwa mtu mwingine mwenye huruma na utu katika jamii. Kwa hivyo, mtoto si wa kutupwa bali anafaa kulelewa katika mazingira mazuri.

Mtoto huyo anapolelewa, hapaswi kubaguliwa au kutendewa unyama. Kwa mfano, Sudi alitimiziwa yote yaliyopaswa kutendewa kama mtoto.
Zaidi ya kupelekwa shule, Bimkuhwa alimchukulia kama mtoto wake kabisa. Hiyo ndiyo sababu amekuwa akimwita, “Sudi mwanangu” (Uk.110). kwa ambavyo Sudi alikuwa “mwana” wa Bimkubwa anaeleza kuwa “Nilimuandikia mwanagnu Sudi tangu alipokuwa mdogo” (Uk.118). huo ni upendo mkubwa wa mzazi kwa mwanawe. Kwa hivyo, malezi ya mtoto hayawezi tu kutimizwa kupitia kwa mzazi wa damu hata kupitia kwa mzazi mlezi.

2. **Utu**

Bimkubwa alimwokoa Sudi alipokuwa ametupwa kwenye pipa la taka. Kadhalika,Sudi na “mamaye” walikuwa na mahusiano mazuri pale nyumbani. Kila mara walipozungumza

heshima ilidumishwa. Hakuna hata mara moja ambapo walikoseana heshima. Mama huyo alipokuwa akihuzunika alitulizwa moyo na Sudi kwa kauli kama vile, “Usilie mama” (Uk.111).

Kadhalika, kudura mfanyikazi wa nyumbani alikaribishwa kwa mapokezi mazuri. Bimkubwa alizungumza naye vizuri na malikuwa na mahusiano murua. Kudura alipokuwa kwao Sudi alipewa “chakula na pahali pa kuweka ubavu” (Uk.114). nguo pia alipata.

Kutokana na heshima aliyokuwa nayo Sudi, hakuwahi, “kumtuma hata kijiko cha kukorogea sukari” (Uk.115). hii ni kwa sababu Bi. Kudura alikuwa hirimu la “mama” yake.

Utu wa Sudi ulimfanya kutompita Kudura kila alipomsimamisha barabarani karibu na mavani.

Sudi aliweza kumsaidia Kudura kupata ajira pale kwao. Kwa sababu mama huyo hakuwa akijiweza kimaisha.

Katika maisha yake, Sudi alikuwa na marafiki wengi wa kike lakini hakuwahi kujiingiza katika masuala ya kuvunjiana utu wala heshima. Kwa mfano, baada ya starehe zao alimpeleka Chia alikoishi kabla ya kufululiza kwenda kwao.

3. **(Uhusiano wa Kijamii)**

Uhalisi wa mambo ni kwamba, Sudi hakuwa mwanawe Bimkubwa kwa damu. Mamake alikuwa Bi. Kudura. Kudura alimtupa mtoto huyo akiwa mchanga. Huenda Bi. Kudura wakati huo alikuwa bado kijana na hakujua matokeo ya tendo lake hilo la unyama. Hata hivyo, kati ya Sudi na Bi. Kudura kulikuwa na mvuto Fulani. Hii ndiyo sababu kila mara mama huyo alikuwa akimpungia au kumsimamisha Sudi barabarani.

Kutokana na mvuto huo, Sudi aliamua bila kujua kumwajiri Bi kudura pale kwao. Jambo hilo halikuwa limepangwa lakini ilitokana na miujiza ya Mwenyezi Mungu. Katika shughuli zake pale nyumbani, Bimkubwa alikuwa akimtupia jicho na kumfananisha na Sudi. Katika mazungumzo yao pale nyumbani, Bimkubwa anatambua kuwa Bi. Kudura ndiye mama yake Sudi. Katika hali hiyo Sudi anapatanishwa kisadfa na mamaye mzazi.

Bi. Kudura na mwanawe walikuwa wamepoteleana kwa miaka mingi lakini damu hiyo haikupotea. Hii ndiyo sababy ya Sudi kuelezwa kuwa; “damu hiyo haikupotea. Hii ndiyo sababu ya Sudi kuelezwa kuwa; “damu yake imetoka ilikotoka na kukufuata” (uk.118)

4. **Majuto**

Kulingana na mawazo ya mtunzi ni kwamba mtu huweza kutenda mambo ambayo si mazuri labda kwa kufahamu au kutofahamu lakini baadaye huweza kujuta vitendo vyake.

Kwa mfano, Bimkubwa alitenda wema kwa kumwokoa Sudi alipokuwa ametupwa jalalani. Hata hivyo, hakuwahi kumwambia "mwanawe" ukweli kuhusu vile alivyomwokota. Kila mara Sudi amekuwa akiulizia kuhusu baba yake lakini jambo hilo lilikuwa limesitiriwa. Hata hivyo, Bimkubwa hakutaka kusema ukweli kwa kuhofu kuwa Sudi angekosa furaha.

Ilipobainika kuwa ukweli mchungu kwa kusema kuwa, "Naomba unisamehe sana kwa kukudanganya nilivyokudanganya na kuichezea akili yako..." (Uk. 118).

Kadhalika, Bi. Kudura alitenda unyama kwa kumtupa mtoto wake. Jambo hilo lilikuwa lilisumbua akili yake. Hakujua ni kwa nini alitenda unyama huo.

Katika dhiki alizozipata anasema kuwa, "Asaa angekuwa mtoto wa heri na ngome imara kwangu, lakini wapi!" (uk. 117). Hata hivyo, anajuta kuwa, "Laiti si huo ujana amabao sikuona faida yake hata saa zaidi ya hasara si ajabu na mie leo ningekuwa naye mwanangu" (Uk.117). haya ni baadhi ya majuto yaliyowafika baadhi ya wahusika katika hadithi hii. Kadhalika, Sudi ambaye alikuwa na mwelekeo mzuri, hasa katika masomo na maisha yake yaliyonyooka, hakuwahi kujuta maishani mwake.

Maudhui mengine ambayo yanaweza kujadiliwa darasani ni kama vile:

5. **Changamoto za ujana**. (Zingatia Bi. Kudura na maisha yake ya hapo awali)
Bi. Kudura alipenda sana anasa za ujanani na kwa kushiriki ngono, aliweza kupata ujauzito nap engine kwa kuhofia shtuma kutoka kwa wazazi na wanajamii,anaamua kumtupa mtoto.

6. **Starehe na anasa**.Sudi alivyokuwa akifumuika na vijana wenzake akiwa Ulaya na hasa katika karamu ya Easter Get Together na pia huko Tea Breeze.
   Vilevile,leohii tunaona jinsi anavyoandamana na mpenziwe ili waende wakajivinjari.
7. **Umuhimu wa elimu**. Zingatia jinsi Sudi alivyojitahidi hadi kupata shahada ya udaktari wa sheria. Vilevile,tunaona kuwa ni kutokana na elimu hii ndiposa ana uwezo wa kuwakimu anaowakimu.
8. **Ukatili**. Bi.Kudura alimtupa mwanawe kwenya jalala lataka bila huruma. Motto huyu huenda angeliwa na mbwa au hata kufa kutokana na baridi kali.

Ujenzi wa Usawiri wa Wahusika

Mhusika mkuu ni Sudi Abdalla; Bi. Mkubwa na Bi. Kudura ni wahusika wadogo lakini mhimu katika hadithi.

Sudi Abdalla

Ni mhusika mkuu katika hadithi hii. Hakujua asili yake. Hapo awali hakumfahamu mama yake mzazi. Kwa sababu mama yake alimtupa jalalani akiwa mchanga. Baba yake hakufahamy kabisa. Mawazo kuhusu baba yake yalimsumbua mno na kila mara alimuuliza "mama" yake. Hata hivyo, hakutka kumhuzunisha "mama" yake. Kwa sababu "mama" yake alimweleza mkasa uliomtokea na "baba" yake Abdalla.

Sifa

a) Alikuwa ***mwenye heshima*** sio tu kwa "mama" kwa mama yake bali pia kwa mtumishi wao wa nyumbani. Kwa mfano, hakuwahi kumtuma "hata kijiko cha kukoroge sukari" (Uk.115). aliwazungumzia akina mama hao kwa adabu. Elimu aliyokuwa nayo haikutia kiburi, kwa sababy alimheshimu "mama" na mtumishi wao. Heshima yake pia ilimfanya kusimamisha gari lake alipopungiwa mkono na mama aliyekuwa akisimama kando ya barabarani kuelekea kwao. Alimhurumia mno "mama" yake na kumtulisa alipoonyesha dalili za kuhuzunika.

b) Kila mara alipenda kuwa ***nadhifu*** na "mtanashati" (uk.111). Ingawa alikuwa na umbo la kupendeza hakujita kiburi wala kuwadharau wenziwe.

c) ***Ni msomi.*** Katika masomo yake alitia bidii hadi akapata, "shahada ya juu ya udaktari wa sheria" (Uk. 111) yaani uzamifu. Wakati wa mapumziko alipenda kujumuika na vijana wenzake lakini aliitunza heshima yake. Kwa mfano, baada ya sherehe alimpeleka "Chia wake nyumbani kwao" (Uk.113)

d) Alikuwa na **msimamo dhabiti**, maisha ya ughaibuni hayakumfanya kujiingiza katika maswala ambayo yangempotezea mwelekeo katika masomo yake. Kila jambo alilizingatia kwa udadisi na uzingativu. Kwa mfano, alipokuwa kielea kwao wakati wa usiku, "alijikaza na kutazama vizuri na akaita kumbukizi na sura zikamjia" (Uk.113). na baada ya hapo ndipo alipogundua huyo hakuwa kizuu cha makaburini bali, "bibi mmoja ambaye alikwishamzoea" (Uk.113). alipotoa maagizo, aliyabainisha vizuri bila utata. Kwa mfano, mtumishi wao alipofika kwao kwa mara ya kwanza alimwambia "mama" yake kuwa, "sasa wewe utakuwa ukimpa chakula, mahali pa kuweka ubavu na kumdiriki nguo usizozitaka" (Uk.114). Huyu ni miongoni mwa wahusika wema katika hadithi hii.

e) **Mkarimu na mwingi wa utu**. Bimkubwa alimwokoa Sudi alipokuwa ametupwa kwenye pipa la taka. Kadhalika,Sudi na "mamaye" walikuwa na mahusiano mazuri pale nyumbani. Kila mara walipozungumza heshima ilidumishwa. Hakuna hata mara moja

ambapo walikoseana heshima. Mama huyo alipokuwa akihuzunika alitulizwa moyo na Sudi kwa kauli kama vile, “Usilie mama” (Uk.111).

Kadhalika, kudura mfanyikazi wa nyumbani alikaribishwa kwa mapokezi mazuri. Bimkubwa alizungumza naye vizuri na malikuwa na mahusiano murua. Kudura alipokuwa kwao Sudi alipewa “chakula na pahali pa kuweka ubavu” (Uk.114). nguo pia alipata.

Kutokana na heshima aliyokuwa nayo Sudi, hakuwahi, “kumtuma hata kijiko cha kukorogea sukari” (Uk.115). hii ni kwa sababu Bi. Kudura alikuwa hirimu la “mama” yake.

Utu wa Sudi ulimfanya kutompita Kudura kila alipomsimamisha barabarani karibu na mavani.

Sudi aliweza kumsaidia Kudura kupata ajira pale kwao. Kwa sababu mama huyo hakuwa akijiweza kimaisha.

Katika maisha yake, Sudi alikuwa na marafiki wengi wa kike lakini hakuwahi kujiingiza katika masuala ya kuvunjiana utu wala heshima. Kwa mfano, baada ya starehe zao alimpeleka Chia alikoishi kabla ya kufululiza kwenda kwao.

Mpenda anasa na starehe- Sudi alivyokuwa akifumuika na vijana wenzake akiwa Ulaya na hasa katika karamu ya Easter Get Together na pia huko Tea Breeze. Vilevile,leohii tunaona jinsi anavyoandamana na mpenziwe ili waende wakajivinjari.

Umuhimu wa Mhusika Sudi Abdalla

i) Ni kielezo cha vijana ambao licha ya elimu yao ya kiwango cha juu wana utu na heshima kwa wazazi na jamii kwa jumla.
ii) Mwandishi amemtumia kuonyesha mvumilivu hula mbivu.
iii) Mwandishi amemtumia kuonyesha athari za kisaikolojia zinazoletwa na kutofahamu asili ya mtu.

Bimkubwa

Ni mama mlezi wa Sudi. Katika maisha yake hakujaliwa kupata mtoto. Kwa sababu hiyo alifurahi mno alipompata mtoto aliyetupwa jalalani.

Sifa

a) Alikuwa ***mwenye utu na huruma*****.** Hii ndiyo sababu ya kumlea Sudi kama mtoto wake.

b) ***Alithamini elimu*** na alikuwa mwenye maono katika maisha. Kwa mfano, zaidi ya kumlea Sudi, alimpeleka shule hadi na shahada ya juu ya udaktari wa sheria akahitimu na kupata kazi nzuri.
c) ***Ni msiri***. Ingawa alimsaidia Sudi, alimficha uzawa wake, kwa sababu alichelea kumkosesha furaha mwana huyo.
d) Ni mtu ambaye ***ana heshima*** kwa "mwana" wake na kwa Bi. Kudura. Alikuwa mwenye mlahaka mzuri nao, aliwaheshimu. Kwa mfano, anamweleza Sudi kuhusu mgeni aliyefika kwao kwamba, "Sudi, umemwona mgeni? (Uk.113) na kuitikiwa "Ndiyo mama, nimemwona" (uk.113).
e) ***Mwenye bidii*** alijitahidi katika maisha. Katika juhudi zake aliweza kuwa na nyumba nzuri aliyomrithisha, Sudi tangu alipokuwa mdogo" (Uk.118).
f) ***Msamehevu*.** Endapo alikosea alipenda kuomba msamaha kama inavyoelezwa kuwa, "Naomba unisamehe sana kwa kukudanganya nilikokudanganya" (Uk.118). Hata hivyo, kudanganya huko kulikuwa na nia nzuri. Kwa sababu, hakumjua baba na mama yake. Kadhalika, angemwambia kuwa Sudi ni mwana wa kuokotwa labda mtoto huyo angejidharau.

Umuhimu wa Bi. Mkubwa

i) Kielelezo cha wanajamii wenye utu ambao wanaweza kulea wana wasiojua asili yao, kama wana wao wakuzaa.
ii) Mwandishi amemtumia kuonyesha kuwa kuna nyakati ambapo ukweli unaweza kubanwa hadi wakati mwafaka wa kuubanisha.

Bi. Kudura

Ni mamake Sudi. Jambo hili hakulifahamu mwanzoni, kwa sababu
Alipomzaa mwanawe alimtupa jalalani na kuokotwa na mhisani. Akiwa kijana hakuwa mwadilifu.

Sifa

a) ***Mwenye kujirudi*.** Alitenda tendo hili la kumtupa mwanawe akiwa bado kijana. Hata hivyo, jambo hilo lilimhuzunisha sana katika maisha yake ya baadaye na akaandamwa na majuto.
b) ***Mwenye subira.*** Alipenda kusimama pembezoni mwa barabara pale mavani labda alikuwa akitaka aweze kupata mhisani wa kumwajiri. Sudi alimfahamu kutokana na mazungumzo yao mazuri.
c) ***Alipenda kujenga mlahaka mzuri***na wale aliozungumza nao. Kwa mfano, nyumbani kwao Sudi, alikuwa na masikilizano mengi na Bimkubwa.

d) ***Ni msema kweli*** kulingana na maelezo aliyoyatoa kuhusu tendo la kumtupa mwanawe jalalani. Alifanya kazi yake nyumbani kwao Sudi kwa kujitolea hata akapendwa mno.
e) ***Hakupenda makuu/Mnyeynyekevu-*** bora amepata riziki kwa haki.

Umuhimu wa Bi. Kudura

i) Kupitia kwake mwandishi anaonyesha kuwa matendo afanyayo mtu huweza kumwathiri na kuwa change cha majuto tele.

ii) Kielezo cha wanajamii ambao wakikosa, wanajuta na kuomba msamaha kisha wakasamehewa.

Wahusika wengine ambao wanaweza kujadiliwa darasani ni kama:

- Waridi.
- Radhia au Chia
- Abdalla bin Sudi. Huyu ni mhusika wa 'kidhahania' ambaye Bi. Mkubwa alidai ndiye Sudi.

Mbinu za Lugha

1. **Misemo**

Katika hadithi hii misemo iliyotumiwa ni mingi. Mifano hiyo ni kama vile:

a) Jina si mboje. (Uk.110)
b) Hazikuzaa matunda (Uk.110).
c) Akamtia jichoni (Uk.110).
d) Mbivu au mbichi (Uk.110).
e) Kufa kupona (Uk.110).
f) Siku zile za asali (Uk.110).
g) Babu kubwa (Uk.112).
h) Usingizi mzito (Uk.111).
i) Suti aliyoivaa ilimtoa akatoka (Uk.111)
j) Bonge la karamu (Uk.111).
k) Wametia ngosho (Uk.112).
l) Siku ya siku (Uk.112)
m) Alipiga gari lake moto (UK.112).
n) Kitoto cha umbo na sura (UK.112).
o) Akapiga mkwaju (Uk.113).
p) Hawajijui hawajitambui (Uk.113).
q) Midomo yao haifungiki (Uk.113).
r) Najimwagia maji (Uk.114).
s) Kufungua kinywa (Uk.114).
t) Kinywa wazi (Uk.115)

u) Apige moyo konde (Uk.116).
v) Mambo yako uwanjani (Uk.116)

2. **Tashihisi**

Kupitia kwa kauli ya tashihisi, ujumbe huhuishwa na kupewa sifa za viumbe vyenye uhai. Mifano hiyo ni kama vile:

a) Jitihada za kuulizia habari za baba yake hazikuzaa matunda (Uk.110).
b) Msiba mzito ukanigeukia (uk.111).
c) Taa zake za rangi mbalimbali zilizowaka kwa mtindo wa kukonyeza (Uk.112).
d) Machupa ya soda, bia, mvinyo na vinywaji... vikaonekana kushiriki kikamilifu katika dhifa ile (Uk.112).
e) ...liliotambaa na kuanza kuyabungunya masafa ...(Uk.112)
f) Vinywa visivyopenda taabu na mashaka (Uk.113).
g) Gari likatimka kuelekea tibirinzi (Uk.113).
h) Hata walevi walikuwa wakizingumza na chapa zao za pombe (Uk.113).
i) Akaita kumbukizi na sura zikamjia. (Uk.113).
j) Siku hazikusimama, zilikutwa zikachwa na maisha yakapungua (Uk.114)
k) Bahati katu haiji mara mbili (Uk.116).
l) Maneno hayo yalikuwa msumeno butu unaokeketa kwa maumivu makali (uk.118).
m) Damu yake imetoka ilitoka na kukufuata (Uk.118).
n) Maneno ... kwa yule mtumishi wao, yalimchoma kwa woga na wasiwasi (Uk.1180.

3. **Tashibihi**

Mbinu hii ya lugha humithilisha jambo au kitu na kitu au jambo jingine ili kukoleza wazo linalowasilishwa.

a) Sudi alikuwa akimuona baba yake sawa na mhusika wa hadithini au wa mchezo wa kuigiza (Uk.110).
b) Sudi hutukia japo si kama maji ya mtungi (Uk.110).
c) Maneno yake daima yalikuwa hay ohayo kama kuyahifadhi kipembeni mwa pango lake la moyo (Uk.110).
d) ...apapa machozi – ikawa kama mtu aliyefundua tandu akafundika nge! (Uk.111).
e) Mlikuwa na mseto wa furaha na huzuni kama ilivyokuwa ada ya maisha (Uk. 113).
f) Sudi alimtazama mama yake usoni kama kutaka kuhakikisha kwamba hachukizwi na maneno amuambiayo (uk.114).
g) ...lakini ulimi wangu mzito kama nanga. (Uk.115).
h) Kiroho kikimdunda na kupumua kama aliyeona jinni (Uk.115).
i) ...naye akakuwa kama mgomba, mnazi unachelewa. (Uk.115).

4. **Chuku**

Matumizi ya chuku yametumiwa katika hadithi hii ili kupanua zaidi ukawaida wa kitu au jambo. Mifano hiyo ni kama vile:

a) ...angalau kwa pupa ya nukta kama dakika haipatikani. (Uk.110).
b) Hakuna aliyekosa kujua zama hizo habari za mapenzi yetu. Nani? Tokea kifaranga hadi kuku! (Uk.110).
c) Sudi alikuwa akiwaniwa na kila mwanamke (/Uk. 112).
d) Basi watu walicheza mpaka wakacheza tena, wakafurahi na wapenzi wao hata wakasahau matatizo yao. (Uk.112)
e) Sudi na Rodhia walipita wote wakatazama na kufurahi palipofurahisha, wakahuzunika palipohuzunisha (Uk.113).
f) Midomo yao haifumbiki kwa kushindiliwa vitu! (Uk.113).
g) Wenye mate nao waliemewa. Hao ni ahali makoo! Walikuwa hawajui waende kwa nani wamuache nani ... (Uk.113).

5. **Maswali ya Balagha**

Haya ni maswali ambayo yameibuliwa kwa makusudi ili kuchochea utafakari na usaili wa mawazo yanayowasilishwa katikahadithi hii.

a) Aghalabu maswali hayo huwa na kiashiria cha kiulizi, kwa mfano, nani vile? (Uk.110).
b) Bila shaka ungemuita asingekataa kuitikia na kwa nini akatae? (Uk.110).
c) Mara ngapi Sudi amekuwa akimuuliza mama yake habari za baba yake? (Uk.110).
d) Kwa nini mama yake amfiche? (UK.110).
e) Kwa nini asiniambie ukweli? (Uk.110).
f) Furaha yangu itoke wapi tena? (Uk. 111).
g) Kumbe ni kweli wanavyoniita? (uk. 111).
h) Sasa alichokumbuka ni nini hasa – suti yake au Waridi? (Uk.112).
i) Je, Bimkubwa aidanganye nafsi yake kwa kuendelea kuficha ukweli au apige moyo konde afichue siri? (Uk.116).
j) Inakuwaje mtu akiambiwa kwamba yeye ni kiumbe wa kuokotwa? (Uk.118).
k) Hakuaje? Husimamaje? (Uk.118).
l) Huendaje katika dunia ya masuto na nazaa? (Uk.118).
m) Atafanyaje Sudi? (Uk.118).

6. **Jazanda**

Jazanda katika hadithi imetumiwa ili kuifanya hadhira kuweza kutafakari zaidi na kupatanisha ujumbe unaowasilishwa na tajriba zao. Mifano hiyo ni kama vile:

a) Mtoto wa kutupwa au kuokotwa (Uk.110).
b) Tangu hapo nikawa mkiwa tena wa maisha (Uk.111).
c) ...ndiyo nusura yake (Uk.111).
d) Kutia mkono na kupapasa katika kiza hicho cha kumbukizi (Uk. 112).
e) Nadhani isingekuwa ua hilo hata Sudi asingekumbuka Suti ile aliyoivaa. (Uk.112).
f) Alikuwa akiwaniwa na kila mwanamke. (Uk.112).
g) ...kutaka ithibati ya maneno yake. (Uk.114).
h) Bimkubwa anamhukumu kwa dhambi aliyotenda lakini wapi? (Uk. 116).
i) Sauti ya shetani ikimtonesha ... angekuwa na yai lake mwenyewe (Uk.116).
j) Dawa ya sahau, dawa ya dunia (Uk. 118).
k) Msumeno butu unaokeketa kwa maumivu makali (Uk.118).
l) Damu yake (Uk.119).
m) Mtu huweza kupoteza mizizi na matawi yake nab ado akabaki mtu. (Uk.119).

7. **Methali**

Katika hadithi hii methali zimetumika kufumba busara ya mawazo yanayowasilishwa. Methali hizo ni kama vile:

a) Mungu akikupa kilema hukupa na mwendo (Uk.110).
b) Yaliyopita huwa yamepita (Uk.112).
c) Kuvyaa kupona (Uk.114).
d) Ukitaka kujua hasara za kukosa mtoto tazama faida ya mwenye mtoto. (Uk.115).

8. Nguvu za maji na mawe, mlimwengu ni mwanawe (Uk.116).
9. Bahati katu haiji mara mbili (Uk.116).
10. Damu iliyo daima nzito kuliko maji (Uk.119).

Kupitia kwa utafakari wa methali hizo zilizotumiwa, ujumbe unaowasilishwa hupata nguvu.

9. **Mbinu Rejeshi (au Viona Nyuma)**

Kupitia kwa mbinu hii matukio ya awali yanajenga dibaji au muktadha wa kuelewa matukio ambayo yanawasilishwa katika hadithi. Mifano hiyo ni kama vile:

a) Ndiyo ... maana hata mwenyewe hakuwa na uhakika wa jina lake. (Uk.110).
b) Usinikumbushe baba yako! Unaniumiza kwli mwanangu lakini hujui. (uk.110).

c) Karamu yenyewe ilifanyika katika ukumbi wa hoteli moja kubwa iliyoitwa Royal Palm (Uk.112)
d) Waridi, mwanamke mmoja aliyekuja kutoka Gaboron, Afrika Kusini, alijua kumpendeza Sudi (Uk.112).
e) Bimkubwa bibi yangu nikwambie nini mhisani wangu/ mimi niliwahi kuzaa mtoto mzuri wa kiume, lakini kwa kuwa nilimzaa nje ya ndoa na siku hizo ujana unanenda ... (uk. 115).
f) Sudi mwanangu mimi sikusuudika kuzaa mtoto katika umri wangu wote ingawa nilikuwa na hamu kubwa ya kupata mtoto (Uk.118).
Kupitia kwa kauli hizo, matukio muhimo yaliyopitika katika maisha ya wahusika yamebainisha.

10. **Majazi**

Wahusika wamepewa sifa zinazolingana na tabia au zifa zao. Kwa mfano;
a) Sudi ana bahati aliokuplewajaani. Alilelewa vizuri. Anampata mamake hatimaye.
b) Waridi – msichana mrembo sana.
c) Radhia – mpenziwe Sudi, anamridhisha.
d) Bi. Kudura – amekuwa akitegena Kudura na hatimaye anapumzika.

11. **Sadfa**

Mbinu hii imetumika kuibulia jambo geni katika hadithi hii. Mifano hiyo ni kama vile:
a) Bimkubwa alipomwokota Sudi jalalani.
b) Sudi kumwona Bi. Kudura kule mavani na kumwalika aje kwao.
c) Bi. Kudura kuajiriwa katika nyumba ya mama mlezi wa mwanawe Sudi.
d) Sudi kufahamu asili au mizizi ya uzawa wake.

12. **Kinaya**

Kinaya katika hadithi hii kimetumiwa kujenga kinyume cha uhalisi wa matarajio yaliyopo, mifano hiyo ni kama vile:
a) Sudi, ambaye ni mwanawe Bi. Kudura, anamrejelea mamake kama mtumishi. Hata hivyo, uhalisi huo ulikuwa haujabainika.
b) Bimkubwa kurejelewa na Sudi kama mama ilihali ni mama mlezi.

13. **Taharuki**

Mbinu hii imetumiwa makusudi kuchochea ilihamu ya hadhira katika usomaji wa hadithi hii. Mifano hiyo inayojenga taharuki ni kama vile:
a) Bimkubwa anavyoelezea kuhusu kukimbiwa na mumewe, Abdalla Sudi (Uk.111)

b) Njia nzuri alikuwa akiwaza mambo tele (Uk.113).
c) Bi. Kudura kumjibu Sudi kuwa “Naam mwanangu” (uk. 114), ingawa kwa wakati uliopo Sudi alifahamu kuwa huyo alikuwa mtumishi wao.
d) Bimkubwa alivyomtilizia jicho mtumishi wake mpaka akaona haya (Uk.114).
e) Ati huyu Sudi ni mtoto wako wa kumzaa (Uk.1150.
f) Bimkubwa kutambua kuwa mtumishi wao ni mamake Sudi kutokana na maelezo yaliyotolewa (Kur. 115-116).
g) Nataka nikwambie “...mtoto huyo ni wewe Sudi” (Uk.118).

14. **Taswira**

Katika hadithi hii taswira ni picha ya mawazo inayoundiwa hadhira. Mifano hiyo ni kama vile:
a) Jinsi sherehe moja ya ‘Easther Get together ilivyohudhuriwa na Sudi huko Ulaya (Uk.112).
b) Tafrija iliyohudhuriwa huko Tea Breeze. (Uk.113).
c) Bimkubwa walivyokuwa wakiishi na “mwanawe” Sudi.
d) Mahusiano baina ya Bimkubwa, Bi. Kudura na Sudi.
e) Bimkubwa alivyoandaa kikao cha kufumbua ukweli kuwa Sudi na mwanawe Bi. Kudura.

Maneno ya Kiingereza/ Kuchanganya Ndimi.
a) Handsome (Uk.111).
b) Easter Get Together (UK.112)
c) Tea Breese.

Maneno hayo yametumika kufafanulia muktadha wa ughaibuni.

15. **Utohozi**

Katika hadithi hii kuna maneno ya Kiingereza ambayo yameendelezwa kwa Kiswahili. Maneno hayo ni kama vile:
a) Suti (Uk.112) (suit)
b) Treni (Uk.113) (train)
c) Madisko (Uk.113) (disco)
d) Densi (Uk.113) (dance)
e) Samba (samba)
f) Matarumbeta (Uk.113) (trumpet)
g) Bosi (Uk.114) (boss)
h) Hepi (Uk. 116) (happy)

16. **Visehemu katika Uwasilishaji wa Hadithi**

Hadithi hii imegawanywa katika sehemu tatu muhimu:
Sehemu ya 1: Imezingatia udibaji, yaani namna Bimkubwa alivyompata Sudi na maisha yao kwa ujumla.

Sehemu ya 2: kupitia, binu rejeshi, imezingatia maisha ya Sudi yalivyokuwa huko Ulaya na jinsi alivyokuwa akiendesha maisha yake kwa wakati uliopo. Anapatana na Bi. Kudura na kumwalika kwao.

Sehemu ya 3: Imezingatia baada ya majilio ya Bi. Kudura kama mtumishi kwao Sudi na ufumbuzi wa uzawa na Sudi.

Hadithi Ndani ya Hadithi
Ndani ya hadithi hii kuna kadhia mbili zinazowasilishwa na wahusika wawili: Bimkubwa na Bi. Kudura. Aidha, kuna hadithi inayowasilishwa na mtunzi.

SHAKA YA MAMBO

FAROUK TOPAN

Ufaafu wa Anwani.

Anwani inaafikiana na hadithi hii kutokana na sababu zifuatazo:

b)

Dhamira ya Mtunzi

Mtunzi wa hadithi hii alidhamiria kuelezea kuhusu athari ya maisha ya kisasa hasa za jiji kubwa kama vile Nairobi. Baadhi ya vijana wamekuwa na mwelekeo kwamba mji wa Nairobi ni pepo bila ya kufahamu kuwa kuna matatizo pia. Aidha, baadhi yao kama vile kamata ni wajanja. Wanataka kuwatumia wasichana ovyo na wakipata mahala pa kulaghai, wanachukua fursa hiyo mara moja.

Maudhui

Maudhui makuu ni kama vile anasa na starehe, suala la pesa, kazi na utu.

1. **Anasa na Starehe**

   Katika hadithi hii, mtunzi ameeleza kuhusu starehe na anasa mbalimbali ambazo huwazuzua vijana. Kwa mfano, Esther anamuuliza Grace "kwani miadi yako ni saa ngapi?" (Uk.70).
   Kadhalika, kamata anaulizwa "Ehhe, mpenzi tuambie leo unakwenda wapi?" (Uk.71). katika mpango hiyo ya starehe, Kamata alisema kukwa "amekuja kuchukua gari la mwenzake ambaye anamwazima kwa usiku huo" (Uk.71). katika muktadha huu, vijana hawa huzunguka kwa anasa zilizopo katika mji badala ya kufikiria mambo ya muhimu kama vile kujitahidi kuboresha hali zao za maisha. Grace kwa upande wake anasema kuwa ana, "miadi muhimu sana Nairobi" (Uk.70). swali ni kwamba, miadi hiyo ni muhimu kweli au ni mipango ya starehe? Zaidi ya hayo Grace yu tayari kulipia kutokuwepo kwake kazini kama anavyosema, "nitakulipa zaidi ya malipo yako ya kawaida dada yangu" (Uk.70). kwa upande mwingine Esther haonekani kuridhishwa kukaa pale kwa mzee Mwinyi kwa sababu, "amekuja Nairobi kujifunza usekretari na kujipa uhuru. Yote mawili hana" (Uk. 69). Kwa heshima, mzee Mwinyi alimchukulia Esther kama mtoto wake, na alimtaka asimezwe na anasa za kimji lakini hayo yalichukuliwa vingine kuwa ni mbinu za kumdhibiti au kumkosesha Esther starehe. Katika majumba ya starehe, fedha ndizo huwekwa ,mbele na vijana wamekuwa wakizifuja katika harakati za kujitafutia anasa. Uhuru ambao Esther anaoutaka si uhuru bali ni kujihangaisha na kuhidhikisha.

2. **Suala la Pesa**

   Katika muktadaha wa wahusika waliosawiriwa katika hadithi hii, fedha ndio ufunguo wa hawaa na maisha ya dunia. Jambo hilo limedhihirishwa kupitia kwa Esther kuwa, "angalau atakuwa bado ameshika kazi ya kumpatia pesa za kuendeshea maisha.

Pesa! Kila kitu pesa. Mtu hawezi kupiga hatua duniani bila ya pesa" (Uk.69). kulingana na Esther, fedha ndizo huweza kumpa mtu uhuru wa kuhitawala na anasa. Kuna uwezekano kuwa Grace na Esther walimpenda Kamata kutokana na fedha alizonazo. Kwa mfano, imeelezwa kuwa Kamata alipotokea: "alikuwa amevaa suti ya buluu, shati la manjano hafifi na tai ya kijivujivu. Uso wake uling'ara kwa furaha" (Uk.71). hapa inabainika kuwa Kamati alitumia fedha zake katika mapambo na pia kuwa kivutio cha wasichana kama vile Grace na Esther. Hata hivyo, anasa zinapomtawala mtu hujenga ulaghai wa aina Fulani. Kwa mfano, Kamata anapoziona fedha zilizosahauliwa na mteja pale mkahawani anamwambia Esther kuwa , "Nipe mimi ntampelekea" (uk.73). Grace naye aliongezea "Ndiyo, mpe Kamata" (Uk.73). fedha hizo ziliwafurahisha mno akina Kamata na Grace, kwa sababu waliona furaha yao itaongezeka. Vijana ambao hawana magari hujaribu kuazima ili wajionyeshe kuwa wao pia wanajiweza. Kwa mfano, Kamata ameazima "gari la mwenzake" (Uk.71) ili walitumie kuenda kwa sehemu za starehe. Kulingana na mwandishi, hayo ni maisha ys kidhahania.

3. **Kazi**

Kulingana na mtunzi, kazi ni msingi wa uhai kwa kila mja. Hata hivyo, kuna baadhi ya vijana ambao wana mielekeo ya kuchagua kazi badala ya kufahamu kuwa kazi ni kazi. Kwa mfano, Esther anasema kuwa, "amekuja Nairobi kujifunza usekretari na kujipa uhuru" (uk.69). kwake aliona kuwa kazi ya kiofisi ndiyo yenye hadhi zaidi ya kutoa huduma yake katika mkahawa. Zaidi ya hayo baadhi ya vijana kama vile Grace, starehe na anasa ndizo zinazopewa kipaumbele. Kwa mfano, Grace, amesema kuwa "ana miadi muhimu sana Nairobi" (Uk.70). kinachobainika ni kuwa hana lolote la kufanya huko jijini Nairobi isipokuwa kuandamana na Kamata katika starehe. Anakwepa kufanya kazi. Kadhalika, Esther anapokuwa kazini huwa mawazo yake yamo katika kumfikiria Kamata. Katika hali ya kumwaza Kamata anasema, 'sijui amekuja kazini leo'? (uk.70). mfano mzuri wa mtu aliyefanya kazi kwa dhati ni baba yake Esther ambaye muda wake mwingi aliutumia katika kilimo, kama inavyoelezwa kuwa, "tangu siku hizo hakuwa akija Nairobi ila mara moja tu; hasa kwa shughuli zake za ukulima. Tena alikuja asubuhi na kurudi jioni" (Uk.69). kadhalika, mzee huyo alikuwa akifanya kazi huko Nairobi na baada ya kustaafu alirudi kwao Machakos. Katika kazi kama ilivyodhihirishwa kupitia kwa Esther, ni muhimu kuzingatia uaminifu. Kwa mfano, Esther alipogundua kuwa mteja wao alisahau kitita cha fedha alimkimbilia ili amkabidhi lakini hila hizo zinanyakuliwa na Kamata na Grace wake.

4. **Utu**

Suala la utu ni miongoni mwa maudhui muhimu yaliyowasilishwa katika hadithi hii. Mzee Mwinyi alionyesha utu kwa Esther, kwa sababu, Esther alikuwa ni msichana mdogo ambaye analingana na watoto wake. Kwa hivyo, alimchukua kama mtoto wake. Hili limedhihirishwa kuwa "mzee Mwinyi na familia yake wanamtunza kama mtoto wao" (Uk.69). Utu huo ulifasiriwa vingine na Esther kwamba, "yeye hana uhuru wa kutoka nje kutembea Nairobi atakavyo na saa atakazo" (uk.69). Esther alionyeshea utu wakati mteja wao pale mkahawani aliposahau bunda la noti. Hela hizo zilimhangaisha na alitaka kumrejeshea mwenyewe lakini hakumpata. Kinyume na Esther, Kamata na Grace wametawaliwa na ubinafsi. Huenda hilo ni jambo ambalo wamelizoea. Mfano mwingine wa utu ni pale ambapo abiria mmoja katika matatu alipompa kiti Esther. Jambo hilo lilimshangaza Esther. Kwa sababu, Kamata ambaye alikuwa wanafahamiana hajawahi kumtendea hisani kama hiyo.

5. **Uhusiano Ya Kimapenzi**

Mtunzi hana imani na baadhi ya mahusiano ya kimapenzi yanayoanzishwa na vijana. Kwa mfano, Kamata amekuwa akizinguka na wasichana tofauti tofauti. Leo ni Esther, kesho ni Grace. Mapenzi ya Kamata kwa Esther yalikuwa ya kupotezeana muda tu. Kwa mfano, Esther alikuwa akifikiri kuwa amempata mtu wa dhati lakini ilikuwa kinyume cha uhalisi huo. Huenda Kamata alikasirika wakati ambapo miadi yake ilivunjwa na Esther. Kwa hivyo, alikuwa hampitii, kazini kama ilivyokuwa hapo awali. Kadhalika, Kamata alikuwa na mpenzi mwingine pale kazini kwao Grace; hayo ni mahusiano ambayo hayakujengwa katika misingi ya utu. Katika misingi hii, mtunzi anawataka vijana kuwa waangalifu wakati wa kuanzisha mahusiano kama hayo.

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

1. **Esther**

Ni msichana aliyetoka huko Machakos. Alipofika jijini Nairobi, alipata makazi kwa mzee mwinyi huko Makadara.

Kwa bahati nzuri, alipata ajira katika mkahawa mmoja katika uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta.

Sifa

a) *Ana malengo mahsusi maishani*. Lengo lake lilikuwa kujifunza taaluma ya usekretari na pia kujipatia uhuru kutokana na udhibiti wa wazazi wake.
b) *Alikuwa mwenye utu na heshima*. Kwa mfano, anapopewa nafasi ya kuketi katika matatu anashukuru kwa "ahsante" (Uk.68). Hisani hiyo hakuitarajia

kutoka kwa vijana kama vile Kamata. Katika akili yake alielewa kuwa siku moja ataiacha kazi hiyo ya kuhudumu katika mkahawa lakini hiyo ilikuwa siri yake. Kwa mfano, imeelezwa kuwa, “Esther hakumwambia kitu waajiri wake wala hakuwakumbusha kwa sababu naye alikuwa na mpango wake” (Uk.69).

c) *Mpenda anasa***.** Ingawa alielewa vizuri na wazazi wake alizuzuliwa kwa anasa na starehe za kimjia alizowahi kuzisikia. Kwa hivyo, alipotua jijini Nairobi alianza kujiingiza katika masuala hayo.
d) *Mjinga.*Hakuwa mweledi katika janja za kimji.
e) *Mpenda amani.*Ni mtu ambaye hapendi kuzua zogo. Kwa mfano, anapogundua kuwa Kamata na Grace wana uhusiano Fulani anawaachia nafasi hiyo.
f) *Ni mwaminifu na mwenye utu.*Yeye ni tofauti na baadhi ya vijana ambao si waaminifu. Kwa mfano, mteja ambaye alisahau bunda la noti pale mkahawani alitaka kumpelekea hela zake. Kadhalika, hela hizo anawaonyesha akina Grace na Kamata ambao wanafanya hila na kuzichukua. Kutokana na umakini wake, ingawa hakufuatilizia angegundua kuwa hela hizo zimetekwa. Kwake fedha si utu bali maelewano mema. Kwa mfano, Grace anamwambia kuwa, “ Nitakulipa zaidi ya malipo yako kwa kawaida” (Uk.70). Esther anajibu kuwa, “Aa, sitaki kulipwa mimi” (Uk.70). kauli hizo aliyoitoa Esther ilielekezwa kwa utu alionao kinyume na mwelekeo wa vijana wenzake. Anapoambiwa na Grace kuwa ampe Kamata bunde hilo la noti, hasiti kufanya hivyo. Anatii mara moja labda kwa sababu Grace ni mkubwa wake pale kazini.

Umuhimu wa Esther

i) Ni kielelezo cha vijana waishio mjini ambao bado hawajashawishika kujitoma wazima wazima kwenye anasa na starehe za mji.

2. **Kamata**

Ni mvulana ambaye anafanya kazi ya ukaguzi wa mizigo katika uwanja wa ndege wa Jomo Kenyata.

a) *Yeye hupenda starehe na anasa* hasa kwa kuandamana na wasichana. Grace na Esther waliweza kunaswa katika mitego yake.
b) *Ni ndumakuwili.* Si mtu ambaye ana mapenzi ya dhati kwa wasichana aliojuana nao. Kwa mfano, Esther alichukulia kuwa kamata ni wake kumbe Grace alikuwa wake pia.

c) *Mlaghai.* Inapoelezwa kuwa bunda la noti limesahauliwa pale mkahawani analichukua kwa ulaghai huku akifahamisha kuwa, “nipe mimi ntampelekea” (Uk.73).
d) *Mwenye kujishaua.* Hupenda kujionyesha kwa wasichana na kujitia ukubwa. Kwa mfano, anapoenda kumchukua Grace anasema kuwa, “amekuja kuchukua gari la mwenzake ambaye anamwazima” (Uk.71). vile vile, “alikuwa amevaa suti ya buluu ... tai ya kijivu” (uk.71) ili awavutie akina Grace na Esther.
e) *Mwenye papara.* Ni mtu ambaye hana subira. Kwa mfano, Esther alipokosa kuandamana naye disko, anakasirishwa mno. Kwa ujumla yeye ni mpenda anasa na laghai katika maisha yake.

Umuhimu wa Kamata

i) Ni kielelezo cha vijana ambao wanaongozwa na starehe kiasi cha kukosa utu.
ii) mwandishi anamtumia kuonyesha jinsi pesa huwafanya watu kulaghai.

3. **Grace**

Anafanya kazi pamoja na Esther katika mkahawa wa uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta. Walijuana na Esther.

Sifa

a) *Ni mpenda starehe na anasa.* Huandamana na Kamata katika majumba ya starehe. Kwa mfano, anasema “ana miadi muhimu sana Nairobi” (uk.70).
b) *Mwenye ubinafsi na kujipenda.* Hupenda mipango yake ifanyike kwa haraka na kwa kutumia pesa. Hiyo ndiyo sababu ya kumwambia Esther kuwa, “N’takulipa zaidi ya malipo yako ya kawaida” (Uk.70) ili aweze kuenda katika starehe.
c) *Ana tamaa.* Alipoliona bunda la noti zimesahauliwa, mara moja tamaa inamwingia kutaka kuzichukua akiwa na Kamata.
d) *Ni Msiri.* Anapenda kufanya mambo kwa siri. Kwa mfano, hataki kuelezea iwapo ana mpenzi.
e) *Yeye ni mwongo.* Hatimizi ahadi zake. Aliahidi kumshikilia zamu Esther, jambo ambalo hajalifanya hata mara moja.

Umuhimu wa Grace

a) Kama ilivyo na Kamata ni kielelezo cha vijana wanaojiingiza katika starehe pasi na kujali kazi zao.
b) Pia anawakilisha watu walaghai. Yeye ndiye alimshinikiza Esther ampatie Kamata lile bunda la noti.

Mbinu za Lugha

Mwandishi amewasilisha ujumbe wake kwa lugha inayomtia kwa kutumia mbinu kama vile tashihisi, semi, tashibihi na maswali ya balagha.

1. **Tashihisi**

a) Usiku uliopita ulimbembeleza na kumlaza usingizi mtamu (Uk.68).
b) Gari loikaingia barabara kuu. Likawa sasa linasimama kila mara ...(Uk.68).
c) Kujisukuma garini macho yangali yamejaa usingizi (Uk.69).

2. **Maswali ya Balagha**

Maswali haya yamebainisha hali ya matatizo aliyo nayo Esther kuhusu maswala mbalimbali na kudokeza migogoro ya nafsi inayomtawala

a) Ugeni au usasa gani? (Uk.68).
b) Ndiyo kazi anayo, lakini kazi gani hii ya kuamka alfajiri siku sita kwa wiki na kujisukuma garini macho yangali yamejaa usingizi? (Uk.69).
c) Anaumwa? Au hamjali tena kwa sababu amekataa kuenda naye disko? (Uk.70).
d) Kila akipiga simu huwa ama haipokewi au hukatika. Au hukatwa? (uk.71).

3. **Semi**

a) Kijana mwenzake katuna fahari ya kidume (uk.68).
b) Kupiga taipu.
c) Naye Kamata akapiga mbio kuelekea mlango nambari 4 (uk.73).

4. **Tashibihi**

a) Wanamtunza kama mtoto wao (Uk.69).

Mtindo katika Uwasilishaji

1. **Viona Vyuma (Mbinu rejeshi)**
   a) Esther anaeleza jinsi baba yake alifanya kazi Nairobi miaka ya 70 (Uk. 69).
   b) Alihama na kurudi kwao Machakos baada ya Mzee Kenyatta kufariki mwaka 1978 (Uk.69).
   c) Nairobi aliyokuwa akijua hasa ni hiyo ya zamani (Uk.69).

2. **Utohozi**

Maneno yaliyotoholewa

a) Taipu (uk.68) (type)
b) Vilabu (club)
c) Blauzi (Uk.69) (Blouse)
d) Disko (Disco)
e) Usekretari (Uk.69) (secretary)
f) Buluu (Uk.71) (blue)
g) Kanta (Uk.70) (counter)
h) Keki (Uk.71) (cake)
i) Marekani (Uk.71) (America)
j) Nambari (Uk.73) (Number)
k) Lifti (Uk.73) (lift)
l) Shati (Uk.71) (shirt)
m) Tai (uk.71) (tie)
n) Dola (uk. 71) (dollar)

KANDA LA USUFI

Rhoda Nyaga

Dhamira ya Mtunzi

Dhamira ya mtunzi ilikuwa ni kuelezea kuhusu wanafunzi wanafunzi wanapo kuwa shuleni. Kwamba, shule za mabweni haziwezi katu kuwafanya wanafunzi wasiweze kuwa na uhusiano wa kimapenzi katu kuwafanya wanafunzi wasiweze kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Kadhalika, vijana hujiingiza katika maswala ya kimapenzi bila kuwa na mwelekeo unaofaa. Wasichana wanapopata mimba huongezea mzigo kwa wazazo wao. Baadhi ya wazazi huwalaumu walimu wana wao wanapokwenda kombo. Mtunzi anawataka vijana kujiepusha na kuanzisha uhusiano wa kimapenzi wakiwa shuleni, kwa vile hawamudu, kukabiliana na matokeo ya mahusiano hayo.

Maudhui

Kuna maudhui makuu yafuatayo.

1. **Elimu kwa Vijana**

   Swala la elimu limetiliwa mkazo katika hadithi hii. Kwa hivyo, wazazi wana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata elimu; si kwa wavulana tu, pia kwa wasichana. Hii ndiyo sababu wazazi wa Sela wakampeleka katika shule ya bweni ya Askofu Timotheo, kadhalika Masazu kupelekwa kwa shule ya Lenga Juu. Walimu katika shule huhakikisha kuwa wanafunzi wanafundishwa huku wazazi wakifahamu kuwa wana wao wanapata mafunzo hayo muhimu. Licha ya ulinzi mkali, baadhi ya wanafunzi hujiingiza katika mapenzi ya faragha. Jambo hili hutatiza masomo ya wanafunzi. Walimu kama wazazi huwapa wanafunzi mielekeo ya kimaadili. Hii ndiyo sababu ya kuelezwa kuwa baada ya Sela kugundua kuwa amepata mimba: hakuwa na utulivu masomoni (Uk. 61). Tukio hilo pia lilimwathiri mno Masazu, “kwamba naye hakuweza kutunza makini yeke masomoni” (uk..61). Vijana wanapojiingiza katika mapenzi shuleni huwasababishia wazazi machungu.Baadhi yao husema kuwa,”Mwalimu, nina swali moja ambalo nigetaka unijibu. Je, kwa nini huwaletea watoto shuleni? Mzee Butali aliuliza kwa sauti iliyojaa uchungu’’ (Uk. 62). Ni kweli kwamba walimu wana jumuku la kuhakikisha kkuwa wanafunzi wanalelewa vizuri lakini wakati mwingine inakuwa vigumu kutokana na njama za wanafunzi. Kadhalika, suala la elimu ya watoto linajumuisha juhudi za walimu na wazazi.

2. **Mapenzi ya Wazazi kwa watoto**
   Wazazi huwa na mapenzi makubwa kwa watoto wao. Hata kama mtoto atakuwa ametenda tendo ambalo linamharibia maisha bado kuna uhakika wa kuwepo kwa mapenzi ya dhati: kwa mfano Sela anapopata mimba akiwa shuleni na kupoteza

mwelekeo bado, mama yake anamchukulia kuwa, “huyu ni mtoto wetu, sio maradhi” (Uk.63). ingawa hilo ni tatizo ambalo linawakera, wazazi wanaendelea kuonyesha mapenzi kwa mtoto wao. Mamake Sela pia anasaidia katika kumlea na kumsaidia mjukuu wake licha ya ufukara uliowaathiri. Kwa mfano, “ilibidi matambara yatumiwe kukivisha kitoto” (Uk.63). ingawa mzee Butali alikuwa na uchungu mkubwa kutokana na ujauzito wa Sela, alihakikisha kuwa mtoto wao anaendelea na masomo. Kadhalika Sela na Masazu wangependa kumlea mtoto wao hata ingawa maisha yao yalikuwa magumu. Kwa mfano inaelezwa kuwa, “Sela alihisi kuwa hakukamilika sawasawa bila mwana wao ambaye alimwona kama kiungo muhimu katika mahusiano yao” (Uk.64). kwa hivyo, yeye na Masazy wanapanga mipango ya siri ya kwenda kumchukua mtoto wao. Mzee Butali anapokuwa na hasira kuhusu kitendo cha bintiye anafahamishwa na wanakijiji kuwa “maji yakimwagika hayazoleki. Huruma zinamwingia na hasira zikapungua” (Uk.63). kwa hivyo mtoto huweza kutenda visivyo lakini bado ni mtoto. Kadhalika, mama na Seoa wanapokaripiwa na mzee Butali wote wanaondoka pale nyumbani. Kitendo cha mama kuandamana na bintiye ni kutokana na kuwa, “uchungu wa mzazi aujuaye ni mzazi” (Uk.63).

3. **Ujirani Wema**

   Katika kijiji mzee Butali na mkewe walimoishi, watu wamekuwa wakiishi kwa ushirika na amani. Kila jambo baya linapotokea au kunapohitajika ielekezi, wanajamii huzingatia busara ya kusuluhisha. Kwa mfano, ujauzito wa Sela unazua zogo na kutosikilizana katika jamii ya mzee Butali. Mzee Butali anashindwa kuvumilia aibu aliyoipata na mama na bintiye wanafukuzwa pale nyumbani. Hapo mwanzo mzee Butali hakutaka bintiye kurudi shule. Hayo ni kutokana na hasira iliyomfanya asizingatie utu. Kwa mfano, mzee Butali, mama na binti yake, “mtwae kilicho chenu mniondokee” (Uk.63). mama naye anamsihi kuwa, “Baba Sela, nani kasema kuwa huu ni msimba wangu? Tutautatua pamoja” (Uk.63). hayo ni baadhi ya matatizo ambayo yalishamini katika familia yam zee Butali kutokana na ujirani mwema, wazee wenye busara waliingia kati na kusuluhisha zogo hilo. Katika maongezi hayo, “mzee anaelewa kuwa maji yakimwagika hayazoleki. Huruma zinamwingia na hasira zinapungua” (Uk.63). kadhalika, mzee Butali anafahamu kuwa mtoto ni mtoto na hasira hazifai kati ka malezi ya mtoto. Katika mkutasha huo wa ujirani mwema, familia yam zee Butali inarejea hali ya kawaida.

4. **Kazi ni Kazi**

   Mtunzi wa hadithi hii ameleza kuwa kazi ni muhimu na lazima binadamu afanye kazi. Kwa mfano masazu alipomaliza masomo yake alitafuta kazi mjini Dafina ili aweze kujisaidia. Naye Sela alipomaliza masomo, “alihamia mjini Dafina kuenda kutafuta kazi” (Uk.63). kazi aliyoipata ilikuwa, “kibarua cha kuvuna mkonge”

(Uk.63). mshahara aliupata ulikuwa mdogo lakini aliweza kujikodishia nyumba na chakula kukipata. Kulingana na mtunzi ni kwamba hakuna haja ya kubagua kazi mradi mtu anapata mahitaji yake ya muhimu. Hata hivyo, endapo kuna maswala ya ulezi wa mtoto, kati yao au mmoja wao anaweza kubaki nyumbani ili kutekeleza wajibu huo muhimu. Uzohali ni jambo ambalo linakemewa na mtunzi kwamba, Sela "hakupenda kukaa nyumbani tu bila chochote cha kufanya" (uk.64). kwa upande wa Masazu alijitahidi mchana kutwa akiwa kazini, kwani alifahamu kuwa bila kazi familia yake itatatizika.

Maudhui mengine ambayo yanaweza kujadiliwa darasani ni kama:

a) *Ugumu wa maisha ya mjini*. (Zingatia maisha ya Masazu na Sela huko mjini Dafina)
b) *Idhini ya ndoa kutoka kwa wazazi.* (Zingatia namna Sela na Masazu wanapoamua kuishi pamoja kabla ya ndoa kuidhinishwa na wazazi).
c) *Taasubi ya kiume.* (Zingatia namna mzee Butali anavyomfukuza mkewe na binti yake pale nyumbani)
d) *Hasira.* (Zingatia kauli mbalimbali anazozitoa mzee Butali kwa mkewe na mwanawe. Maswali ambayo mzee Butali anamuliza mkuu wa shule ya Bweni ya Askofu Timotheo).
e) Wajibu wa walimu katika jamii.

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

Wahusika wakuu ni Masazu na Sela. Wengine kama Bi. Margaret. Mzee Butali, mamake Sela na Rozina ni wahusika wadogo.

Chris Masazu

Ni kijana ambaye ni mwanafunzi katika shule wa wavulana ya Lenga Juu.

Sifa

a) *Ni mjaja*. Kwa mfano, "alimrai Sela. Sela aliingia barabara katika mtego" (Uk.60). ingawa hiki ni kitendo ambacho hufanywa na vijana wengi, yeye hakustahili kuzingatia hilo.
b) *Mwenye shukrani*. Kwa mfano anapokabidhiwa mkoba na hatimaye Kadogo anasema, "ahsante" (Uk.66).
c) *Mwoga na asiye dhabiti wa msimamo*. Hata hivyo, hana uamuzi wa kibinafsi hasa inapozingatiwa kwamba, Sela anapomtaka waende kumchukua mtoto wao kwa siri anakubali bila ya kusaili.
d) *Anajali maslai ya awapendao*. Anapoandamana na Sela kwenda na kutoka mtoto wao, yeye ndiye anayeongoza njia usiku. Anahimili mvua na baridi kali. Aidha Sela na Kadogo wanapozama majini, anaruka kujaribu kuwaokoa.

e) *Mwenye bidii*. Alikuwa ni kijana ambaye alijitahidi katika masomo yake hadi akamaliza kidato cha nne.
f) *Alikuwa na maono mazuri*. Katika maisha kwani alijitafutia kazi na kuifanya kwa moyo wake wote. Alipomaliza masomo yake, alitaka kuwa na maisha mema. Hiyo ndiyo sababu ya kuamua kuanza maisha akiwa na Sela.
g) *Ni kigeugeu*. Kwa vile mwanzoni hamuungi mkono, Sela anapopata taarifa ya mimba kutoka kwake.

Umuhimu wa Masazu

i) Ni kielelezo cha vijana wanaojiingiza katika mapenzi bila kutafakari matokeo yake.
ii) Anatumiwa kuonyesha kuwa watu hubadilika, Hamuungi mkono Sela anapopata mimba lakini baadaye anaonekana kuwajali yeye na mtoto wao Kadogo.
iii) Mwandishi anamtumia kushauri vijana kuwajibika baada ya vitendo vyao.

Sifa

a) *Ana moyo wa utu na huruma*. Kwa mfano, Masazu alipomweleza kuwa ni mgonjwa anaamua kumsaidia kumpeleka kwa matibabu katika kliniki ya shule.
b) *Ni mwepesi kudanganywa*. Hakujua ujanja au njama za mwanafunzi mwenzake. Hakuwa mtu wa kutathmini mambo, kwa sababu anapokea barua ya kimahaba akiwa bado mwanafunzi. Alikubali kuendeleza uhusiano huo wa siri. Hata hivyo anapomjulisha Masazu kuhusu hali yake ya ujauzito na kuambiwa kuwa, “kwa nini hakujikinga” (Uk.62) anahuzunika huku akilia.
c) *Sela alikuwa jasiri*. Kwa sababu alipanga mipango ya siri ya kwenda kumchukua mtoto wao. Alifahamu kuwa mipango hiyo isingeweza kukubaliwa na wazazi wake. Hata hivyo, anafanya hivyo kwa msaada wa Masazu. Isitoshe baada ya kumaliza shule hakutaka kuwa mzigo kwa wazazi wake ambao walikuwa masikini. (Uk.63).
d) Alikuwa mwenye maamuzi mwafaka kwa vile aliamua kumlea mwanawe.

Umuhimu wa Sela

i) Ni kielelezo cha wasichana ambao hata baada ya ‘kuteleza’ hujikakamua, wakapiga moyo konde na kuanza upya. Alisema baada ya kujifungua Kadogo.

ii) Anawakilisha mzazi mwenye mapenzi kama mwanaye kwa vile anafanya juu chini kumpata mwanawe amlee.
iii) Anatumiwa kuonyesha umuhimu wa kusamehe.

Bi. Margaret

Alikuwa mwalimu mkuu katika shule ya Bweni ya Askofu Timotheo.

Sifa

Ni mwenye ushauri. Aliwashauri wanafunzi kutozingatia maswala ambayo yangeyaathiri masomo yao. Kadhalika, alitumia nasaha katika kuzungumza na kuwaelekeza wazazi wakati wa kutafuta suluhisho la tatizo. Kwa mfano aliwaelezea wazazi wa Sela kwamba, "ingawa sisi hufanya tuwezayo wanetu, mara nyingi tabia zao hutupiga chenga" (Uk.62). Anafahamu kuwa ni jukumu lake kuwaelekeza wazazi kuhusu elimu ya watoto wao. Kwa hivyo, alitaka Sela aendelee na masomo yake katika shule nyingine. Hii haikumaanisha kuwa anamfukuza Sela bali alitaka ajiunge na aendeleze masomo yake katika mazingira ambayo hatafanyiwa kebehi au stihizai na wanafunzi wengine wanaomjua.

Umuhimu wa Bi. Margaret

i) Ametumiwa kubainisha dhima ya walimu, si kufunza pekee bali kushauri wanafunzi na hata wazazi wao. Hawapaswi kuwahukumu wanafunzi wanapojipata matatani.

Mzee Butali

Ni babake Sela

Sifa

a) *Mwenye maneno*. Alikuwa na maono mazuri kuhusu bintiye. Hii ndiyo sababu ya kumpeleka Sela katika shule ambayo angepata elimu na maadili meme katika maisha.
b) *Mwepesi wa hasira*. Ni mtu ambaye ana hasira kubwa. Kwa mfano, alipopata habari kuhusu ujauzito wa bintiye anakasirishwa mno na tukio hilo. Anapendwa na ki...
c) *Ni mpenda kulaumu*. Hupenda kueleza lawama kwa wengine. Anapoelezwa na mwalimu mkuu kuhusu yaliyompata binti yao anauliza swali kwa uchungu kuwa, "mwalimu, nina swali moja ambalo ningetaka unijibu. Je, ni

kwa nini sisi huwaletea watoto shuleni" (Uk.62). anawafukuza mke na bintiye akisema kuwa, "mtwae kilicho chenu mniondokee" (Uk.63).

d) *Ana taasubi ya kiume*. Anawalaumu mkewe na bintiye na kuwafukuza nyumbani.
e) Kwa upande mwingine ni *mwenye busara* na anayetia maanani mawaidha anayopewa na wazee wenzake.

Umuhimu wa Mzee Butali

i) Ametumiwa kuonyesha kuwa wazazi japo watakasinshwa na wanawao, wanapaswa kuwasamehe na kuwasaidia kujenga upya msingi wa maisha yao.

Rozina

Ni halati yake Kadogo

Sifa

a) *Ni mtiifu*. Amekuwa akiwatii wazazi wake. Kwa mfano, anapoambiwa kuwa amlee kadogo kwa kuwa Sela anahitahi kuendelea na masomo, hapingi jambo hilo.
b) *Ni msiri*. Amekuwa akijiingiza katika mipango ya siri ili kumsaidia Sela ambaye ni dada yake. Swali hapa ni: Je, wazazi wake wakifahamu mipango hiyo atafanyaje/ hili hakuliwazia bali alifanya uamuzi wa haraka ili kumridhisha dada yake.

Umuhimu wa Rosina

i) Ni kielelezo cha udugu anajitolea kumlelea dadake mwana bila manung'umiko. Wahusika wengine ambao wanaweza kuzingatiwa ni kama vile:
- Sista
- Wazee wa kijiji
- Kadogo

Mbinu za lugha

1. **Tashibihi**
   a) Amekishikilia kichwa kana kwamba kingemdondoka (Uk.60).
   b) Aliitunza barua ile kama uhai (Uk. 61).
   c) Kikalegeza kiwiliwili chake mithili ya mbwa anayekabiliana na chatu macho kwa macho (Uk.61).
   d) Mwana wao ambaye alimuona kama kiungo muhimu katika mahusiano yao. (uk.64).

2. **Tashihisi**
    a) Mambo haya mawili yalielekea kuungana kuhujumu mkakati wao (uk.59).
    b) Matone ya mvua, yalikuwa yakipenya baina ya majani ya maembe, waliojikinga mvua, nayo yalitoa sehemy yayo ya hujuma. (uk.59).
    c) Mabasi ya shule ngeni yalikuwa yameanza kuingia huku yakiendelea kutapika wanafunzi wa kike na wa kiume (Uk.59).
    d) Moyo wake daima uliyeyushwa na huruma alipomwona mja akiteseka. (Uk.59).
    e) Barua ile ilifungua parafujo Fulani moyoni mwa Sela (Uk.61).
    f) ...akawa kama tiara inayopeperushwa na upepo...
    g) Kiapo hicho kiliiyeyusha nafsi ya Sela (Uk.61).
    h) Saa sita za usiku kiza kilikuwa kimeuma kila mahali (Uk.64).
    i) Kama chui aliyevizia windo lake... (Uk.60)

3. **Istiara**
    a) Kataa mkatao wa mbuzi achomekaye kwato ardhini anapovutwa (Uk.61). jinsi Masaru alivyokataa kabisa kurudi zahanatini kwa vile alijua hakuwa mgonjwa, alisingizia tu.
    b) Parafujo. (Uk.61) Athari ya mapenzi baina ya Sela na Masazi.
    c) Jahanamu (Uk.63) Jumbani mwake mzee Butali hamna amani.
    d) Msiba (Uk. 63) mimba yake Sela inalinganishwa na msiba.
    e) Kanda la usufi (Uk.62) jambo linalomlemea mmoja (Sela) lakini mwingine (Masasu) analiona jepesi.
    f) Usiku wa giza (Uk.62) lisilobainika wazi.

4. **Methali**
    a) Yajapo yapokee (Uk.62)
    b) Uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi (Uk.63)
    c) Maji yakimwagika hayazoleki (Uk.64).

5. **Misemo**
    a) Kutapika wanafunzi (Uk.62).
    b) Mkatao wa mbuzi achomekae kwato ardhini anapovutwa (Uk.61).
    c) Mzowa wa majuto (Uk.61).
    d) Kutunza makini yake masomoni (Uk.61).
    e) Kanda la usufi (Uk.62).
    f) Alitia udibaji (uk.62).
    g) Kulegeza msimamo (Uk.63).
    h) Ni mtoto wetu, si maradhi (Uk.63).

i) Pangu pakavu (Uk.63).
j) Makini ya rubani wa ndege (Uk.64).
k) Akimfuatia unyounyo (Uk.66).

Mtindo Katika Uwasilishaji

1. **Utohozi**
   a) Kliniki (Uk.60) (clinic).
   b) Daktari (Uk.60) (doctor).
   c) Glasi (Uk.60) (glass).
   d) Sista (Uk.60) (sister).
   e) Sampuli (Uk.61) (sample).
   f) Gesi (Uk.669) (gas).
   g) Sigara (Uk.66) (cigarette).

2. **Maswali ya Balagha /Maswali Butu**

   a) Huyu si mtoto wetu sisi wawili? (uk.59).
   b) Je, ni kwa nini sisi huwaletea watoto shuleni? (Uk.62).
   c) Baba Sela, nani kasema huyu ni msiba wangu? (Uk.63).
   d) Leo ndiyo mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka (Uk.63).
   e) Sikutumia hela zangu mimi katika elimu yake hadi nikaitwa pangu pakavu? (Uk.63).

3. **Mbinu Rejeshi**

   Mwandishi anatufahamisha jinsi uhusiano wa Sela na Masazu ulivyoanza na matokeo yake kupitia mbinu rejeshi.

4. **Taswira**
   a) Athari la hakikisho la mapensi alilotoa Masazu kwake Sela. ‘Kiapo ...kikalegeza kiwiliwili chake mithili ya mbwa anayekabiliana na chatu macho kwa macho (Uk.61).
   b) Hali ilivyokuwa afisini mwake mwalimu mkuu. ‘Wakati huu wote wazazi wa Sela walikuwa wamenyamaza. Mama yake Sela alikuwa akimtazama Bi. Margaret huku mzee Butali akiwa ameinama. (Uk.62).
   c) Hali ilivyokuwa walipojaribu kumwita Rozina awapishe Kadogo. “Rozina aligutuka na kunyanyuka kitandani taratibu, naye pia akaitika kwa mnong’ono” (Uk.64).

5. **Majazi**
    a) Mlimani (Uk.59).
    b) Lenga juu (UK.59).
    c) Sista (Uk.60).
    d) Kadogo (Uk.63).
6. **Taharuki**
    Mwandishi ametumia kauli na hali zinazochochea hamu ya wasomaji kutaka kujua yatakayojiri na yataotokeaje. Msomi anajiuliza maswali mengi na hana budi kusoma ili apate majibu.
    a) Kauli ya mwanzo hadithini inazua taharuki, 'Jambo ambalo Sela alikuwa akisubiri basi lilielekea kutimia.' Msomaji anatiwa hamu kusoma zaidi ili kujua jambo hili ni lipi na mbona Sela amelingojea kwa hamu.
    b) Je, Masazu anazifanyiaje dawa alizopewa? Zitamdhuru?
    c) Hatima ya uhusiano wao Masazu na Sela ni ipi?
    d) Hali itakuwaje Sela anapogunduliwa kuwa na mimba?
    e) Je, atafanikiwa kusoma tena kama Bi. Margaret alivyoshauri?
    f) Watafanikiwa hatimaye kukipata kitoto chao?
    g) Hadithi inaishia kwa taharuki. Sela na Kadogo wamezama majini. Je, Masazu atafanikiwa kuwanusuru?
7. **Nahau/Misemo**
    a) Huyu si mtoto wetu si wawili/ (Uk.59).
    b) Masazu alivibwakia vidonge vile na akavibana chini ya ulimi (Uk.60).
    c) Sela alimwandikia Masazu barua ya kujuza hali ya mambo (Uk.61).
    d) Ofisini, Bi. Margaret alitia dibaji (Uk.62).
    e) Boma la mzee Butali liligeuka jahanamu (Uk.63)
    f) Walipofika dirishani, Masazu alibisha taratibu juku akimwita halatiye Kadogo kwa mnong'ono (UK.64)

MASIKINI, BABU YANGU

Ken Walibora

Dhamira ya Mtunzi

Dhamira ya mtunzi ni kubainisha athari za ubaguzi wa kikabila, rangi na tamaduni hasi katika jamii. Katika muktadha huo, mtunzi amedhihirisha jamii ambayo haikubali utangamano wao makabila. Kwa sababu, kabila mojo huliona jingine kuwa hasidi. Matokeo ya uhalisi huo ni vifo na maangamizi ya watu. Kupitia kwa kalamu yake, mwandishi anapiga vita uhasama wa kikabila katika jamii.

Amedhihirisha pia kuwa japo wanajamii wanatengana na kuchukiana tu, makabila ni mawili tu, maskini na matajiri kaba babu Maende alivyobaini.

Maudhui

Maudhui makuu ni kama vile ubaguzi wa kikabila, umasikini na umuhimu wa kazi.

1. **Ubaguzi wa kikabila/ukabila**
   Katika hadithi hii msimulizi amebainisha kuwa ametokea magharibi mwanchi ya Sakati. Baadhi ya makabila yanayopatikana huko kama vile jamii ya Kitantele na Kisubu hayakuweza kujumuika pamoja.

   Suala la ndoa linalokata katika makabila hayo lilikuwa halikubaliwi katika tamaduni hizo. Msimulizi anasema kuwa 'ndoa kati ya Watantelel na makabila mengine nchini sakata ni nadra' (Uk.76). wawili hao walikutana katika kituo cha kibiashara.
   Kutokana na rangi na maumbile yao tofauti waliweza kujitofautisha na kuzua uhasama miongoni mwao.
   Msimulizi anasema kuwa hata wamindi 'kuoana na makabila mengine hutokea na tukizi kama kupatikana kwa wanasiasa mwadhilifu (Uk.76.). Kwa hivyo, baadhi ya wanajamii waliweza kuendeleza mahusiano hayo kwa siri kama inavyobainishwa kuwa, "palikuwa na muamana mzuri kati ya familia ya Maende na babu Tadeka" (Uk.76).

   jambo hilo la ubaguzi halitokei tu vijijini bali hata mjini. Kwa mfano, mitaa hujulikana kwa majina kama vile, "Daando, Summa na Kochokocho" (Uk.76). jamii mbalimbali hujitenga katika maeneo maalumu ya mitaa.

   Tukio baya la ubaguzi wa kikabila liliweza kushuhudiwa kule Kochokocho ambapo baba Maende aliyekuwa mweusi ilihali mjukuu wake alikuwa maji ya kunde. Kwa hivyo, alituhumiwa mwizi au mchawi ambapo alipigwa kitutu hadi akafariki.

   Ukabila unazua hisia za chuki baina ya watu wenye asili tofauti.
   - Wanakitantele na Wasubuni nadra kuoana ndiposa ndoa ya wazaziwe msimulizi ni 'mmoja kati ya maekfu'
   - Wamindi hawaoani na makabila mengine nchine – wamejitenga.
   - Watu wanajitenga na kuishi maeneo yao kutegemea asili yao. Ndiposa msimulizi na b abuye wanapofika eneo la Wantele, wanang'amua mara moja.
   - Kuna ukabila wa aina nyingine; unaiwagawa matajiri na masikini.

- Maskini wanaishi katika mazingira duni na wamejawa na dhiki.
- Wanaishi kinyama na ndiposa babu anapendekeza warudi makwao waishi maisha ya maana kidogo.
- Kwa mjibu wa babu Maende, hali hii ilizuka baada ya uhuni.
- Makazi yametengwa kulingana na kabila la mtu.
- Hata hivyo, si watu wote wanaoathiriwa na ukabila.
- Familia ya msimulizi; kuumeni na kuukeni haiathiriwi nao.
  Kuna matumaini.

2. **Umuhimu wa kazi**

Umuhimu wa kazi umesisitizwa katika hadithi hii. Kwa mfano, baba Maende alipenda shughuli yake ya ufugaji. Hata anapokuwa si buheri wa afya, huona muhali kuacha mifugo yake huko kijijini kwao. Kulingana na mwandishi, kazi ni kwa kila rika, iwe ni wazee au vijana. Kadhalika, kutokana na juhudi za kibinafsi, babake msimulizi alipandishwa "cheo hadi kiwango cha mrakibu wa polisi" (Uk.76). hata wakazi wa kitongoji duni cha Kochokocho, wamo katika kuututumua uchumi wao. Kwa mfano, imesemekana kuwa huko Kochokocho kulikuwa na "akina mama waliouza chapatti ...mandazi, maembe ...vitunguu ..., mapapai, macheriza na njugu ...karanga" (Uk.78). kwa hivyo, jamii za matabaka mbalimbali hushiriki kazi ingawa kwa viwango mbalimbali. Kutokana na kazi, babake msimulizi aliweza kuwasaidia wazazi wake huko vijijini. Kwa mfano, babu Maende alipokuwa muwele aliweza kushawishiwa kuja mjini Pilka ili kuweza kupata huduma nzuri ya matibabu.

3. **Umasikini Katika Jamii**

Katika hadithi hii, mtunzi amesawiri mazingira ya umasikini uliokithiri katika jamii. Kwa mfano, baadhi ya mitaa kama vile Daando, Summa na Kochokocho imesawiriwa katika hali ya kukatisha tamaa. Mitaa hiyo ilijulikana kwa kashfa yaani "madongoporomoka" (Uk.77).

ukata wa wanajamii, "uliwafunika, uliwafanya wawe kabila moja, kabila la wachochole" (Uk.77). kadhalika, babu Maende alitoa usijali wake kwa kutamka, " Salalaa! Mbona wasirudi kwao waishi maisha ya maana kidogo" (Uk.78). kwa walalahoi, maisha hayo ni ya kawaida isipokuwa kwa jicho la wanaojiweza.

Isitoshe, baadhi ya watu ambao hawajaushuhudia uhalisi huo huanza kusaili. Mwafaka wa uhuru wa Sakata kama ulileta manufaa yoyote kwa jamii. Kulingana na maelezo yanayotolewa, hali hizo zimesababishwa na, "... ukabila, ... ufisadi, hongo" (Uk.78). hii ni kwa sababu baadhi ya watu waliolekezwa kwa ubinafsi usiojali hali zawenzao katika jamii.

Kadhalika, mitaa hiyo ya mabanda kuwa imesahaulika katika mipango ya maendeleo katika nchi ya Sakata. Makazi hayo duni si ya kufaa, kama inavyobainishwa kwamba, "wauzaji wote walikuwa na kibarua cha "kuliwinga wimbi kubwa la nzi waliotaka kula uhondo"

Pia kulikuwa na uvundo usiostahimilika (Uk.78).

Upigaji Watu Kitutu/Ukatili

Katika hadithi hii, mtunzi hapendezwi na tabia za watu kuwapiga wenzao kitutu. Huu ni uhalifu na unapaswa kuthibitiwa kisheria. Kwa mfano, babu Maende hakuwa na hatia lakini anavamiwa bure na kuuawa hadharani. Kulingana na maelezo yanayotolewa, watu hao huwa wanachukua sheria mkononi mwao. Hasira zinawapanda, hawasiti wakachunguza iwapo tuhuma hizi ni za uhakika. Hasira hizo zinapaswa kuelekezwa kwa maridhiano ili suluhu iweze kupatikana. Labda halaiki hiyo ingesubiri na kuuliza huenda maafa hayo yaliyompata babu Maende yasingetokea. Kutokana na kutokufikiria, watu hao walimshuku babu hiyo kuwa mchawi au mwizi. Jambo ambalo linalaumiwa pia ni namna wanahabari wanavyojipatia sifa kutokana na matangazo yao yasiyozingatia uhalisi wa mambo. Hiyo ndiyo sababu ya kuelezwa kuwa, "mpiga picha wa runinga aliyenasa tanzila hiyo alitunukiwa tuzo kwa uhodari wake". Hayo ni mambo ambayo yameupotosha uhalisi wa mambo.

Maudhui mengine ambayo yanaweza kujadiliwa darasani ni kama vile:

4. **Uwajibikaji- B**abake msimulizi amewajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yake kama afisa wa polisi. Anafanya kazi kwa bidii na kuikimu familia yake.
   Yeye huwa anawajali wazazi wake na huwatembelea mara kwa mara.
   Babake msimulizi alimchukua babu Maende alipokuwa mgonjwa na kumpeleka hospitalini ili aweze kutibiwa.
   Babu maende kwa upande wake anapenda kuwatunza mifugo wake na kutokuwepo kwake nyumbani karibu na mifugo wake kunamfanya asiwe na utulivu.
5. **Utabaka** Mwandishi amedokeza kuwa katika mtaa wa kochokocho kuna walala hoi na walalahai. Babake msimulizi aliishi katika eneo la Sarani ghorofani na alikuwa ampakana na mitaa kama vile Summa, Dando na mitaa mingine duni.

Babu Maende ilibidi atolewe mashambani aje mjini ili aweze kupata matibabu, jambo linaloashiria kuwa kiwango cha maendeleo kinatofautiana.tunaarifiwa kuwa kule kijijini watu walitegemea miti shamba kwa matibabu.

6. **Elimu -T**unaarifiwa kuwa msimulizi alikuwa yuko katika darasa la tano. Pia na bayana kuwa makaazi ya msimulizi yalikuwa mkabala na shule ya wasichana ya Kabucheka.
7. **Suala la Ndoa.** Babake na mamake msimulizi walikuwa katika asasi ya ndoa. Hata hivyo, asasi ya ndoa kutoka makabila tofauti zinapingwa kwa dhati kutokana na uhasama wa kikabila. Ndoa kati ya wazazi wa msimulizi ilikuwa imara kwani wazazi walitembelea wazazi wao kutoka pande zote mbili.
8. **Tuhuma.** Babu Maende alivamiwa na watantele kwa tuhuma za kumwiba motto wa kitantele(Msimulizi) msimulizi alipojaribu kutoa ukweli wamambo, wanajamii wale walimtuhumu kuwa amemloga motto "wao".

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

1. **Msimulizi**

Kwa ambavyo matukio muhimu yameumuliwa kupitia kwake anakuwa ni mhusika mkuu katika hadithi hii. Ni suriama. Wazazi wake wametokana na jamii mbili. Mama yake ni Mtatele na baba yake ni Mkabucheka au Msubu. Kwa sura amemranda mno mamaye. Machoni pa watu alionekana kama Mtantele. Aliishi huko Pilka ambapo baba yake alikuwa akifanya kazi katika jeshi la polisi.

a) Ni mtu ambaye ***ana kumbukumbu nzuri***ya uzawa na usuli wake. Mambo muhimu ambayo yalimtokea akiwa mchanga bado nayakumbuka. Kwa mfano, anakumbuka namna babu yake Maende na babu Tadeka walivyokuwa wenye muamana mzuri. Kadhalika, anakumbuka vizuri namna babu Maende alivyowazuri kabla ya "kumfika yaliyomfika" (Uk.76).
b) ***Mwenye utangamano mwema*****.** Aliweza kuwa na mahusiano mazuri na mababy na nyanya zake wote. Hiyo ndiyo sababy ya kusema kuwa, "kwangu mimi vipindi vya ziara za mabibi na mababu vilikuwa ndivyo vyenye furaha zaidi maishani kwangu" (uk.76). Zaidi ya hayo furaha zaidi ilizidi wakati walipokuwa wakiwazuru wavyele hao wa pande mbili. Katika wakati wake aliweza kuzuru maeneo ya karibu na Sarani, yaani Kochokocho.
c) Yeye ni mwenye***msimamo imara*****.** Alipoona mambo yamechacha na hata kilio chake hakisikizwi alikabiliana kwa kumuuma mama mmjoja aliyemnyaka baby yake kofi. Ingawa alikuwa mdogo alitumia nguvu zake katika kumtetea babu yake

lakini haikuwezekana. Hiyo ndiyo sababu ya kubebwa hobelahobela hadi kwenye chumba asicho kijua.

d) Yeye alikuwa **mwenye ujasiri**. Hii ni kutokana na juhudi zake za kujaribu kumnusuru babu Maende kwa kumshambulia mama mmoja aliyemzaba babu kofi. Tunaarifiwa pia kuwa msimulizi amekuwa na ugumu wa kusimulia kilichotokea lakini anaamua kupiga moyokonde na kusimulia ingawa jambo hili linatonesha kidonda moyoni mwake.
e) **Muoga –** msimulizi alipoona kuwa mambo yameharibika, alimshikilia babu kwa hofu. Fauka ya hayo, alianza kupiga mayowe.
f) **Mvumilivu-**Msimulizi amekuwa akiishi na uchungu

Umuhimu wa Msimulizi

i) Ni kielelezo cha watoto wanaozaliwa katika ndoa mseto.
ii) Mwandishi ametumia kuonyesha jamii inapaswa kuwasetiri wana wao na kuwaepusha na visa vitakavyowaathiri daima.

2. **Babu Maende************

Ni babuye msimulizi. Alikuwa akiishi huko Kabucheka.

a) ***Mwenye jitahada na bidii*****.** Ni mzee ambaye alipenda sana kujitahidi katika shughuli zake za kila siku. Kwa mfano, “hakuwa anapenda kuiacha mifugo yake aliyoithamini mno” (Uk.76). Endapo mwanawe alitaka aende mjini Pilka kuwazuru, “alikuja kwa msukumo, sio kwa kuraiwa” (uk.76). hii inamaanisha kuwa alikuwa ni *mtambuzi* wa janja zilizoweza kutumiwa.

b) Kwa upande mwingine alikuwa mzee ***mwenye busara na hekima*****.** Kutokana na mawazo yake alitambua kuwa, nchi ya Sakata zaidi ya kuwa na makabila mengi, kuna makabila mawili tu: lile linalojiweza na like lisilojiweza. Kwa mtazamo wake mwelekeo huo haukuwa mwafaka. Alipozuru sehemu ambazo alizisikia kupitia kwa santuri, alishangaa zaidi kuhusu maisha ya mabanda. Kwa hivyo, aliona kuwa nakama hizo zinaweza kupata suluhu kwa watu hao kurudi kwao mashambani. Hii ndiyo sababu ya kusema kuwa, “Mbona wasirudi kwao waishi maisha ya maana kidogo” (Uk.78). Haoni ni kwa nini, watu wapate shida za maisha ilihali wana kwao ambapo hakuwezi kuwa jijini” (Uk.78). katika muktadha huo, imedhihirishwa kuwa mzee huyo anafahamu maswala ya kisiasa ambapo uhuru ulitarajiwa “utaleta manufaa kwa watu wote” (Uk.78). Kutokana na busara yake kuhusu siasa ya nchi ya Sakata, mwelekio unaotawala si mzuri. Kwa sababu mwafaka wa uhuru bado haujafikiwa.

c) ***Huyu ni mzalendo*** ambaye amezinduka na anayefahamu haki ya wanajamii. Hakusumbuliwa na mawazo ya ukabila uliokuwepo, kwa hivyo hakuwahi kuzungumzia kuhusu ndoa ya mwanawe iliyokuwa ukikata katika jamii mbili za Kitantelete na Kabucheka.

d) ***Alikuwa mcheshi***. Alipokuwa kwa mwanawe huko Pilka, familia nzima ilifurahia kuwepo kwake. Kwa sababum alikuwa kila mtu alifurahia "vicheko, tabasamu na ngano zizizokwisha na nyimbo alizoziimba ... (Uk.77). kwa hivyo, kifo chake kilikuwa pigo kubwa kwa wana na mjukuu wake. Alipokuwa ameenda kuzuru mtaa wa Kochokocho, aliweza kujitoa mhanga wamtoe roho lakini mjukuu wake asishuriwe, kwa mfano, alipoona vurumai limepamba moto alisema kuwa, "basi niueni lakini mjukuu wangu msimdhuru jamani" (Uk.81).

e) ***Mwenye Huruma.-*** Aliwahurumia wachochole wa kochokocho na kupelekea yeye kupendekeza kuwa watu wale wanafaa kurudi mashambani ili waweze kupata maisha bora.

Umuhimu wa Babu Maende.

i) Ni kielelezo cha wazee wenye bidii, busara na ambao ni watambuzi wa matatizo yanayoisibu jamii yao.
ii) Ni kielelezo cha wazazi wanaowapenda wana wao kiasi cha kujitoa kafara ilekuwanusuru.
iii) Mwandishi amemtumia kudhihirisha kuwa jamii haipaswi kutuhumu pasi na ushahidi. Baadhi ya wanapopigwa kitutu hadi kufa huwa watu wasio na hatia.

3. **Baba yake Msimulizi**

Ni mwanawe babu Maende.

a) ***Mwanamapinduzi/mwanamageuzi*.** Aliweza kuenda kinyume na matarajio ya utamaduni kuhusu ndoa zilizokata katika kabila la Kitantele na lile la kisubu. Kwa hivyo, hakutilia maanani tofauti hizo.
b) ***Ana mapenzi ya dhati***. Alimpenda mke wake na familia yake kwa ujumla. Kila alipokuwa na nafasi aliwazuru wavyele wake wa pande hizo mbili. Kadhalika, wazazi hao walikaribishwa katika makazi yake huko Pilka.
c) ***Alikuwa mkarimu/mwenye utu*.** Kila alipowazuru wazazi wake aliwapelekea zawadi. Ukarimu huo umedhihirishwa kupitia kwa msimulizi kuwa, "kila tulipokwenda Kabucheka na wazazi wangu wakizuru wazazi wao huku garini tumebeba zawadu tele kwa pande zote mbili". (Uk.76). pia alichukua hatua ya kumpeleka babake hospitalini alipokuwa mgonjwa.

d) ***Mwenye bidii na matumaini***. Alikuwa akiifanya kazi yake kwa bidii ndiyo sababu ya kupandishwa, “cheo hadi kiwango cha mrakibu wa polisi” (Uk.76).
e) ***Mpenda elimu na maarifa***. Kadhalika, alifahamu umuhimu wa elimu, kwa hivyo, alimpeleka mwanawe shuleni kama invyoelezwa na mwanawe kuwa, “nimekwisha hitimu shule ya chekechea, nimeingia shule ya msingi nimo katika darasa la tano” (Uk.77).
f) ***Mzalendo***- yeye alikuwa anafafanya kazi katika idara ya polisi. Aliasi taratibu za wanajamii kwa kukiuka kasumba za kikabila na kuoa mke wa kabila tofauti.

Umuhimu wa Babake Msimulizi

i) Kielelezo cha wanajamii ambao hupuliza tamaduni zinazowaganya watu katika msingi ya kikabila.
ii) Anawakilisha wana wanaowajali wazazi wao na pia kuwatunza ilivyo wana wao.
Wahusika wengine ambao wanaweza kuzingatiwa katika mijadala ya darasani ni kama vile:

- **Umma . –** Kupitia kwa umma, ukatili unadhihirika . fauka ya hayo, chuki miongoni mwa makabila inadhihirika.

Mbinu za lugha

1. **Methali**
   a) Kinolewacho hupata (Uk.75)
   Methali hii imetumiwa kuelezea namna msimulizi alivyokuwa akisukumwa ili kuwasilisha kadhia au uzawa wake ambao hakutaka kusimulia.
   b) Yaliyopita hupishwa (uk.75)
   Methali hii imetumiwa na msimulizi kuwa mambo ambayo yalimtendekea kwa sasa yako katika kumbukizi.

2. **Tashibihi**

   a) Ulimi wake ulikuwa mwepesi kusarifu kama wenyeji (Uk.75).
   b) Kuwaona na makabila mengine hutokea kwa tukizi kama kupatikana kwa mwanasiasa mwadilifu (Uk.76).
   c) Kumbukizi zangu kama jeraha mbaya la jana ... (uk.77).
   d) Mabati yaliyojifunika libasi ya kutu na vilango vilivyosimama vizingitini kama vibua vya mtama vilivyosubiri kuanguka (Uk.78).
   e) Vilango vilivyosimama vizingitini kama vibuu (uk.78)
   f) Vitoto vyembamba kama mimi na pua zilizochongoka kama yangu. (Uk.79).
   g) Akina mama waliozhabihiana na mama yangu walimtumbulia macho kama kwamba walikuwa wameona kioja (Uk.79).

h) Babu aliziambua nyayo na kupiga hatua mbele huku nimekamata mkono wake kama kwamba mustakabali wangu ulikuwa umening”inia kwenye mkono huo. (Uk.79).

Kauli hizo za kitashibihi zimetumiwa katika kutia nguvu ujumbe unaowasilishwa.

Kauli hizo za kitashibihi zimetumiwa katika kutika nguvu ujumbe unaowasilishwa.

3. **Takriri**
   a) Kuna usambamba au takrini ya kimuundo katika kauli ‘...akatangamana na watoto wa kisubu ...akaenda nao shuleni ... akateka maji ... akacheza nao ...akapiga kachombe ... akaimba nyimbo ...
   b) Jumamosi ile naikumbuka ...jumamosi iliyosimama kwenye kiwiliwili cha kumbukizi zangu ... (Uk.77)
   c) Marudio ya neno ‘duni’ katika Uk.78.

4. **Maswali ya Balagha (Maswali Butu)**
   a) Mtu atasemaje kwamba haya ninayoyasema ni zao la uzushi, ubunifu na jaribio la kusema vile nilivyotaka mambo yawe kuliko yalivyotumika hasa?
   b) Kulikoni jamani?
   c) Wacha! Wacha! Unawezaje kumpata mjukuu wa Kintantele? Ee? (Uk.79).

   Maswali hayo hayahitaji majibu ingawa hujenga usaili na utafakari katika akili ya msomaji.

5. **Tashihisi**

   a) Maradhi Fulani ya uzeeni yalikuwa yamemvamia (uk.76).
   b) Jumamosi inayosumama kwenye kiwiliwili cha kumbukizi zangu (Uk.7)
   c) Kumbukizi zangu kama jeraha baya la jana linalopwitpwita machungu (Uk.77).
   d) Ukata ulikuwa umewafumka, uliwafanya wawe kabila moja (Uk. 77)
   e) Mtaa wenye mabanda yaliyoinamiana na kuoneana imani (uk.78)

6. **Chuku**

   Hii ni mbinu ya kutilia maneno chumvi ili kusisitiza habari inayotolewa.
   a) Muhimu hapa ni kwamba ndoa yao ilikuwa ndoa moja katika maelfu. (Uk.76)
   b) Ukata ...uliwafanya wawe kabila moja, kabila la wachochole (Uk.77)

c) Kitanga change kidogo kimezama katika bahari ya kitanga chake kikubwa (Uk.78)
d) Vinginevyo, tufani ndogo au mvua kidogo yenye dhoruba inatosha kuyadondosha. Au labda yanaweza kuanguka kwa upepo wa mtu apigaye mbinja (Uk.78).
e) Kuta za mbuvu za mbwa, mabati yaliyojifunika libasi ya kutu na kuvu na vilango vilivyosimama vizingitini kama vibua ... (Uk.78).
f) Sakata haina makabila zaidi ya arubaini kama wengine wasemavyo; yapo makabila mawili tu ...(Uk.78)
g) Wauzaji wote walikuwa na kazi kubwa kuliwinga wimbi kubwa la nzi waliotaka kula uhondo (Uk.78).
h) Viwili vitatu ndivyo vilikuwa vyeusi kuliko masizi ya chungu cha bibi wa Kabucheka, mkewe babu Maende (Uk.79).
i) Mama mmoja mwenye umbo la kifaru (Uk.79).
j) Mbele kulikuwa hakwendeki tena (Uk.79).
k) Unyende wangu ulipotelea kwenye mzozo uliotokota nje ... (Uk.81).

7. **Misemo**

a) Kufunika pazia (Uk.75).
b) Kupiga moyo konde (Uk.75).
c) Nameza mate machungu (Uk.75).
d) Kuunga mkufu wa mambo (Uk.75).
e) Akapiga kachombe nao (uk.75).
f) Nywele zake za singa (Uk.75).
g) Kumfika yaliyomfika (Uk.76).
h) Alimshikia shokoa (Uk.76.
i) Kataakataa za babu ziligonga ukuta (Uk.76).
j) Amepata ahueni (Uk.77).
k) Mama alikuwa mja mzito (Uk.77).
l) Jua lilikuwa utosini (Uk.77).
m) Hana udole (Uk.77).
n) Nyakanyaka za watu (Uk.77).
o) Kuyaweka kwenye mizani (Uk.77).
p) Kukatisha tamaa (Uk.78.
q) Kula uhondo (uk.78).
r) Kunitumbulia macho (Uk.79).
s) Ghafla bin vuu (Uk.79).
t) Moto mmoja (Uk.78).
u) Walimpiga kitutu (Uk.78).

Matumizi ya misemo yametapakaa kote katika hadithi hii.

Misemo imetumiwa ili kutilia nguvu hoja zinazowalishwa.

8. **Tabaini**

Miongoni mwa kauli, mtunzi ametumia “si” ili kusisitiza zaidi hali inayowasilishwa. Mifano;

a) Si aghalabu watu wa kabila la mama yangu kuvuka mipaka ya kabila lao...(Uk.76).
b) Amechangamka si haba (Uk.77).
c) Si siahi, si mayowe, si miluzi ...(Uk.81).

Mbinu Za Uwasilishaji

1. **Mbinu Rejeshi/Kisengerenyuma**

Mifano ya matumizi ya mbinu rejeshi ni kama vile:

a) Katu sikutaka kukumbuka, au kuandika mambo yaliyojiri nilipokwenda kutembea na babu yangu mtaa wa Kochokocho (uk.75).
b) Mama yangu alivyokutana na baba ni siri na kutoa ni kuwakosea heshima wazazi wangu (Uk.75).

Mbinu ya viona nyuma au rejeshi imetumiwa kujenga dibaji ya muktadha ambamo matukio ya hadithi yamejengwa.

2. **Hadithi Ndani ya Hadithi**

Hii ni hadithi ya mtunzi. Hata hivyo katika uwasilishaji wake amesimulia kisa au matukio ambayo yamegubika siri ya uzawa au usuli wake.

3. **Majazi**

Majina yaliyotumiwa katika hadithi hii, yana maana maalum katika kubainisha kadhia inayowasilishwa. Kwa mfano:

a) *Baba Maende*. Ni babu yake msimulizi. Kupitia kwake, matukio ya kihistoria yanabainishwa. Pia anauawa na ‘kujiendea’ zake.
b) *Kisubu*. Neon linalotokana na kusibu yaani tukio ambalo limeathiri hali Fulani katika maisha ya mtu au jamii kwa ujumla.
c) Pilka. Imetumiwa kubainisha harakati za kijamii yaani shughuli zinazofanyika. Jijini pilka mnazo shughuli au pilkapilka nyingi.
d) Sakata. Limetumiwa kama jila la nchi na pia tukio la kashifa lililoshuhudiwa katika jamii. Kwa mfano, maafa yaliyomkuta babu Maende. Pia nchi hii inakumbwa na sakata nyingi alizozungumzia Babu Maende (Uk.78), mathalani; ukabila, ufisadi na hongo.

e) Kochokocho. Ni mseto wa mambo ambayo hawezi kuhesabiwa. Kwa hivyo, ni mambo mbalimbali yanayoendelea katika mtaa wa Kochokocho.

f) Madongo. Ni pahali ambapo hapana mpango wa kimazingira. Hii ni sehemu chafu ambayo haifai kuwa makazi ya watu. Kwa mfano mtaa wa Kochokocho unafahamika kama madongoporomoka.

4. **Jazanda**

a) Donda ...limejaa usaha na karaha na daima kunifanya kuhaha (Uk.75).
b) Tope jeusi ... (Uk.78).
c) Mabanda yaliyoinama na kuoneana imani (Uk.78).
d) Mbavu za mbwa (Uk.78).
e) Maisha ya wasakata (Uk.78).
f) Wauzaji wote walikuwa na kazi kubwa kuliwinga wimbi kubwa la nzi waliotaka kula uhondo (Uk.78).
g) Unyende wangu ulipotela kwenye mzozo uliotokota nje (Uk.81).

Mbinu ya jazanda imetumiwa ili kuifanya hadhira kujenga usaili na utafakari wa ujumbe unaowasilishwa.

5. **Taswira**

Hii ni mbinu ambayo huchangia maelezo yanayotolewa moja kwa moja na mwandishi. Kwa hivyo, hadhira hufunuliwa njia changizi katika uwasilishaji wa ujumbe. Kwa mfano:

a) Makazi ya familia ya akina msimulizi huko Pilka ambapo mtu huweza kuona mandhari ya Daando, Summa na Kochokocho (UK.76).
b) Kuwepo kwa babu Maende katika nyumba ya mwanawe kunatawaliwa na vicheko (Uk.77).
c) Uduni wa maisha katika mtaa wa Kochokocho ambapo watu huishi maisha ya kukatisha tamaa (Uk.78).
d) Zogo lililoanza na maafa yaliyompata babu Maende (Uk.79-80).

6. **Masimulizi**

Hadithi hii imewasilishwa kimasimulizi ambapo mtunzi ametumia nafsi ya kwanza. Mifano inayodhihirisha usimulizi ni kama vile: “ni”, “ali”, “unge”, “usiku...” “uli”, “tuli”, na kadhalika. Mtunzi anapotoa kauli ya mhusika mwingine hutumia kiakifishi cha kufungua na kufunga usemi. Hii ni mbinu ambayo hutumiwa mno katika utambaji wa hadithi na tamthilia.

SAMAKI WA NCHI ZA JOTO

Doreen Baingana

Dhamira ya Mtunzi

Dhamira ya mtunzi wa hadithi hii ilikuwa ni kudhihirisha namna wageni wanavyoishi maisha ya kikabila na kibepari kwa kulikamua jasho la wenyeji. Kutokana na utajiri walioupata, hujiingiza katika starehe na anasa. Baadhi ya wasichana wa kiafrika wamekuwa wakiwahusudu na kuunda ndoto ya kuolewa nao, pasi na kujua kuwa wanatumiwa tu. Wanafunzi hasa wa ngazi za juu hawafahamy kuwa wanajichimbia kaburi, kwa vile msingi wa maisha ya vijana umeelekezwa kwa anasa na starehe.

Maudhui

1. **Elimu**

   Suala la elimu limeangaziwa katika hadithi hii. Wataalamu mbalimbali waliweza kupata ujuzi huo kutoka kwa Chuo Kikuu cha Makerere. Chuo hicho kilikuwa ni mashuhuri hapa Afrika ya Mashariki na kilisifika ulimwenguni kote. Kutokana na sifa zake kilijulikana kama, "Havard ya Afrika" (Uk.11).

   Vijana kama vile, Miriam, Zac na Christine waliweza kupitia katika chuo hicho. Baadhi ya wataalamu kama vile maprofesa waliokuwa wakitoa huduma zao chuoni hapo mbeleni, waliweza kuuawa au kutorokea ughaibuni wakati wa enzi za utawala wa Idi Amin. Hivyo basi, hali inyosawiriwa ni ya kukatisha tamaa kuhusu hao waliopata elimu ya juu kwani waliweza tu kupata kazi za ujira duni. Kwa mfano, "Zac alipokuwa anamalizia shahada yake ya B. A. Katika somo la fasihi" (Uk.11). alifanya kazi kwenye kampuni ya Mr. Peter wakati wa likizo. Kadhalika, alipenda kuzungumza kama "Wamarekani weusi" (Uk.13). ingawa jamii ilifahamu kuwa elimu ni ufunguo wa maisha, wanafunzi walikuwa wakijihusisha na anasa na starehe zisizohusiana na masomo yao. Kwa mfano, Peter anamuuliza Christine, "Hivi, wewe ni mwanafunzi?" (Uk. 13). Kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, wanafunzi walianza kujiingiza katika ulevi, ukahaba na ulanguzi wa mihadarati miongoni mwa maovu mengine. Hata hivyo, baadhi ya vijana walijitahidi katika masomo yao na kuitunza heshima yao kama vile Dorothy, ambaye ni dada yake Christine.

   Elimu ni msingi wa maendeleo katika nchi na iwapo wataalamu hawapatikani kupitia asasi za elimu basi hata uchumi wa nchi huyumba. Hili limedhihirishwa kupitia kwa maprofesa "wengi waliokimbilia uhamishoni" (Uk.11) wakati wa utawala wa Idi Amin nchini Uganda.

2. **Udhalimu**

Katika hadithi hii, udhalimu umeweza kubainishwa kupitia kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, nchi ya Uganda imebarikiwa kuwa na rasilimali kubwa ya samaki. Hii ni kutokana na maziwa yaliyopo katika maeneyo hayo kama vile Victoria, Albert, Kyoga na mto Nile (Uk.11). wavuvi na wafanyakazi za sulubu walikuwa ni Waafrika wenyeji. Kwa mfano, Christine anasema, "siku hiyo nilipompitia Peter ofisini, nilimkuta akisimama, wafanyikazi wake wakipakia mizigo katika lori, nje ya ofisi. Hapa alikuwa mnyapara hasa. Aliwatolea wafanyikazi wake amri kwa sauti ya juu." (Uk.19) Wafanyikazi hao hulipwa ujira duni ilhali Peter anapata faida kubwa. Maisha aliyoishi Peter ni ya kifahari yakilinganishwa na ya wale wanaofanya kazi za sulubu. Zaidi ya kujitahidi katika kazi, wanakemewa na kudharauliwa. Wale wenye uwezo wa kifedha wamekuwa waliwanyemelea wasichana wadogo ambao wana ujuzi finyu katika maisha na kuwaingiza katika maisha yasiyokuwa na mwelekeo mzuri. Kwa mfano, Christine bado ni mwanafunzi wa chuo kikuu lakini amekuwa akitumiwa kama chombo cha kudumisha starehe na anasa za Peter kama anavyosema Zac, "Ulimpendeza sana Mzungu huyo" na Christine anapojiuliza "Je, ni kweli Peter alinitaka?" (Uk.14). hayo ni mawazo ya kubabaisha ambayo yamekuwa yakizuga akili za vijana. Kwa sababu hiyo, vijana hao husahau kutilia maanani masomo yao. Kwa mfano, Christine alitawaliwa na Peter, akama aelezavyo, "siku nyingi za ijumaa jioni nilijikuta nikiondoka chuoni kuenda kumtembelea." (Uk.15). kadhalika, watoto ambao hawajazaliwa huavywa kutokana na ukosefu wa utu wa madaktari. Kwa mfano, Christine anapogundua kuwa yu mjamzito anasaidiwa kuto mimba na Margaret. Christine anasema, "Margaret alikuwa muuguzi katika zahanati mojo jijini. Nilipowaeleza nia yangu, hakuna aliyenizuia!" (Uk.17). isitoshe, Wazungu au wenye kujiweza ndio walioweza kupat starehe katika hoteli za kifahari kama vile Entebbe Sailing Club, Sheraton. Kutokana na kunyanyaswa kwa wenyeji, hawakuweza kufurahia matunda ya uhuru.

3. **Shughuli Haramu/Magendo**

Magendo ni shughuli haramu zinazofanywa kinyume cha sheria au maadili.

Miongoni mwa shughuli zisizokuwa za halali ni kama vile biashara ya ubadilishaji wa fedha za kigeni, kuavya mimba, uuzaji wa bangi, ukahaba na mishahara duni kwa wafanyakazi. Peter ambaye anafahamu thamani ya dola, huzipata kimagendo au kwa njia isiyo halali. Kwa mfano, "Jagjit alikuwa amekuja kumuuzia Peter dola za Kimarekani. Hii ilikuwa ni biashara ya magendo. Iliidhinishwa kufanywa tu na

Benki Kuu ya Uganda." (Uk.18). katika biashara hizo, kulikuwa na ulaghai miongoni mwa waliohusika. Kwa mfano, miongoni mwa noti zilizoletwa kwa Peter zilikuwepo bandia. "Nasikitika, hii noti Bwana Jagjit ni bandia" (Uk.18). biashara hizo zilifanywa kwa siri bila ya serikali kufahamu na zilikuwa zikiifilisi nchi hiyo mapato ya ushuru.

Haospitali za serikali nazo zimekuwa zikiendesha shughuli zingine ambazo ni haramu kama vile kuwasaidia wajawazito kuavya mimba. Kwa mfano, Margaret alipojulishwa nia ya Christine ya kuitoa mimba, shughuli hiyo inatekelezwa mara moja. Jambo hilo limebainishwa kupitia kwa maelezo yake Christine kuwa, "mtaalamu' wa unusukaputi wa hapo zahanatini alinidunga sindano. Mwili haukufa ganzi ... alinihakikishia shughuli yote ingekamilika vizuri. Nilielewa fika chochote kingeweza kutokea." (Uk.17). shughuli hizi huweza kuhatarisha maisha ya mtu lakini hakuna anayejali mradi fedha zinatolewa.

Isitoshe, Zac ni mwanafunzi wa chuo kikuu lakini hujihusisha na utafutaji wa mihadarati kama vile bangi. Hii ndiyo sababu ya Peter kumpitia pale kwake.

Aidha, wasichana walishiriki ngono na unywaji pombe wakiwa shuleni, tena bila wazazi wao kujua.

4. **Utabaka katika Jamii**

Katika hadithi hii, mwandishi amewasilisha maisha ya matabaka mawili: matajiri wanaojiweza kiuchumi na lile lipatalo dhiki katika maisha. Tabaka la juu huishi katika mitaa ya kifahari kama vile Tank Hill. Christine anasema, "Zac aliniambia kuwa Peter alitaka tupange tumtembelee nyumbani kwake Tank Hill." (Uk.14). zaidi ya kuishi katika mitaa ya kifahara, watu hao hujipatia fedha nyingi kupitia kwa ulaghai kama vile kuwapunja mishahara wanaowafanyia kazi na pia kushiriki biashara za magendo. Jambo hili limedhihirishwa kupitia kwa uhusiano wa Peter na Jagjit ambaye "...alikuwa amekuja kumuuzia Peter dola za Kimarekani." (Uk.18). kutokana na fedha nyingi walizonazo, watu hao walijiingiza katika anasa na starehe za hali ya juu nyumbani kwao na hata katika mahoteli mashuhuri mjini. Marafiki zao wa dhati ni wale wa tabaka lao. Ikibidi huwaendea watu wa tabaka la chini ili kuwatumia kukamilisha starehe zao. Kwa mfano, Peter anamwendea Zac ili kupata bandi na anaanzisha uhusiano wa kimahaba kama anavyokiri Christine, "mwishowe, nilijikuta kitandani." (Uk.16).

Tabaka la chini limedhihirishwa kupitia kwa wenyeji waafrika. Aghalabu hao wa tabaka la chini huwa ni watumishi wa nyumbani kama vile Deogracias anayefanya

kazi ya “uboi” (Uk.14). watu hao huwa wanafahamu uzandiki na ukosefu wa utu wa matajiri wao lakini hufyata ulimi wasije wakamwaga unga. Kutokana na ufukara unaowaandama, huishi katika mitaa isiyokuwa ya kifahari. Mazingira ya ufukara yamebainishwa kupita kwa chumba cha Zac ambacho ni kidogo na hata vyombo vyake. Kwa mfano, “Zac alifunfua kikabati kidogo cheusi. Akatoa sahani mbili nyekundu za plastiki zilizoonyesha kuwa na mafutafuta...” (Uk.13). Zac hana watumishi kama Peter: anajifanyia mwenyewe kazi za nyumbani. Kulingana na Peter, watu wa tabaka la chini ni wahitaji wa fedha. Anamuuliza Christine, “Unataka pesa?” (Uk.19). katika majumba ya starehe kama vile Half-London, watu wa tabaka la chini hawawezi kuende huko ili k ua kukaribishwa na watu wenye fedha. Katika muktadha huo, matabaka hayo hutengana kama mbingu na nchi. Kadhalika, urafiki wao huwa si wa dhati.

5. **Mapenzi na urafiki**

Uhusiano wa mapenzi na urafiki umeweza kubaininshwa kupitia kwa Zac, Christine, Miriam na Mr. Peter. Kulingana na mwandishi, mahusiano ya wahusika hao hayana mwelekeo mzuri. Kwa mfano, urafiki kati ya Mr. Peter na Zac haukujengeka katika kuridhiana wala kusaidiana. Peter amekuwa akienda kwa Zac ili kujipatia bangi na pia kama pahali pa mawindo ya wasichana. Katika hadithi hii, Christine anasema kuwa: “Jioni moja, tulikuwa tunapiga gumzo chumbani mwa Zac alipofika Peter. Kutokana na tamaa yangu maishani ya kumtafuta mpenzi wa kiume, nilijipata nikiulainisha ujanajike wangu Peter alipoingia.” (Uk.11). kwa hivyo, uhusiano huo ni wa starehe na anasa. Kutokana na hali duni kimaisha, wasichan huwa windo jepesi kwa wenye nacho. Kwa mfano, Peter amependezwa na Christine kwa sababu ni mrembo na pia hatatiliwa doa kwa vile ni msichana mbichi anayesoma katika chuo kikuu cha Makerere. Hata hivyo, mwandishi ana mwelekeo kwamba mahusiano hayo si murua kwa sababu, hakuna kinachofikiriwa isipokuwa starehe na anasa. Peter amekuwa akiwaalika “marafikize” kwenda kwake na kwa majumba ya starehe. Maisha hayo ni ya hatari kwa vile wasichana huhadaiwa na kushika mimba na baada ya hapo uhusiano huo hukatika. Mwandishi anaona kuwa uhusiano huo huendeleza ukosefu wa kimaadili katika jamii. Kwa mfano Dorothy anamweleza dada yake, “Koma kuhusiana na Mzungu huyo.” (Uk.15). kadhalika, Deogracias hakupendezwa na utovu wa kimaadili aliokuwa akiushuhudia. Anaonekana kusema. “...nimewaona wengi kama nyinyi ambao walipitia katika nyumba hii hapo mwanzoni” (Uk.14). Nasaha hizo hazikutiliwa maanani bali alichukuliwa kuwa anaendeleza ujuba. Mwandishi anawataka wenye kujiingiza katika usuhuba usiokuwa maudhui madogo wakome kufanya hivyo.

Maudhui madogo ambayo yanaweza kuzingatiwa katika mijadala ya darasani ni kama vile:

6. **Umuhimu wa Kazi Katika Jamii:**
   Hoja za kuzingatiwa ni:
   a) Uhaba wa kazi katika jamii
   b) Mishahara duni kwa wafanyakazi
   c) Kufanya kazi halali

7. **Unafiki**
   Hoja za kuzingatiwa ni:
   a) Urafiki wa Mr. Peter na Christine
   b) Asili guni yake Mr. Peter
   c) Urafiki wa Mr. Peter na Zac
   d) Uhusiano wa kibiashara kati ya Mr. Peter na Bwana Jagjit (Uk.19)

8. **Ukahaba ba Maradhi Hatari ya Ukimwi**

   Hoja ya kuzingatiwa ni:
   a) Mapenzi ya kiholela kati ya Mr. Peter na Christine
   b) Mr. Peter kuwa na wapenzi wengine (Zingatia anavyosema Deogracias)
9. **Ulevi na anasa**
   Hoja za kuzingatiwa:
   a) Starehe na anasa (Zingatia Zac, Christine, Peter na Miriam)
   b) Zac kumletea Peter wasichana wa chuo kikuu
   c) Mihadarati inayofafutwa na Zac
   d) Uvutaji wa sigara

10. **Utu**
    Hoja wa kuzingatiwa:
    a) Nasaha anazozitoa Deogracias kwa Christine
    b) Nasaha za Dorothy kwa Christine
    c) Nafsi yake Christine inavyomsimanga (Uk.17,19)

Usawiri na Ujenzi wa Wahusika

Katika uwasilishaji wa hadithi hii kumetumiwa wahusika mbalimbali kama vile: Christine,

Mr. Peter, Zac, Mzee Deogracias, Dorothy, Miriam, Margaret, Jagjit and Sunjah Patel.

1. **Christine**

Christine ndiye mhusika mkuu katika hadithi hii. Msichana huyu wa miaka ishirini ni mwanafunzi katika chuo kikuu cha Makerere.

a) *Mpenda raha na anasa*. Anatamani kuwa na uhusiano wa kimapenzi na watu wanaojiweza kifedha. Kwa mfano, anajiuliza kuwa: Je, ni kweli Peter alinitaka? (Uk.14).
b) *Ni kinyago cha mpapure. Hana msimamo dhabiti*. Anataka kuanzisha mahusiano ya kimapenzi ya kiholela. Kwa sababu hiyo kila ijumaa huenda kumtafuta Peter ili wakajivinjari. Amekuwa akitenda haya bila ya kujua kuwa anatumiwa hadi anapochikwa mimba bila kutarajia.
c) *Ni mwoga*. Hawezi kuidhibiti hamu yake ya kujihusisha katika mapenzi. Anapogundua kuwa ni mjamzito, hana ujasiri wa kumweleza mwenzake kuhusu hali hiyo. Badala yake anavya mimba ile. Hii ni kwa sababu alihofu kuwa angemkasirisha mwenzake. Kwa mfano, Peter anamuulizwa Christine, "anapopitia kazini mwake naye. Unataka nini hapa?", anajibu, "Nilikuwa napita tu." (Uk.19.
d) *Mwenye majuto*. Baada ya kuavya mimba anajuta na anakataa pesa ambazo Peter anampa. Nafsi yake ina msimanga mara anapotenda uovu.
e) *Si mwadilifu*. Christine anaamua kuiavya mimba bila kujali yatakayompata. Anafanya mapenzi kiholela. Hazingatii mabusu hadharani, ni utamaduni wa kigeni.
f) *Ni mgumu wa kushauriwa*. Nasaha alizopewa na Dorothy na Deogracias hazikutiliia maanani.

Umuhimu wa Christine

i) Mwandishi amemtumia kama kipasa sauti, kutangaza yaliyoisibu jamii nchini Uganda enzi zile.
ii) Anawakilisha vijana wasomi katika jamii wanaotelekeza masomo yao huku wakishiriki anasa.
iii) Kupitia kwake tunafahamishwa jinsi wazungu wanavyo wadhulumu Waafrika kiuchumi na kihisia.
iv) Uhusiano wake na Mr Peter haumridhishi na mwandishi ametumia kuwaonya vijana dhidi ya kutamani mahusiano na wageni matajiri.
v) Ametumiwa kujenga na kuendeleza maandhui ya ukahaba, ulevi, magendo na kuvunjika kwa maadhili katika jamii.

2. **Mr. Peter (au Mr. Smithson)**

Ni mzungu mwenye asili ya tabaka la chini huko Cockney Uingereza. Hata hivyo hakuipenda nchi ya Uganda na mazingira yake.

a) *Ni mwenye kiburi na dharau*. Aliwadharau waafrika na kuwachukulia kuwa hawana ustaarabu. Anafikiri utu wao unaweza kununuliwa kwa pesa.
b) *Ni laghai*:Amejipata utajiri kutokana na biashara ya samaki kutoka Uganda na pia kwa kujihusisha na biashara haramu ya ulanguzi wa fedha za kigeni na mihadarati.
c) *Mr Peter anapenda mno starehe na anasa*.Kwa mfano;Ana wasichana mbalimbali ambao hustarehe nao.Deogracias ambaye ni mtumishi wake wa nyumba ameonekana kusema, "Nimewaona wengi kama nyinyi ambao walipitia katika nyumba hii hapo mwanzoni"(Uk 14).Kwa hivyo amekuwa akiwabadilisha wanawake katika starehe na anasa zake.Hufanya mapenzi kiholela na wasichana wengi bila kujali maradhi hatari ya ukimwi. Hiyo ndiyo sababu ya kutembelewa na Christine kila ijumaa.Jambo hili linabainika pale ambapo Christine anasema, "Kila ijumaa jioni nilijikuta nikiondoka chuoni kuenda kumtembelea"(Uk15)
d) *Hana utu*. Anapoambiwa kuwa Christine ameavya mimba mara moja anamuuliza, "Unataka pesa?" (Uk.19). kwa hivyo, anaamini kuwa pesa ndio msingi wa maisha. Katika shirika lake la samaki, huwalipa mshahara duni wafanyikazi na kuwakemea.
e) *Ni mlevi*. Anapenda kushiriki ulevi wa vileo na bangi. Hali hiyo inadhihirika anapopanga hafla mbalimbali nyumbani kwake na katika hoteli za kifahari huko Half – London.
f) *Ni msiri mkubwa*. Majina yake halisi hayafahamiki. Kwa mfano, Ugand aanafahamika kama Mr. Peter, huko kwao anafahamika kama Mr. Smithson. Kadhalika, alijihusisha na biashara za siri katika ulanguzi wa fedha za kigeni. Anapotaka kufanya starehe anatalii Kenya na si Kampala anapojulikana.
g) *Huwa makini katika shughuli zake*. Anazikagua dola alizoletewa na Jagjit na kugundua kuwa noti ya dola elfu moja ilikuwa bandia. Akiwa kazini hapendi mzaha inavyobainika katika safari yake Christine. (Uk.19).
h) *Ni mwenye bidii*. Japo biashara zake ni haramu anazifanya kwa bidii. Anaishi katika mtaa wa kifahari, yaani Tank Hill. Ni bayana kuwa alifanya kazi kwa bidii hadi kujiweka katika hali hiyo. Pia ana uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi akiwemo mlinzi. Hii ni kupitia kwa bidii yake biasharani.

Umuhimu wa Mr. Peter

i) Kupitia kwake mwandishi anaonyesha jinsi Ukoloni mamboleo unavyoendeshwa, namna Wakoloni wanavyo wapunja Waafrika.

ii) Mwandishi ametumia uhusiano wake na Christine kama onyo kwa vijana wasitumiwe na watu sampuli hii.
Mwandishi pia ametumia wahusika wadogo kama vile Deogracias, Dorothy, Miriam na Margaret.

3. **Zac**

a) *Ni msomi*. Amesoma hadi msomi chuo kikuu na yu karibu kupata shahada ya B.A. katika somo la fasihi.
b) Ni mwenye dharau na aliyekengeuka. Aliwachukulia wenyeji kama watu duni. Kwa hivyo, alihusiana na watu wa tabala la chini wakati aliopata matilaba yaje yatengenee tu. Huonea aibu Uafrika wake. Kwa hivyo, huzungumza kizungu kwa lafudhi ya Mmarekani mweusi. Picha alizotundika chumbani kwake zilikuwa za Bob Marley na vitabu alivyovihusudu vilikuwa vya "Penguin Classics" vinaashiria haya (Uk.11).
c) Ni laghai. Alishiriki katika biashara haramu ya kuuza bangi.
d) Mpenda raha. Alikuwa mshiriki wa karibu wa Mr. Peter kutokana na uhusiano wao katika sherehe za starehe na anasa. Pia alifanya kazi kwenye kampuni ya Mr. Peter wakati wa likizo ili apate masurufu ya starehe na anasa. Kila mara alikuwa akishiriki ulevi nyumbani kwake na katika majumba ya starehe.
e) Ni kuwadi. Alipenda kuwanasa wasichana kutoka chuoni ili awapelekee watu wenye fedha kama vile Mr. Peter. Ndiye anayetumwa na Mr. Peter kwake Christine. (UK.14)
f) Mwenye matumaini. Yeye kama vijana wengine wenye mwelekeo wake wana matarajio ya maisha makuu siku za usoni lakini hajitahidi katika shughuli muhimu.

Umuhimu wa Zac

i) Kama ilivyone Christine, mwandishi anamtumia kuwakilisha vijana wasomi waliopotoka.
ii) Kupitia kwake, mwandishi anawaonya vijana kuwa wenzao wanaoweza kutia mitego, alivyomfanyia Christine.
iii) Amedhihirisha ukengeushi wa wasomi. Badala ya kujivunia Uafrika wake, anauonea aibu na kuiga mienendo ya kigeni.

4. **Deogracias**

Ni mzee wa makamo mtumishi wake Mr. Peter
a) *Ni mwenye busara.* Atatambua nyendo zisizofaa za tajiri wake na kuwatahadharisha kwa njia isiyo moja kwa moja wasichana walioingia katika

mtego wa Mr. Peter. Kwa mfano, Christine anawaambia wenzake kuwa ujuba wa Deogracias ulielekea kusema, “Nimewaona wengine kama nyinyi” Pia ni kama aliendelea kumwonya kama asemayo Christine, macho yake kila mara yalimuhukumu (Uk.15). hata hivyo, anapuuziliwa. Ni mtu ambaye hataki kutoboa siri ya maisha ya tajiri wake.

b) *Ni mwenye bidii kwa kazi yake.* Kila wakati tunamwona akimhudumia mwajiri wake pamoja na wageni.

5. **Dorothy**

Ni dada yake Christine.

a) Yeye ni mwadilifu. Hapendi kujiingiza katika maisha yasiyofaa kama vijana wa kisasa. Kwa mfano, tunaambiowa”... alikuwa Mkristo aliyeokoka”(Uk15)
b) Ni mshauri.Hakusita kumwelekeza dada yake, anamwambia, “...koma kuhusiana na Mzungu huyo”(Uk15)
c) Ni mwenye mafumbo. Haelezi mambo kinaganaga.Ingawa hutumia sauti ya shime, hatoi ufafanuzi kuhusu kauli zake za busara.Pia badala ya kumweleza Christine moja kwa moja anajua anahusiana na mzungu, anazingia ndoto na Christine anampuuza.

Mbinu za Lugha

Katika hadithi hii kuna matumizi mbalimbali ya lugha katika uwasilishaji.

1.**Tashibihi**

Huu ni ulinganishi wa moja kwa moja kwa kutumia viunganishi;kama, vile mithili ya, sawa na n.k.’

a) Mwili kama wa mwanamke (Uk11)Christine anaeleza jinsi Peter alivyokuwa na mwili mwororo.
b) Alitazama kila kitu kwa makini kama wafanyavyo watalii (Uk 11)Peter alikuwa akikagua chumba uchwara cha Zac.
c) Kicheko kilisikika kama radi(Uk 17)Umati wa watu unamcheka Christine baada ya uhusiano wake na Mr.Peter kudhilifika hadharani.
d) Niliingiwa na wazo la kuwa kama debe tupu(Uk 17).
e) Nikiwa na shahada ningekuwa kama ng’ombe wa Kizungu(Uk17)
f) Aliangalia kwa makini kama mwanasayansi (Uk 18).

g) ....Alimtumbulia macho kama kwamba alikuwa mzuka(Uk.17)
h) Akaviangalia vipande vilivyoraruliwa kama kwamba alitaka kuvinyakua(Uk.19).
i) Nilitembea barabarani kama mtembea-usingizini(Uk.20)

2.**Tashihisi**

Hii ni mbinu ya kuipa vitu visivyo na uhai sifa za kuweza kutenda au kuhisi kama binadamu. Mifano:

a) Springi za kitanda zililalamikia uzito wake wa ziada (Uk.13)
b) Aibu ni hisia wala haina uwezo wa kumvaa mtu.
c) Mvinyo umenipa ujasiri Fulani (Uk.15).
d) Macho yake kila mara yalinihukumu (Uk.15).
e) Wacha ukimwi uwateketeze (Uk.17).
f) Kicheko kilinguruma tena (Uk.17).
g) Mtazamo mwingine wa hali hiyo ukaanza kunishawishi kuwa alitaka kunionyesha macho yao niliyahisi ya kunikashifu (uk.19).
h) Nafsi ilinisuta (uk.19).
i) Jua liliendelea kuadhibu kila kiumbe (Uk.20).

3.**Maswali ya Balagha/ Maswali butu**

Haya ni maswali ambayo hujenga usaili na utafakari katima usomaji wa hadithi. Kadhalika, ni maswali ambayo yanahitaji kutolewa ufafanuzi wa kibinafsi, wala si majibu ya papo hapo. Mifano ni kama vile;

a) Je, ni kweli Peter anamtaka? (Uk.14) Christine alikuwa akitafakari mwaliko wake Mr. Peter, mwandishi anamchochea msomaji kuutafakari uhusiano unaochipuza baina ya wahusika hawa wawili.
b) Na kwa nini Wamisri hao hawakuyaandikia hayo yote? (Uk.15). Swali lake peter ambalo linatudokezea jinsi anavyowadharau waafrika.
c) Kwani Zac alifikiria sikumjua Peter vyema? (Uk.16) Swali analojiuliza Christine ambalo linatudokezea kinaya katika uhusiano wake na Mr. Peter kwa hakika hamfahamu Mr. Peter.

Mifano mingine;

a) Kumbe alikuwa mzungu wa tabaka la chini kwao? (Uk. 16)
b) Ningeendea nini? (Uk.16).
c) Kwani walisoma maandishi ya aibu nguoni mwangu? (Uk.19)

d) Je, ni zawadi alizonipa? (Uk.19).
e) Nafasi ya kumtembelea huko Tank Hill alikoishi? (Uk.19).
f) Uhusiano wetu wa siri? (Uk.19).
g) Au matumaini ya kesho? (Uk.19).
h) Kila mmoja wetu alitaka nini kutoka kwa mwingine? (Uk.19).

4.**Utohozi**

Hii ni mbinu ya kuyaendeleza maneno ya kigeni kwa lugha lengwa. Matumizi hayo yametumika kujenga athari za maisha ya kigeni katika mazingira ya Afrika. Mifano ya maneno yaliyotumiwa ni:

a) Afrika (Uk.11) – Africa
b) Balbu (Uk.11) – Bulb
c) Maprofesa (Uk.11) – professors.
d) Filamu (Uk.13) – film
e) Springi (Uk.13) – spring
f) Gilasini (Uk.13) – glass
g) Kozi (Uk.13) – course
h) Sosholojia (Uk.13) – sociology
i) Uboi (Uk.14) – boy
j) Video (Uk.15) – video
k) Jenerata – generator
l) Plastiki – plastic
m) Denmaki (Uk.16) – Denmark
n) Krismasi (Uk.17) – christimas
o) Mdeni – dane
p) Wikendi – weekend
q) Teksi – taxi
r) Shati – shirt
s) Noti (Uk.18) – note
t) Shilingi (Uk.18) – shilling

5.**Misemo**

Misemo ni mafungu ya maneno ambayo huletwa pamoja kuwasilisha ujumbe maalum. Hutumiwa zaidi ili kuipamba lugha iliyotumiwa.

a) Kumpasulia tabasamu (Uk.13) – Mr. Peter anatabasamu huku akimwelezea Christine njama zake za kumnasa msichana yule.
b) Kupiga funda (Uk.13). kumeza sehemu kubwa ya kinywa kama alivyofanya Christine.

c) Kimya chenye mshindo (Uk.13). msemo iliokita katika methali. “Kimya kina mshindo” kurejelea kimya kilichotawala chumbani walimoachwa Christine na Peter.
d) Macho ya vikombe (Uk.14).

Mifano mingine;

a) Huu ulikuwa ulimwengu uliokuwa mbali na ulimwengu wa nyumbani (Uk.15).
b) Aliniya kimya (Uk.13)
c) Alipasua kicheko (Uk. 15)
d) Alifyata mkia (Uk.16)
e) Sikutaka kukitilia kitumbua chetu mchanga (Uk. 16)
f) Debe tupu (Uk.17)
g) Peter alimpasulia mbarika (UK.18).

6.**Kuchanganya Lugha**

Mbinu hii hutumika pale ambapo mtunzi hutumia mifumo miwili ya lugha katika uwasilishaji wa kazi yake. Aidha, maneno yayo hayo huweza kutumiwa. Kwa mfano:

Hey man (UK.13)

Kauli hiyo imetumiwa wakati Zac alipokuwa akimkaribisha Peter nyumbani kwake. Hata hivyo, imetumiwa kwa maksudi ili kudhihirisha kuwa jamii hiyo imeathiriwa na wageni. Wasomi wamekengeuka kuiga mienendo ya kigeni.

7.**Methali**

Ni kauli ambazo zimekubaliwa katika jamii. Zinapotumiwa huwasilisha hekima na busara ya jamii. Mfano:

Mwiba wa kujidunga ...(Uk.17)

Ingawa methali iliyotumiwa si kamili, ile sehemu ya awali inaashiria sehemu baki. Kwa hivyo, methali yenyewe ni: mwiba wa kijidunga hauna kilio.

Mtindo Katika Uwasilishaji wa Hadithi

1. **Taashira**
   a) Dhana ya “Samaki wan chi za joto” imetumiwa kuashiri njia rahisi za kupata starehe na anasa kupitia kwa wasichana waliopo, uraibu wa aina

mbalimbali kama vile vileo, bangi na kadhalika. Kwa hivyo, walionacho huvua kutoka kwa chuo kikuu cha Makerere.

b) Sangara. Samaki walioletwa na wazungu. (Uk.18) wanawakilisha taathiri potovu zilizoletwa na wazungu barani Afrika. Waafrika walizichangamkia, kumbe zimewaletea maovu na maangamiz tele; hali ambayo ingali inaendelea hata baada ya nchi hizi kupata uhuru, huu ni ukoloni mamboleo. Kwa mfano; wazungu kama Mr. Peter wanawapunja waafrika wakijionyesha kuwa wawafaa kwa kuwapa nafasi za kazi (adimu).

2. Taharuki

Mbinu hii imejengwa kutokana na kauli mbalimbali zilizotumiwa. Mifano:

i) Sadfa ya kuwepo kwa Zac ambaye alijuana na Mr. Peter. Uhusiano wao ulikuwa upi?

ii) Sadfa ya Christine kuja kwa Zac na pia Peter kufika huko kwake. Christine anakiri kutamani uhusiano, je atafanikiwa?

iii) Uja uzito wa Christine. Kunampeleka kwa zahanati ambapo anasaidiwa kuavya mimba.

iv) Kauli alizozitoa mzee Deogracias kwa Christine.

v) Mwandishi hajabainisha wazi hatima ya uhusiano wa Christine na mzungu.

Kwa hivyo kutoka na mifano hii, ni bayana kuwa, sadfa ina mchango mkubwa katika kujenga taharuki katika hadithi hii.

3. Viona Nyuma/Mbinu Rejeshi

i) Hadithi imeanza Christineakiwa kitandani mwa Mr. Peter, kisha tunafahamishwa jinsi walivyokutana na kufahamiana na yaliyojiri baadaye.

ii) Muktadha wa kihistoria umejengwa kuhusu utawala wa kidikteta wa Idi Amin.

iii) Uchumi wan chi ya Uganda ulivyosambaratishwa na uongozi dhalimu.

Katika muktadha huo, ujumbe unaowasilishwa katika hadithi hufafanuliwa kwa uangalifu zaidi.

Mbinu ya ziada zilizotumiwa na mwandishi ni:

a) Istiara

b) Sadfa

c) Mafumbo
d) Usemezano wa nafsi wa mtu na mtu au mtu na watu.